AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

**BARAZA KUU**
**Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Sita**
**12-13 Februari 2025**
**Addis Ababa (ETHIOPIA)**

**EX.CL//Dec.1279- 1309(XLVI)**
Lugha Chanzi: Kiingereza

# MAAMUZI

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI NDOGO ZA KAMATI YA WAWAKILISHI WA KUDUMU (PRC)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** mapendekezo ya PRC kuhusu Ripoti za Kamati zake Ndogo kw kuzingatia ufafanuzi uliotolewa na Nchi Wanachama ;

## I. KUHUSU MKUTANO WA PAMOJA WA KAMATI NDOGO YA USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA WA MASUALA YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA (GSCBFAM) NA WATAALAM WA KIUFUNDI WA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA WATANO (F15)- EX.CL/1548(XLVI)

2. **LINAZINGATIA** Ripoti za PRC na Mkutano wa Pamoja wa Kamati Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala na Wataalamu wa Kiufundi wa F-15.

**Ripoti ya Nusu Mwaka ya Utekelezaji wa Bajeti ya Umoja wa Afrika kwa mwaka 2024**

3. **LINASISITIZA** wasiwasi wa Nchi Wanachama kuhusu viwango vya chini vya utekelezaji wa bajeti na **LINATOA WITO KWA** Kamisheni ya AU na Vyombo vingine vyote vya AU kuhakikisha kuwa wanapanga na kupanga bajeti kiuhalisia kulingana na uwezo uliopo na changamoto zilizopo.

4. **LINAIPONGEZA** Kamisheni kwa juhudi zake zinazoendelea za kuimarisha uwezo wa wafanyakazi wa AU katika Mipango na Bajeti inayozingatia Matokeo, pamoja na mipango yake ya kuboresha utoaji ripoti wa Utekelezaji wa Bajeti katika AMERT na **LINAHIMIZA** dhamira endelevu ya kujenga uwezo katika maeneo haya.

5. **LINAIDHINISHA** jumla ya bajeti ya ziada ya dola za Marekani 23,513,271 kwa mwaka 2024 iliyogawanywa hapa chini:

   a) Bajeti ya uendeshaji ya dola za Marekani 10,834,194, na
   b) Bajeti ya programu ya dola za Marekani 12,679,077

Bajeti ya ziada ya 2024 ni kama ifuatavyo:

   c) Kwa chanzo cha fedha

| Chanzo cha Fedha | Jumla |
|---|---|
| Mfuko wa Akiba wa AU | 14,375,305 |
| Gharama ya Utawala | 3,293,672 |

| | |
|---|---|
| Mchango wa Hiari | 1,129,656 |
| Wabia | 4,714,638 |
| **Jumla Kubwa** | **23,513,271** |

d) Kwa Vyombo na Taasisi:

| Chombo | Uendeshaji | | | | Programu | | | | | Ziada ya 2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mfuko wa Akiba | Michango ya Hiari | Gharama ya Utawala | Jumla | Mfuko wa Akiba | Wabia | Michango ya Hiari | Gharama ya Utawala | Jumla | Uendeshaji | Programu | Jumla |
| AUC | 3,880,872 | - | - | **3,880,872** | 3,022,543 | - | - | 1,275,000 | **4,297,543** | 3,880,872 | 4,297,543 | **8,178,415** |
| PAP | 1,400,000 | - | - | **1,400,000** | - | - | - | - | **-** | 1,400,000 | - | **1,400,000** |
| AfCHPR-Mahakama | - | - | - | **-** | 500,588 | - | 99,996 | - | **600,584** | - | 600,584 | **600,584** |
| ACHPR-Tume | 309,512 | - | - | **309,512** | - | 214,638 | - | - | **214,638** | 309,512 | 214,638 | **524,150** |
| ECOSOCC | 484,622 | - | - | **484,622** | - | - | - | - | **-** | 484,622 | - | **484,622** |
| AUDA-NEPAD | 296,364 | - | 2,018,672 | **2,315,035** | 247,290 | - | 400,000 | - | **647,290** | 2,315,035 | 647,290 | **2,962,325** |
| AUABC | 131,376 | - | - | **131,376** | - | - | - | - | **-** | 131,376 | - | **131,376** |
| PSC | - | - | - | **-** | 250,000 | - | - | - | **250,000** | - | 250,000 | **250,000** |
| APRM | 737,015 | 400,000 | - | **1,137,015** | 307,547 | - | - | - | **307,547** | 1,137,015 | 307,547 | **1,444,562** |
| AFREC | 249,100 | - | - | **249,100** | - | - | - | - | **-** | 249,100 | - | **249,100** |
| Afrika CDC | 156,412 | - | - | **156,412** | - | 4,500,000 | - | - | **4,500,000** | 156,412 | 4,500,000 | **4,656,412** |
| AfCFTA | 627,282 | - | - | **627,282** | - | - | - | - | **-** | 627,282 | - | **627,282** |
| PAU | - | - | - | **-** | 1,631,815 | - | 229,660 | - | **1,861,475** | - | 1,861,475 | **1,861,475** |
| ACSRT | 142,968 | - | - | **142,968** | - | - | - | - | **-** | 142,968 | - | **142,968** |
| **Jumla Kubwa** | **8,415,522** | **400,000** | **2,018,672** | **10,834,194** | **5,959,783** | **4,714,638** | **729,656** | **1,275,000** | **12,679,077** | **10,834,194** | **12,679,077** | **23,513,271** |

6. **LINAIDHINISHA ZAIDI** ugawaji upya wa bajeti kwa mwaka 2024 kama ifuatavyo:

| Chombo/Ofisi | Uendeshaji | Programu | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Nchi Wanachama | Wabia | |
| Kamisheni | 694,874 | (1,610,774) | **(915,900)** |
| PAP | 200,000 | 1,236,898 | **1,436,898** |
| AfCHPR-Mahakama | - | 163,092 | **163,092** |
| AFREC | - | 64,500 | **64,500** |
| IPED | (215,254) | - | **(215,254)** |
| CIEFFA | - | 146,284 | **146,284** |
| AOSTI | (197,277) | - | **(197,277)** |
| AfCDC | 31,740 | - | **31,740** |
| PANASTAT | (129,560) | - | **(129,560)** |
| Kituo cha Uangalizi-Khartoum | (384,523) | - | **(384,523)** |

7. **LINATHIBITISHA** ombi la kubeba bajeti ya dola za Marekani **155,520** kutoka 2024 hadi Machi 31, 2025, kwa ajili ya Sekretarieti ya Mfuko wa Amani, ili kugharamia gharama zinazohusiana na kuajiri Wajumbe wa Kikundi Huru cha Tathmini.

8. **LINAIAGIZA** Kamisheni kutoa taarifa za mara kwa mara kwa PRC kuhusu mchakato wa kuajiri Kikundi Huru cha Tathmini (IEG) unaofanywa na Jopo la Waafrika Mashuhuri.

9. **LINAKUMBUKA** Uamuzi EX.CL/Dec.1265(XLV) wa Julai 2024, ambao uliagiza Kamisheni kufanya upembuzi yakinifu kuhusu pendekezo la kulipa sehemu ya michango iliyotathminiwa katika sarafu za kitaifa, kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za AU. **LINAOMBA** ripoti ya utafiti wa awali iwasilishwe kwa Baraza Kuu mwezi Julai, 2025 kwa ajili ya kujadiliwa.

## Msaada wa mwitikio wa nchi nyingi kwa mlipuko wa *Monkey Pox* barani Afrika

10. **LINAZINGATIA KWA WASIWASI** kuzuka kwa ugonjwa wa *Monkey Pox* katika Nchi Wanachama kadhaa wa AU.

11. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Africa CDC kuhusu kuimarisha Mwitikio wa Nchi Mbalimbali wa Mpox barani Afrika, na ombi la bajeti ya msaada kwa mwitikio wa nchi nyingi kukabiliana na mlipuko wa *Monkey Pox* barani Afrika kutoka kwenye salio la mfuko wa UVIKO-19**.**

12. **LINAKUMBUKA** Uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV) wa Februari 2024 kuhusu uanzishwaji wa Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika ambao ulielekeza kwamba ikiwa hakuna fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya ombi lolote la dharura la ufadhili, Africa CDC kupitia Kamisheni inaweza kupeleka ipasavyo ombi kwa PRC, kwa utaratibu sahihi, kwa kuzingatia hali husika ya kila kesi.

13. **LINAIDHINISHA** fedha za bajeti ya dharura ya **dola za Marekani 10,400,000** ili kusaidia mwitikio wa nchi nyingi kwenye juhudi za *Monkey Pox* kutolewa kwenye salio la fedha za UVIKO-19 na **LINAELEKEZA** Afrika CDC kutoa taarifa ya mara kwa mara kwa Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC).

## Sera ya Usafiri ya AU iliyorekebishwa na Rasimu ya Sera ya Kikao Kazi ya AU

14. **LINAZINGATIA** nyaraka ya Sera ya Usafiri ya AU iliyorekebishwa, na **LINAPENDEKEZA** Mwenyekiti wa AUC kuidhinisha nyaraka hiyo ya Sera.

15. **LINATAMBUA** maendeleo yaliyofikiwa katika utayarishaji wa Sera ya Kikao kazi ya AU na **LINAOMBA** kukamilishwa kwa sera hiyo itakayowasilishwa katika Mkutano wa Kawaida wa Baraza la Kuu mwezi Julai 2025.

**Taratibu za Matumizi na Mchango kwa Mfuko wa Amani**

16. **LINAKUMBUKA** Maamuzi EX.CL/Dec.1240(XLIV) na EX.CL/Dec.1265(XLV), ambapo Kamisheni iliombwa kukamilisha Taratibu za Matumizi na Michango kwa Mfuko wa Amani. **LINAZINGATIA** nyaraka iliyosasishwa, **na LINAPITISHA** Taratibu za Matumizi na Michango kwa Mfuko wa Amani.

**Sera ya Bima ya Umoja wa Afrika**

17. **LINATAMBUA** kuongezeka kwa hatari zinazoletwa na matukio yasiyotarajiwa kama vile dharura za kiafya, uharibifu wa mali, na matukio yanayohusiana na usafiri ambayo yangeweza kuvuruga utendaji wa kawaida wa Umoja wa Afrika. **LINAIOMBA** Kamisheni kuandaa Sera ya Bima ya Shirika la AU ili kutambua, kutathmini, na kupunguza hatari kama hizo kwa ajili ya kujadiliwa na Kamati Ndogo husika za PRC ili iwasilishwe kwa Baraza Kuu mnamo Julai 2025.

**Miradi ya Majaribio ya Mfuko wa Akiba wa Migogoro (CRF) na Mfuko wa Amani wa PAPS kwa mwaka 2025**

18. **LINAIDHINISHA** ombi la kutumia **dola za Marekani milioni 7** kutoka mwaka 2024 kwenda 2025 za CRF, **LINAIDHINISHA ZAIDI** mgao maalum kwa ngazi ya CRF wa **dola za Marekani milioni 10** kwa ajili ya misheni ya baada ya ATMIS mnamo 2025, **AIDHA LINAIDHINISHA dola za Marekani milioni 5** kwa ajili ya Miradi ya Majaribio ya Mfuko wa Amani wa PAPS mwaka 2025, LIKIZINGATIA kwamba shughuli hizi zitafadhiliwa kutokana na mapato ya riba ya Mfuko wa Amani.

19. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya Mfuko wa CRF na Miradi ya Majaribio ya Mfuko wa Amani wa AU pamoja na utoaji taarifa kwa wakati na ulio bora.

**Kuhusu uanzishwaji wa Kitengo cha Uratibu cha G20 na Uendeshaji wa Shirika la Anga la Afrika**

20. **LINAZINGATIA** ripoti za Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Mageuzi ya Kimuundo, pamoja na ripoti ya Mkutano wa Pamoja wa Kamati Ndogo za PRC za Usimamizi na Uratibu wa Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala, Mageuzi ya Kimuundo na Wataalam wa F15.

**21.** **PIA LINAZINGATIA** mapendekezo ya uendeshaji wa Shirika la Anga la Afrika, na uanzishwaji, wa nafasi mbili za kitaalamu ili kusaidia Ofisi ya Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Uchumi, Biashara, Utalii, Viwanda, na Uchimbaji Madini (ETTIM), Mratibu wa Mkutano wa G20 wa sasa kwa muda mfupi.

**22.** **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1275(XLV) wa Julai 2024, ambao uliiomba Kamisheni kuhalalisha uteuzi wa wajumbe waliochaguliwa wa Baraza la Anga la Afrika kwa uamuzi EX.CL/Dec.1256(XLIV) wa Februari 2024, na kuharakisha masuala ya kiutawala na kifedha ili kulifanya shirika hilo kufanya kazi. **PIA LINAKUMBUKA** EX.CL/Dec.1265(XLV) wa Julai 2024 kuhusu pendekezo kutoka kwa Kamisheni la kuundwa kwa Kitengo cha Uratibu cha G20 na kusisitiza umuhimu wa kufuata utaratibu unaofaa katika suala hilo kupitia Kamati Ndogo husika ya PRC.

**23.** **LINAIDHINISHA** bajeti ya dola za Marekani **1,228,798.78** kwa mwaka 2025 kutoka Mfuko wa Akiba wa AU, iliyotengwa kama ifuatavyo:

(i) Dola za Marekani **833,954.26** kwa ajili ya mishahara ya Shirika la Anga la Afrika, na dola za Marekani **178,220** kwa ajili ya mikutano ya kisheria ya Shirika la Anga la Afrika.

(ii) Dola za Marekani **216,624.52** kwa ajili ya mishahara ya nafasi mbili za kitaalamu za G20.

## II. KUHUSU KAMATI NDOGO YA MASUALA YA UKAGUZI - EX.CL/1549 (XLVI)

**24.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi na, **LINAIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake.

**25.** **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1218 (XLIII) aya ya 39, ambao uliiomba Bodi ya Wakaguzi wa Nje (BoEA) kufanya ukaguzi mpana na wa kina juu ya michakato yote ya kuajiri iliyofanyika tangu kuanzishwa kwa Mfumo wa Kuajiri Unaozingatia Sifa (MBRS) na kuripoti kwenye Mkutano wa Kawaida wa Baraza Kuu la Februari 2024 na **LINASISITIZA** kwamba matokeo ya ukaguzi yanapaswa kujadiliwa na Kamati Ndogo husika za PRC na kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Kawaida wa Baraza Kuu wa mwezi Julai 2025.

**26.** **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1189(XLII) aya ya 35(i) na **LINAIPONGEZA** Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi kwa kufanya kikao kazi ili kutekeleza ipasavyo majukumu yake ambayo yanahitaji ujuzi wa kiufundi.

**27.** **LINAZINGATIA** mahitaji ya Viwango Vipya vya Kimataifa vya Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani (IIA) na **LINAIAGIZA** Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi kupitia

Hadidu zake za Rejea kwa kuzingatia mahitaji mapya. Mapitio ya Hadidu za Rejea (TORs) yanapaswa pia kuhakikisha kuwa vipengele vinavyohusiana na Uzingatiaji wa Udhibiti pamoja na Maadili vinajumuishwa kama vinavyofaa kulingana na mahitaji ya utendaji bora.

**28.** **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1126(XXXIX) aya ya 56 (v) na **KUSISITIZA** kwamba OIO inapaswa kuimarishwa na kupata rasilimali za kutosha kwa maana ya wafanyakazi wanaohitajika na bajeti inayohitajika ili kuhakikisha ufanisi wake kulingana na Viwango Vipya vya Kimataifa vya IIA na mbinu bora, na **LINAIAGIZA** OIO kutoa orodha ya nafasi za kipaumbele zilizobainishwa ili zijazwe ifikapo Februari 2026 na **LINAIAGIZA ZAIDI** OIO kutekeleza kikamilifu Viwango Vipya vya Kimataifa vilivyoanza kutumika Januari 2025.

***29.*** **LINAMUOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kupitia Idara za Ufundi kuandaa Ripoti kuhusu Tathmini ya Usimamizi wa Ufanisi wa Udhibiti wa Ndani wa shirika kwa kuitumia vifaa vya Akili Bandia (AI) na kuiwasilisha kwa Vyombo vya Sera kupitia Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi ifikapo mwisho wa kila mwaka, kulingana na mahitaji ya viwango vya kimataifa.

**30.** **LINAUAGIZA** uongozi wa Kamisheni, kila Chombo na Shirika lingine la AU kutoa mipango kazi ya kina kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yote ya ukaguzi ambayo bado hayajakamilika ambayo inapaswa kuwasilishwa kwa OIO kwa ajili ya mapitio, uthibitisho, ufuatiliaji na utoaji ripoti kuhusu hali ya utekelezaji kwa Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi itakayowasilishwa kwenye Mkutano wa Kawaida wa 47 wa Baraza Kuu mnamo Julai 2025.

**31.** **LINAAGIZA ZAIDI** kwamba Ukaguzi wa Ndani na wa Nje unapaswa kuzingatia zaidi mambo ya sasa ili kuongeza thamani kwa shirika, na **LINAISIHI** OIO na BOEA kupanga na kufanya ukaguzi wa wakati halisi (ukaguzi endelevu) kadri inavyofaa na **LINAPENDEKEZA** kwamba tathmini ya utendaji kazi wa Wakaguzi wa Nje na wa Ndani inapaswa kuingizwa katika kazi ya Kamati Ndogo ya Ukaguzi.

**32.** **LINAOMBA** kwamba uratibu unaofaa kati ya menejimenti na Wabia wa Maendeleo ufanyike katika michakato ya ukaguzi wa Fedha za Wabia kwa nia ya kuepuka kurudiwa kwa jitihada. Katika suala hili, pale inapowezekana dhana ya ukaguzi mmoja wa kina na utoaji wa ripoti moja vinapaswa kujadiliwa na kupitishwa, kwa makubaliano na Wabia, ili kuimarisha uaminifu wa ukaguzi na kuongeza imani ya pande zote.

**33.** **LINAUAGIZA** uongozi wa Vyombo vyote vya AU kuchukulia kwa uzito mazoezi ya ukaguzi na kutoa majibu ya uongozi kwa masuala ya ukaguzi na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa Kamati Ndogo ya Masuala

ya Ukaguzi kwa kutumia mipango kazi ya wazi iliyopendekezwa na inayotekelezeka.

**34.** **LINAKUMBUKA** Maamuzi yake EX.CL/Dec.1008(XXXIII) aya ya 17 na EX.CL/Dec.1031(XXXIV) aya ya 11 na **LINAIOMBA** Kamisheni kupitia Kamati ya Uwajibikaji ya Ndani kuhakikisha na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji na kuondoa kutoadhibiwa kwa kufuata sheria na kanuni za AU hasa kwa utekelezaji unaofaa wa mfumo wa vikwazo.

**35.** **LINAIBUA WASIWASI** kuhusu ukosefu wa *Enterprise Risk Management Function* katika AU na **LINAIAGIZA** Kamisheni kusasisha na kukamilisha, mbinu jumuishi na idara zote za Kamisheni na Vyombo vingine vya AU, sera ya usimamizi wa hatari iliyopitishwa mwaka 2017 na kuiwasilisha kwa Vyombo vya sera kwa ajili ya kujadiliwa ifikapo tarehe 30 Juni 2025.

**36.** **LINAIAGIZA** Kamisheni kuimarisha wafanyakazi na uendeshaji wa Kitengo cha Uhakiki Ubora (QAC) ili kuwezesha uratibu katika usimamizi wa hatari na kukuza utamaduni wa uwajibikaji na uwazi ndani ya kamisheni na Vyombo vingine vya Umoja wa Afrika.

**37.** **LINAIDHINISHA** ombi la kubadilisha jina la Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi ili kujumuisha kipengele cha Usimamizi wa Hatari kulingana na mamlaka yake kwa mujibu wa Kanuni ya 96 (3) ya Kanuni za Fedha za AU, na jina jipya lililopendekezwa linalosomeka kama Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi, Usimamizi wa Hatari na Ufuataji wa kanuni.

**38.** **LINAUOMBA** uongozi wa Kamisheni kutoa ripoti kuhusu utekelezaji wa maazimio yaliyopitishwa na Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi katika Kikao kazi chake kilichofanyika mwezi Novemba 2024 huko Adama, kwa PRC, kupitia Kamati yake Ndogo husika ifikapo tarehe 31 Desemba 2025.

**39.** **LINAKUMBUKA ZAIDI** uamuzi wake wa EX.CL/Dec.1233(XLIV) aya ya 52 (ii) ulioiagiza Kamisheni *Kufanya Kikao kazi / Mafunzo Elekezi kwa Nchi Wanachama wote kuhusu masuala ya bajeti na mipango, ukaguzi, usimamizi wa rasilimali fedha na watu ili kuimarisha majukumu yao ya uangalizi* na **LINASISITIZA** kuwa kikao kazi kinapaswa kufanyika ifikapo Novemba 2025.

## III. KUHUSU KAMATI NDOGO YA MAGEUZI YA KIMUUNDO - DOC: EX.CL/1547(XLVI)

**Na**

## IV. KUHUSU MKUTANO WA PAMOJA WA KAMATI NDOGO YA MAGEUZI YA KIMUUNDO, KAMATI NDOGO YA USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA WA MASUALA YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA NA WATAALAMU WA KAMATI YA MAWAZIRI WA FEDHA KUMI NA WATANO (WATAALAMU WA F15) – DOC. EYX.CL/1551(XLVI)

**Kuhusu Mfumo wa Kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika**

**40.** **LINAZINGATIA** ripoti iliyohuishwa kutoka katika CDC Afrika kuhusu kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika;

**41.** **LINAIDHINISHA** Mfumo na kuripoti kuhusu kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika kama Mfuko wa Dhamana, katika kulinganisha na Kanuni za Fedha za Umoja wa Afrika.

**42.** **PIA LINAIDHINISHA** utoaji wa mamlaka wa CDC Afrika ya kusimamia mfumo uliopendekezwa wa Mfuko wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika. **LINAIAGIZA** Africa CDC kutoa ripoti kwa wakati kwa PRC na Kamati zake ndogo husika.

**43.** **LINAIAGIZA** Kamisheni na Africa CDC kufanya ukaguzi wa Mfuko wa UVIKO-19 na kuwasilisha matokeo kwa Kamati ndogo husika za PRC, ili kuongeza uwazi kuhusiana na uhamishaji wa fedha kutoka Mfuko wa UVIKO-19 kwenda katika Mfuko wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko, kwa ajili ya kupelekwa katika Baraza la Mawaziri lijalo mwezi Julai 2025, kupitia PRC;

**Kuhusu kuanzisha Kitengo cha Uratibu cha G20**

**44.** **LINAZINGATIA** pendekezo la Kamisheni la kuanzisha Kitengo cha Uratibu cha G20, pamoja na changamoto zinazohusiana na kuhakikisha uratibu unaofaa wa ushiriki wa UA katika G20, na haja ya kutunza kumbukumbu ya taasisi;

**45.** **LINAPENDEKEZA** kuanzishwa, kwa kipindi cha muda, nafasi mbili (2) za wataalamu ili kusaidia ofisi ya Kamishna ya Idara ya Maendeleo ya Uchumi, Biashara, Utalii, Viwanda na Uchimbaji Madini (ETTIM)/Mwakilishi wa Rais wa sasa wa G20, ambazo ni:

a) Ofisa Sera Mwandamizi – Mratibu wa Masuala ya Fedha (P3, Hatua ya 1)
b) Ofisa Sera Mwandamizi – Mratibu wa Mwakilishi Binafsi wa G20 (P3, Hatua ya 1)

Kwa bajeti ya jumla ya mwaka ya Dola 216,624.52 kwa ajili ya mishahara na marupurupu ya nafasi hapo juu kama hatua ya muda hadi muundo wa kina utakapowasilishwa kwa ajili ya kuidhinishwa kufuatia utaratibu rasmi;

**46.** **LINASISITIZA** umuhimu wa kufuata utaratibu rasmi wa uanzishaji wa Kitengo cha Uratibu cha G20 kupitia Kamati Ndogo husika za PRC na **LINAIOMBA** Kamisheni kuharakisha kumalizika kwa uanzishwaji wa Kitengo hicho ifikapo Julai 2025;

**Kuhusu uendeshaji wa Baraza la Anga la Afrika**

**47.** **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1275(XLV) wa Julai 2024 ambao uliomba Kamisheni kuhalalisha nyaraka za ajira za wajumbe waliochaguliwa wa Baraza la Anga Afrika kwa mujibu wa Uamuzi EX.CL/Dec.1256(XLIV) wa Februari 2024 na kuharakisha vipengele vya utawala na fedha kulingana na muundo wa Shirika ili kulifanya liendeshwe kikamilifu.

**48.** **LINAZINGATIA** masuala yaliyosababisha kuchelewa kuendesha Baraza;

**49.** **LINAZINGATIA** kuwepo kwa kutofuata utaratibu kutokana na kukosekana kwa vigezo vya wazi katika kutaja na kuainisha Wakuu wa mashirika ya AU;

**50.** **LINAREJEA** uamuzi EX.CL/Dec.1265(XLV), aya ya (39) ambao uliiagiza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuandaa pendekezo la mchakato wa kina wa kuweka viwango vya madaraja ya nafasi zote za UA, ikijumuisha Wakuu wa Vitengo vya UA, na kutoa ripoti kwa Vyombo vya Sera vya UA ifikapo Februari 2025; na **LINAELEZA** wasiwasi wake kwa kutopatikana kwa pendekezo lililoombwa; na **LINAIAGIZA** Kamisheni kukamilisha pendekezo hilo ifikapo Julai 2025.

**51.** **LINAPENDEKEZA** hatua za muda mfupi zifuatazo za kuendesha Baraza la Anga Afrika, bila ya kuathiri uamuzi uliotajwa hapo juu:

a) Kumpa Rais daraja la muda SP3 (Hatua ya 5) na Makamu wa Rais daraja la muda la SP3 (Hatua ya 1).
b) Kutoa msaada wa kiuongozi kupitia nafasi nne za nyongeza:
   - Msaidizi Binafsi wa Rais (P3, Hatua ya 5)
   - Msaidizi Binafsi wa Makamu wa Rais (P3, Hatua ya 5)
   - Msaidizi wa Utawala (GSA5, Hatua ya 5) – Nafasi mbili

Kwa bajeti ya jumla ya mwaka ya dola za Marekani 833,954.26 kwa ajili ya mishahara na marupurupu ya nafasi hapo juu na dola za Marekani 178,220.00 kwa ajili ya mikutano iliyopangwa kisheria ya Baraza la Anga Afrika, ikiwa ni jumla ya dola za Marekani 1,012,174.26 kwa ajili ya kuendesha Baraza;

**52.** **LINAIELEKEZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kutoa ripoti ya maendeleo ya uendeshaji wa Baraza la Anga la Afrika kwa Kamati Ndogo ya PRC ya Mageuzi ya Kimuundo.

**53.** **LINAELEKEZA** kwamba mambo yoyote yaliyobainishwa yanapaswa kushughulikiwa kupitia utaratibu unaostahili ifikapo Februari 2026.

**Vipengele vya Jumla**

**54.** **LINASISITIZA** kwamba uidhinishaji huu ni hatua za muda zikilenga kushughulikia mahitaji ya haraka ya uendeshaji;

**55.** **LINASISITIZA** kwamba ajira zote zitafanyika kulingana na Kanuni, Sheria za Wafanyakazi na Mfumo wa idadi ya kikomo (*quota system*) wa UA;

**56.** **LINASISITIZA** kwamba uanzishaji mzuri wa vitengo vyote vipya vya Umoja wa Afrika unapaswa kutekelezwa katika mazingira ya mchakato mpana wa mageuzi ya kitaasisi ya UA.

**57.** **LINASISITIZA** wasiwasi wake mkubwa kuhusu kurudiwa kwa maombi ya bajeti ya ziada, ugawaji upya na uhamishaji, hasa nje ya muda ufaao ulioainishwa katika Sheria na Kanuni za Fedha za AU;

## V. KAMATI NDOGO YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA – DOC. EX.CL/1552(XLVI)

### A. Ubia wa AU - EU

**58.** **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Umoja wa Ulaya (EU) kukubaliana juu ya tarehe inayofaa kufanya Mkutano wa 3 wa Mawaziri wa AU-EU na Mkutano wa 1 wa Kamati ya Ufuatiliaji katika muhula wa kwanza wa 2025, mjini Brussels, Ubelgiji, na kuanza mchakato wa maandalizi mapema iwezekanavyo, kwa kushirikiana na Kikosi cha Kidiplomasia cha Afrika cha Brussels, Ubelgiji.

**59.** **LINAISIHI** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na EU kuhakikisha kwamba ajenda na programu ya kazi ya Kamati ya 1 ya Ufuatiliaji ya Mawaziri wa AU-EU vinazingatia mapitio ya maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Azimio la Brussels la Mkutano Mkuu wa 6 wa AU-EU uliofanyika mwaka 2022.

**60.** **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Kikundi cha Afrika cha Kidiplomasia huko Brussels kuzungumza na EU juu ya haja ya kufanya

Mkutano Mkuu wa 7 wa AU-EU mwaka 2026 na kuhakikisha maandalizi yanayofaa.

**61.** **LINAIOMBA ZAIDI** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, kuanza mchakato wa uchaguzi wa nchi mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 7 wa AU-EU utakaofanyika Afrika kwa uamuzi wa Baraza Kuu, mnamo Julai 2025.

**B. Ubia wa Afrika – Nchi za Kiarabu**

**62.** **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni ishirikiane na Sekretarieti ya Umoja wa Nchi za Kiarabu, kukubaliana tarehe mpya za kufanya Mkutano Mkuu wa 5 wa Afrika na Nchi za Kiarabu.

**63.** **LINAISIHI** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Umoja wa Nchi za Kiarabu, kuendeleza mashauriano yote muhimu kwa ajili ya kukamilisha nyaraka za Kazi za Mkutano Mkuu wa 5 wa Afrika na nchi za Kiarabu.

**C. Mkutano wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD)**

**64.** **LINATOA** shukrani na pongezi kwa Serikali na Watu wa Japan kwa kufanikisha Mkutano wa Mawaziri.

**65.** **LINAIDHINISHA** Taarifa ya Mkutano wa Mawaziri na **KUIOMBA** Kamisheni kwa ushirikiano wa karibu na Japan na Kikosi cha Afrika cha Kidiplomasia, kufuatilia utekelezaji wa haraka wa matokeo ya Mkutano.

**66.** **LINAIOMBA** PRC kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, Kikosi cha Afrika cha Kidiplomasia huko Tokyo, na Serikali ya Japani, kuanza michakato ya maandalizi ya kufanya Mkutano Mkuu wa 9 wa TICAD kwa mafanikio.

**D. Jukwaa la Ushirikiano wa China na Afrika (FOCAC)**

**67.** **LINATOA** Shukrani na kuipongeza Serikali na Watu wa Jamhuri ya Watu wa China kwa kufanikisha Mkutano Mkuu wa FOCAC 2024 uliofanyika Beijing, China, kuanzia tarehe 2 hadi 5 Septemba 2024.

**68.** **LINAKARIBISHA** kupitishwa kwa Azimio la FOCAC 2024 na Mpango wa Kazi wa FOCAC 2025 – 2027 na kuteuliwa kwa Jamhuri ya Kongo kama Mratibu wa upande wa Afrika kwa kipindi hichohicho.

69. **LINAIOMBA** Kamisheni, kwa ushirikiano wa karibu na China na Kikosi cha Afrika cha Kidiplomasia mjini Beijing, kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kazi wa FOCAC wa 2025 – 2027.

### E. Ubia wa Afrika - Uturuki

70. **LINATOA** shukrani na kuipongeza Serikali na watu wa Jamhuri ya Djibouti kwa kufanikisha kuandaa Mkutano wa Tatu wa Mapitio ya Mawaziri wa Afrika- Uturuki uliofanyika Djibouti, tarehe 3 Novemba 2024.

71. **LINAKARIBISHA NA KUIDHINISHA** Taarifa ya Pamoja na Ripoti ya Pamoja ya Utekelezaji wa Mkutano wa Tatu wa Mapitio ya Mawaziri wa Afrika-Uturuki.

72. **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec./1265 (XLV) unaoiomba PRC kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni kubainisha nchi itakayoandaa Mkutano wa Tatu wa Mapitio ya Mawaziri wa Afrika-Uturuki; **LINAKARIBISHA** jukumu la Mwenyekiti wa Baraza Kuu katika kutatua mkwamo kuhusu uandaaji wa Mkutano wa Mapitio wa Mawaziri.

#### Kuhusu Kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa 4 wa Ubia wa Afrika - Uturuki

73. **LINAIOMBA na PENDEKEZA** kwa Mkutano Mkuu, wakati wa Mkutano wake wa Kawaida wa Thelathini na Nane mwezi Februari 2025, kuidhinisha pendekezo la Nchi ya Libya la kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nne wa Afrika-Uturuki mwaka 2026.

74. **LINAIOMBA** PRC kwa kushirikiana kwa karibu na Kamisheni na nchi mwenyeji kukubaliana juu ya tarehe za Mkutano wa Nne (4) wa Ubia wa Afrika-Uturuki na kuanza michakato ya maandalizi kwa ajili ya kufanya Mkutano huo kwa mafanikio.

### F. Ubia wa Afrika na Korea

75. **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa Jukwaa la 5 la Mawaziri wa Korea na Afrika na kuendelea kufanya Mashauriano ya Mwaka ya Sera kwa lengo la kujiandaa kwa Jukwaa la Mawaziri lijalo ambalo litafanyika Afrika mwaka 2026.

76. **LINAIOMBA PIA** PRC kwa kushirikiana kwa karibu na Kamisheni kuanza mchakato wa uchaguzi wa nchi mwenyeji wa Jukwaa la sita la Mawaziri wa Afrika

na Korea, ambalo litafanyika barani Afrika, mwaka 2026 na kukubaliana tarehe za kufanyika Jukwaa hilo.

### G. Ubia wa Afrika na India

**77.** **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, kuzungumza na India ili kukubaliana juu ya tarehe mpya za kufanya Mkutano Mkuu wa 4 wa Afrika na India mwaka 2025.

**78.** **LINAISIHI** PRC, kwa kushirikiana kwa karibu na Kamisheni, Kikosi cha Afrika cha Kidiplomasia cha New Delhi, kuendelea na mashauriano yote muhimu kwa ajili ya kukamilisha Nyaraka za Kazi za Mkutano Mkuu wa 4 wa Afrika na India.

## VI. KAMATI NDOGO KUHUSU NEPAD– DOC. EX.CL/1555(XLVI)

**79.** **LINAZINGATIA** mapendekezo ya PRC kuhusu ripoti ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD;

**80.** **LINAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kazi kubwa inayofanya katika utekelezaji wa Ajenda 2063, na **LINAIHIMIZA** kuongeza juhudi zake katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Miaka Kumi wa Ajenda 2063;

**81.** **LINAIOMBA** Kamisheni na AUDA-NEPAD kuitisha mikutano ya pamoja endelevu na ya mara kwa mara ya upangaji, ufuatiliaji na tathmini kuhusu mipango na miradi mikubwa ili kuboresha na kuimarisha ushirikiano na uratibu katika utekelezaji wa programu za Ajenda 2063, kwa kuzingatia ushirikiano, kuepuka urudufishaji, na ukusanyaji na matumizi fanisi ya rasilimali ili kuongeza athari ya miradi ya bara;

**82.** **LINAZINGATIA** ripoti kuhusu utekelezaji wa uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV) wa Februari 2024 juu ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD na, kuhusiana na hili:

(i) **LINASISITIZA** ombi kwa Kamisheni na AUDA-NEPAD la kuharakisha upembuzi yakinifu kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika kwa Kamati Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Jumla kuhusu Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala; Kamati Ndogo ya Mageuzi ya Kimuundo na kwa PRC kabla ya kuwasilishwa kwa Baraza Kuu kabla au kwenye mkutano wake wa Julai 2025;

(ii) **LINAOMBA** kwamba pendekezo la kufungua ofisi za AUDA-NEPAD katika ngazi ya kitaifa liwasilishwe kwa Kamati Ndogo za PRC zinazohusika (ya Mageuzi ya Kimuundo, na ya Usimamizi na Uratibu wa Jumla kuhusu Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala);

(iii) **LINAKARIBISHA** hatua zilizochukuliwa na Kamisheni kutekeleza Uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV) kuhusu ongezeko la ukomo wa bajeti ya AUDA-NEPAD na Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD;

(iv) **LINAKARIBISHA ZAIDI** hatua zilizochukuliwa na Kamisheni kutekeleza uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV kuhusu mabadiliko ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD kuwa Kamati Ndogo ya Mkutano; ya Nchi Wanachama 55[1];

(v) **LINAZINGATIA** maoni ya Mshauri wa Sheria kuhusu uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV), uliotolewa katika mkutano wake wa 44 mnamo Februari 2024, ambao uliiomba Kamisheni kuchunguza uwezekano wa kuunganisha Kamati Ndogo ya PRC ya NEPAD na Kamati ya Mabalozi kuhusu Ajenda 2063 na kwa kuzingatia uamuzi Assembly/AU/Dec.867(XXXVII, ambao unasema kudumisha muundo wa Kamati ya Mawaziri kuhusu Ajenda 2063 kwa ajili ya utekelezaji bora wa mamlaka yake, kwa hiyo, **LINAPENDEKEZA** kudumisha miundo ya Kamati Ndogo ya PRC ya NEPAD na Kamati ya Mabalozi kuhusu Ajenda 2063 kama ilivyokuwa kwa vile haiwezi kuunganishwa.

(vi) **LINAIOMBA** Kamisheni kukamilisha mchakato wa kuajiri na kupeleka wafanyakazi kwa mujibu wa muundo ulioidhinishwa wa Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD ili kuruhusu kitengo hicho kutekeleza majukumu yake.

**83.** **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kuendeleza mpango wa *WorldSkills Africa* katika mipango yao ya maendeleo ya kitaifa na kikanda na kuiunga mkono Jamhuri ya Zambia kwa ajili ya mashindano yajayo ya WorldSkills yaliyopangwa kufanyika mwaka 2025.

**84.** **LINAIDHINISHA** matokeo ya kikao kazi cha kila mwaka kati ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD na AUDA-NEPAD kilichofanyika kuanzia tarehe 21 hadi 22 Novemba 2024, mjini Johannesburg, Afrika Kusini ili kuimarisha uratibu na ushirikiano kati ya AUDA-NEPAD na Idara/Kurugenzi husika za Kamisheni kwa matokeo bora ya utekelezaji.

**85.** Kwa kuzingatia Hadidu za Rejea za Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD**, LINAIOMBA** AUDA- NEPAD:

(i) kutoa taarifa za mara kwa mara kwa kushirikiana kwa karibu na Kamisheni kuhusu mipango ya kimkakati na shughuli na programu zinazoendelea za Ajenda 2063 kwa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD;

(ii) kuripoti mara kwa mara kwa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD juu ya shughuli zilizofanywa katika utekelezaji wa mamlaka yake, ikiwa ni pamoja na

[1] Reservation expressed by a Member State

utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu na utawala wa NEPAD kuhusu NEPAD kabla ya kuwasilishwa kwa miundo na vyombo vya sera husika vya AU;

(iii) kuwasilisha ripoti yake ya mwaka na nyaraka nyingine muhimu kwa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD, kabla ya kupitishwa na miundo ya Utawala ya NEPAD;

(iv) kuwasilisha kwa ajili ya kujadiliwa rasimu ya pendekezo la bajeti kwa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD kabla ya kujadiliwa na Kamati Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala.

**86.** **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1260(XLIV) uliotolewa Februari 2024; **LINAPENDEKEZA** kwa Mkutano Mkuu kuzingatia kuitisha Mkutano Maalumu kuhusu ufadhili wa Ajenda 2063 ya AU, ili kuhamasisha utashi unaohitajika wa kisiasa ili kukabiliana na changamoto za ufadhili na kuhakikisha kuwa Ajenda 2063 inafanikiwa, wakati wa mwaka 2025.

## VII. KAMATI NDOGO KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, DEMOKRASIA NA UTAWALA (HRDG) – DOC. EX.CL/1557(XLVI)

**87.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli za Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala (HRDG) kwa kipindi cha Januari-Desemba 2024;

**88.** **LINAZINGATIA** kuwasilishwa kwa Ripoti ya Nchi iliyoridhia Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (ACDEG) kulikofanywa na Togo na Rwanda, utambuzi uliofuata na **LINAHIMIZA** Nchi zote Wanachama kuridhia, kuingiza kwenye mipango ya ndani, kutekeleza, na Kutoa ripoti kuhusu mkataba huu;

**89.** **LINATAMBUA** muunganiko wa Haki ya Maendeleo na Maliasili **LINAKARIBISHA** uthibitishaji wa kaulimbiu ya Ripoti ya Utawala wa Afrika ya 2025, ambayo itazingatia "**Utawala wa Maliasili barani Afrika**", iliyoandaliwa na Mfumo wa Kujifanyia Tathmini wa Afrika (APRM) kwa niaba ya Jukwaa la AGA-APSA;

**90.** **LINATAMBUA** jukumu muhimu la AU-ECOSOCC katika kuunga mkono utawala wa kidemokrasia na **LINAIOMBA** Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama, wakati ikikamilisha vigezo vya kuchagua washiriki katika Jumbe za Waangalizi wa Uchaguzi za AU (AUEOM) kuendelea kujumuisha AU-ECOSOCC katika AUEOM;

**91.** **LINAPONGEZA** kazi ya ACERWC na kuunga mkono Kamati ya Mtoto kurekebisha Ibara ya 5(1) ya Itifaki inayoanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR) ili kuwezesha kufikia Mahakama ya Afrika ya Haki

za Binadamu na Watu (HRDG); hata hivyo, Kamati Ndogo ya HRDG inahitaji kuwa na mashauriano endelevu kuhusu suala hilo;

**92.** **LINAZINGATIA** kazi inayoendelea ya Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (PAPS) kuhusu hali ya mradi wa Uingizaji wa ACDEG katika mitaala ya Shule na **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama wote kusaidia mradi huu kwa kuufanya kuwa sehemu ya programu zinazoendelea za Elimu ya Uraia katika ngazi ya Taifa;

**93.** **LINATAMBUA** umuhimu wa uendeshaji wa Taasisi ya Haki za Binadamu ya Afrika (PAHRI), **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1032(XXXIV) wa Mkutano wake wa Kawaida wa 34 uliofanyika Februari 2019, kuhusu kusitisha kuunda vyombo vipya na hatua za kubana matumizi ya bajeti ya AU. **LINAISIHI** Kamisheni kufanya kazi na Vyombo vya AU kama vile Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), Kamati ya Afrika ya Wataalamu wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACERWC), Chuo Kikuu cha Afrika (PAU) na wadau wengine kufungamanisha mamlaka;

**94.** **LINAKUMBUKA** uamuzi AU/Dec.631 (XXVIII) wa Mkutano wa Kawaida wa 28 wa Mkutano Mkuu unaoielekeza APRM kuunga mkono Nchi Wanachama wa AU katika uwanja wa Ukadiriaji wa Mikopo na **LINATOA WITO** wa kuendelea kuunga mkono katika uendeshaji wa Wakala wa Ukadiriaji wa Mikopo Afrika (AfCRA), kama Taasisi inayoendeshwa na sekta binafsi, inayojiimarisha, na **LINAHIMIZA** Nchi zote Wanachama kutumia huduma zake.

**95.** **LINASISITIZA** kuendelea kuunga mkono mamlaka ya Bunge la Afrika (PAP) na Mpango Mkakati wake uliopitishwa hivi karibuni. **LINAELEZA WASIWASI** juu ya uridhiaji wa polepole wa Itifaki ya Malabo inayoipa PAP mamlaka kamili ya kisheria na **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuridhia Itifaki ya Malabo;

**96.** **LINATAMBUA ZAIDI** haja ya msaada thabiti wa kifedha kwa Kamati Ndogo ya PRC ya HRDG na Jukwaa la AGA-APSA pamoja na Sekretarieti ya AGA-APSA ili kuhakikisha ufanisi. **LINASISITIZA** haja ya kuwekea kipaumbele kwa makini mipango ya kuboresha ugawaji wa rasilimali na manufaa yanayoweza kupatikana kwa ushirikiano bila ushawishi wowote usiofaa juu ya mamlaka ya Umoja wa Afrika na ufadhili wote wa nje lazima ujumuishwe katika bajeti ya AU na unapaswa kuwa chini ya uangalizi wa Nchi Wanachama;

**97.** **LINAIOMBA** Kamisheni kuchunguza na kutoa ripoti juu ya uwezekano wa kuunganisha Mfuko wa Utawala wa Afrika kama sehemu ya Mfuko wa Amani wa AU kupitia Baraza la Amani na Usalama (PSC) kwa mwongozo zaidi kutoka kwa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Amani na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za fedha kutatua vikwazo vya bajeti vya Kamati Ndogo na Jukwaa la AGA-APSA;

98. **LINAZINGATIA** kazi iliyofanywa na Wajumbe wa Jukwaa la AGA-APSA kuhusu Uoanishaji wa Michakato ya utoaji ripoti wa Nchi kuhusu Hati za Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala na kuahidi kuunga mkono mpango huu muhimu, kwa kutambua uwezo wake wa kurahisisha taratibu za kuripoti za nchi kwa manufaa ya Nchi Wanachama na Umoja wa Afrika. **AIDHA LINAIOMBA** Sekretarieti ya AGA-APSA kuwezesha maoni kuhusu upembuzi yakinifu wa mpango huu na kuendelea na mazungumzo na wadau wote ili kuhakikisha makubaliano;

99. **LINAIDHINISHA** pendekezo la Ripoti kuhusu Jukwaa la AGA-APSA kuwa ajenda ya peke yake wakati wa Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka (MYCM) na linapendekeza Jukwaa hilo kufanya kazi na Kamati ya Maandalizi ya AU-RECs ili kuhakikisha kipengele hicho cha ajenda kinaakisiwa;

100. **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV) ambao uliamua mwaka 2025 kuwa "Mwaka wa Haki za Kibinadamu, Demokrasia na Utawala Barani Afrika" na **LINAPENDEKEZA** uamuzi huu uendelee kwenye miaka ijayo.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI MAALUMU ZA KITAALAMU (STCs) NA MIKUTANO MINGINE YA MAWAZIRI

**Baraza Kuu,**

1. **LINAPOKEA** Ripoti za Kamati Maalumu za Kitaalamu (STCs) na Mikutano Mingine ya Wizara;

2. **LINAREJELEA** uamuzi EX.CL/Dec.1032(XXXIV) kuhusu kusitishwa kwa uundwaji wa mashirika na ofisimpya;

3. **LINASISITIZA** kuwa uamuzi uliopo haupaswi kuwa na athari zozote za kifedha, kisheria na kimuundo kwa AU na **LINATOA WITO ZAIDI** kwa STCs na mabaraza yote ya mawaziri na vikao vyote vya ufundi kuacha kupitisha miundo au bajeti ambayo haikuzingatiwa na vyombo vya sera kupitia mchakato unaostahili;

4. **LINAZIOMBA** STCs zote kuzipitisha Ripoti zao mwishoni mwa vikao vyao.

### I. MKUTANO WA 5 WA KAWAIDA WA STC KUHUSU MAENDELEO YA JAMII, KAZI NA AJIRA (STC SDLE-5) - Doc. EX.CL/1558(XLVI)

5. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano wa Kawaida wa Tano wa STC ya Maendeleo ya Jamii, Kazi na Ajira ya Umoja wa Afrika (STC-SDLE5), uliofanyika Addis, Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 29 Julai hadi 02 Agosti 2024 na mapendekezo yaliyomo;

6. **LINAIPONGEZA** Kamisheni kwa juhudi zake muhimu ilizozifanya ili kuendeleza ukuzaji wa ukuaji wa Afrika na maendeleo ya kiuchumi kwa kuhamasisha ushirikishwaji wa raia na kuongezeka kwa ushirikiano wa mataifa ya Afrika. **LINAPONGEZA** hali ya sasa ya utekelezaji wa Mpango wa Pamoja wa Utawala wa Uhamiaji wa Wafanyakazi kwa Ushirikiano na Maendeleo barani Afrika (JLMP) uliopitishwa Januari 2015, kupitia uamuzi **Assembly/AU/Dec.6(XXIV).**

7. **LINAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/20(XXIV) ulioidhinisha kuundwa kwa Kamati ya Ushauri ya Uhamiaji wa Wafanyakazi wa Afrika ya sehemu tatu ya AU LSAC. **LINAZINGATIA** mabadiliko ya mara kwa mara, yanayohitaji marekebisho ya ulinzi wa haki za wafanyakazi kwa kuzingatia mwelekeo na taratibu za sasa za kazi na ajira ikiwa ni pamoja na kuongeza manufaa ya AfCFTA,

8. **LINAIDHINISHA** masuala yafuatayo bila athari za kifedha, kisheria na kimuundo:

(i) Mkakati wa Haki na Maadili kwenye Kuajiri barani Afrika
(ii) Kuongeza mamlaka ya LMAC na kuundwa kwake upya kuwa Baraza la Kazi na Ajira la Afrika (ALEC)
(iii) Azimio kuhusu Ulinzi na Uendelezaji wa Haki za Wafanyakazi Wahamiaji

(iv) Miongozo kuhusu Uandaaji wa Mpango/Mfumo wa Mfano wa Ustawi wa Wahamiaji
(v) Mkakati wa Ajira kwa Vijana wa AU/ILO kwa Afrika (YES-Africa)
(vi) Mkakati na Utekelezaji wa Mpango wa Uchumi wa Kijamii na Mshikamano wa Umoja wa Afrika wa miaka 10 (2023-2032)
(vii) Mikakati ya Umoja wa Afrika kuhusu Kukomesha Ndoa za Utotoni na Kutokomeza Ukeketaji (2024 – 2030)
(viii) Mwongozo wa Uwajibikaji wa Umoja wa Afrika kuhusu Kutokomeza Vitendo vyenye Madhara
(ix) Mpango wa Utekelezaji na Mkakati dhidi ya Unyonyaji na Unyanyasaji wa Watoto Mtandaoni
(x) Sera ya AU ya Kulinda Mtoto

9. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutenga kiasi kikubwa na cha kutosha cha rasilimali za bajeti kwa ajili ya mipango inayolinda haki za watoto barani Afrika, kwa kuzingatia zaidi watoto walio katika mazingira hatarishi hasa dhidi ya mila potofu, unyonyaji na unyanyasaji wa watoto mtandaoni, na aina zote za ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto, watoto wanaohama na wale wanaohusika katika utumikishwaji wa watoto, ajira za kulazimishwa, biashara haramu ya binadamu na utumwa wa kisasa kwa mujibu wa Mpango wa Utekelezaji wa AU kuhusu Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Utumwa wa Kisasa Barani Afrika (2020-2030), Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto na Protokali ya Maputo - Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake barani Afrika.

10. **AIDHA LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuharakisha hatua za kuimarisha uhamiaji wenye ufanisi na wenye tija wa wafanyakazi, uhamaji huru wa wafanyakazi ili kuimarisha utangamano wa kiuchumi wa kikanda na ushirikiano ikiwa ni pamoja na uratibu wa kikanda ili kukabiliana na vitendo vya kuvuka mipaka vinavyohusiana na ukeketaji na ndoa za Utotoni.

11. **LINATOA WITO ZAIDI** wa utekelezaji na uwajibikaji katika ngazi ya nchi, pamoja na kuongeza juhudi za kuongeza uelewa katika ngazi pana zaidi, ikiwa ni pamoja na kukuza elimu bila malipo ili kukabiliana na mila potofu.

12. **LINAZIHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kujumuisha uzoefu wa wanadiaspora katika kuboresha mikakati ya kuajiri na kuanzisha mipango ya ulinzi kwa wahamiaji.

13. **LINATOA WITO** wa kuimarishwa kwa ukusanyaji wa data na upashanaji taarifa ili kufanya maamuzi sahihi, kurekebisha afua ipasavyo na kupima maendeleo kwa usahihi katika kukomesha ukeketaji.

14. **LINATOA WITO ZAIDI** wa "Kutokomeza Vitendo Vyenye Madhara" kuteuliwa kuwa kaulimbiu ya Mwaka wa Umoja wa Afrika ifikapo 2030, kwa kufuata taratibu za AU.

15. **LINAUPONGEZA** uongozi wa Kamisheni katika kuunga mkono Nchi Wanachama wake katika kuanzisha na kuzindua mchakato unaoongozwa na serikali wa **Afrika-**

**GCC**, **Mazungumzo ya Lebanon na Jordan kuhusu Uhamiaji wa Wafanyakazi (mazungumzo ya Doha)** ili kuendeleza haki na ustawi wa wahamiaji wa Kiafrika ikiwa ni pamoja na katika nchi za Ghuba na **LINATHIBITISHA** kanuni ya mzunguko inayoangazia kwamba Uenyekiti wa mazungumzo ya Doha utakuwa kwa awamu kati Afrika na nchi za Ghuba.

**16.** **LINAIOMBA** Kamisheni:

(i) **Kuunda** timu iliyojitolea ndani ya Sekretarieti kwa uthibitishaji wa wajumbe wa Nchi Wanachama kabla ya mkutano bila athari za kifedha, kisheria, na kimuundo, kuwasilisha ripoti ya utambulisho katika vikao vijavyo, na **Kuhakikisha** mashauriano ya Washirika wa Kijamii kuhusu kuunda uongozi wa STC.

(ii) **Kuongeza** mamlaka ya Kamati ya Ushauri kuhusu Uhamiaji wa Wafanyakazi wa Umoja wa Afrika na **kuigeuza kuwa** Baraza la Kazi na Ajira la Afrika (ALEC). Kutengeneza Sheria na Masharti yafaayo na kuyawasilisha ili kujadiliwa wakati wa STC inayofuata kuhusu Maendeleo ya Jamii, Kazi na Ajira.

(iii) **Kuendelea na usambazaji** wa JLMP ya bara na kuimarisha ushirikiano na washirika ili kutoa msaada kwa Nchi Wanachama na RECs kuhusu uhamiaji wa wafanyakazi.

(iv) **Kuwezesha** msaada wa kitaalamu kwa Nchi Wanachama katika uanzishaji wa uchunguzi wa kufuatilia maendeleo ya mipango ya SSE katika ngazi ya kitaifa, wakati kusitishwa kwa uanzishaji wa miundo mipya kutakapoondolewa.

(v) **Kutoa** msaada wa kitaalamu kwa Nchi Wanachama kuhusu kujumuisha Uchumi wa Kijamii na Mshikamano (SSE) katika sera zao za kitaifa zilizoundwa baada ya Mkakati wa AU wa miaka 10 wa SSE.

(vi) **Kusaidia** Nchi Wanachama kuanzisha/kuimarisha mifumo jumuishi ya taarifa za soko la ajira kwa ajili ya kupanga kuhusu ujuzi, kulinganisha na kupanga mahitaji ya ujuzi wa siku za usoni ikiwa ni pamoja na kuoanisha mifumo ya kufuzu kwa ujuzi.

(vii) **Kutoa zaidi** msaada wa kitaalamu kwa Nchi Wanachama na RECs katika kuzindua na kutekeleza Mwongozo wa Uwajibikaji wa AU wa Kuondoa Vitendo Vyenye Madhara.

(viii) **Kuwezesha** juhudi za ushirikiano baina ya mashirika ili kuwezesha mikutano ya pamoja na mijadala miongoni mwa Mashirika na Nchi Wanachama wa AU, na uimarishaji wa ubia wa Kikanda.

(ix) Kuimarisha msaada kwenye utekelezaji wa hati zote za AU zilizopitishwa na STC-SDLE5 uliofanyika tarehe 29 Julai hadi 02 Agosti 2024.

## II. MKUTANO WA KAWAIDA WA 5 WA STC KUHUSU AFYA, LISHE, IDADI YA WATU NA UDHIBITI WA DAWA - Doc. EX.CL/1559(XLVI)

**17. LINAWAPONGEZA** Mawaziri wenye dhamana ya Afya, Idadi ya Watu na Udhibiti wa Dawa kwa kufanikisha Mkutano wa Kawaida wa 5 wa STC ya Afya, Idadi ya Watu na Udhibiti wa Dawa (STC-HPDC-5).

**18. LINAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano wa Tano wa STC-H kuhusu Afya ya Idadi ya Watu na Udhibiti wa Dawa uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia kuanzia tarehe 5 hadi 9 Agosti 2024 na mapendekezo yaliyomo;

**19. LINAIDHINISHA ZAIDI** ripoti na nyaraka zifuatazo bila athari za kifedha, kisheria na kimuundo:

(i) Hadidu za Rejea kwa Kinara wa Afya ya Jamii barani Afrika
(ii) Hadidu za rejea kwa Kamati ya Kitaalamu ya Ushauri wa Afya ya Uzazi, Uzazi, Watoto Wachanga, Watoto na Vijana Barani Afrika.
(iii) Hadidu za rejea za Kikosi Kazi cha AU kuhusiana na Afya na Fedha
(iv) Andiko Dhana kwa ajili ya Mkakati wa Uhamasishaji na Mawasiliano wa Bara wa NCD
(v) Ripoti ya Mkutano wa 14 wa Kikosi Kazi cha Afrika kuhusiana na Maendeleo ya Chakula na Lishe (ATFFND).
(vi) Mkakati wa Uhamasishaji na Mawasiliano kuhusiana na Lishe 2024-2028
(vii) Kujadili Mpango Mkakati wa Kuzuia na Kudhibiti Upungufu wa damu barani Afrika
(viii) Andiko Dhana - Maendeleo ya Mkakati wa Lishe wa Kanda ya Afrika 2026-2035 na Mpango wa Vijana
(ix) Tafiti kuhusu Gharama za Chakula na Lishe Barani Afrika (COFAN).
(x) Mwongozo wa 2030 wa Kuendeleza Mapambano dhidi ya UKIMWI, Kuhakikisha Kuimarishwa kwa Mifumo na Usalama wa Afya kwa Maendeleo ya Afrika.
(xi) Mkakati wa Afya wa Kidijitali wa AU (2024-2030)
(xii) Ripoti ya Maendeleo ya utekelezaji wa Azimio la Addis Ababa kuhusu Chanjo (ADI) na Kadi za alama za (ADI)
(xiii) Ripoti ya 2023 kuhusu Mtandao wa Afrika Kuhusu Magonjwa na Matumizi ya Dawa
(xiv) Ripoti kuhusu Kujumuishwa kwa Viongozi wa Kimila katika Kupunguza Mahitaji ya Dawa Barani Afrika

(xv) Ripoti ya utekelezaji wa mapendekezo ya mkutano wa STC ya Afya, Idadi ya Watu na Udhibiti wa Dawa (STC-HPDC-4) uliofanyika Juni 2022.

(xvi) Ripoti ya Mapendekezo ya Mkutano wa Wataalamu Washauri wa Bara kuhusu Kupunguza Mahitaji ya Dawa uliofanyika tarehe 06-07 Novemba 2023, Lusaka, Zambia.

(xvii) Ripoti ya Mapendekezo ya mkutano wa Wataalamu Washauri wa Bara kuhusu Kupunguza Usambazaji wa Dawa uliofanyika tarehe 19-21 Julai 2023, Abidjan, Cote d'Ivoire.

(xviii) Ripoti kuhusu Rasimu ya Msimamo wa Pamoja wa Afrika kwa ajili ya mapitio ya katikati ya muhula wa Azimio la Mawaziri la 2019 kuhusu uimarishaji wa hatua katika Ngazi za kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili Kuharakisha utekelezaji wa Ahadi za Pamoja za kushughulikia na Kukabiliana na Tatizo la Dawa za Kulevya Duniani.

(xix) Azimio la Ngazi ya Juu la Mkutano wa Lusaka kuhusu kushughulikia matumizi ya dawa za kulevya na matatizo yanayohusiana na afya ya akili miongoni mwa vijana, wanawake na watoto.

(xx) Azimio la Kwanza la Jukwaa la Vijana la Umoja wa Afrika kuhusu Kuzuia Matumizi ya Madawa ya Kulevya (2023)

(xxi) Majadiliano kuhusu Hatua Zinazofuata Kuelekea Uandishi wa Mpango wa Utekelezaji wa Umoja wa Afrika kuhusu Kudhibiti Madawa ya Kulevya na Kuzuia Uhalifu (2026-2030)

(xxii) Ripoti kuhusu Mapendekezo Bunge la Afrika (PAP) kuhusu kukabiliana na janga la matumizi mabaya ya dawa kama kikwazo cha ujifunzaji jumuishi, wa maisha yote, bora na muhimu katika Afrika.

(xxiii) Azimio dhidi ya Bidhaa za Tiba Zisizo ubora na Zilizoghushiwa, na kiambatisho chake kuhusu Hadidu za rejea za Kinara wa mapambano dhidi ya Bidhaa za Tiba Zisizo ubora na Zilizoghushiwa barani Afrika.

(xxiv) Ripoti ya Maendeleo ya Uoanishaji wa Udhibiti wa Dawa barani Afrika (AMRH) ili Kujenga Msingi Madhubuti wa Kitaalamu kwa AMA.

(xxv) Ripoti ya Maendeleo ya Kuimarisha Mifumo ya Uangalizi wa Dawa chini ya Mpango wa AU-3S

(xxvi) Ripoti kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Programu Jumuishi ya Usimamizi wa Wadudu wasambazao magonjwa (IVM)

(xxvii) Sheria ya Mfano Iliyosasishwa ya Umoja wa Afrika kuhusu Udhibiti wa Bidhaa za Tiba

(xxviii) Ripoti ya maendeleo ya Kuoanisha Udhibiti wa Dawa barani Afrika (AMRH) ili kujenga msingi thabiti wa kitaalamu kwa AMA.

(xxix) Ripoti kuhusu Kuimarisha Mifumo ya Uangalizi wa Dawa chini ya Umoja wa Afrika - Mpango wa Ufuatiliaji Madhubuti wa Usalama (AU-3S)

**20.** **LINAIOMBA** kamisheni, bila athari za kimuundo, kifedha na kisheria:

(i) Kuwezesha ufunguzi wa ofisi ya mawasiliano ya programu huko Vienna, Austria ili kuwezesha mazungumzo na Ofisi husika za Umoja wa Mataifa kama vile Ofisi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Madawa ya Kulevya na Uhalifu, na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, pamoja na Kundi la Afrika;

(ii) Kuandaa mpango wa utekelezaji wa dawa wa bara uliofanyiwa maboresho ili kuchukua nafasi ya Mpango wa Utekelezaji wa Umoja wa Afrika wa Kudhibiti Madawa ya Kulevya na Kuzuia Uhalifu (2019-2023) ambao muda wake wa utekelezaji uliongezwa hadi 2025 na STC-HPDC4;

(iii) Pia kuandaa kijitabu/mwongozo kwa viongozi wa kimila ili kushughulikia matatizo ya matumizi ya dawa na matatizo yanayohusiana na afya ya akili katika ngazi ya jamii;

(iv) Kuweka pamoja orodha ya mtaala wa kuzuia dawa unaolingana na umri unaolingana na ushahidi ili kutekelezwa na Nchi Wanachama;

(v) Kuanzisha programu ya AU ya mafunzo kwa vitendo/kujitolea kwa vijana katika kudhibiti dawa za kulevya na kuzuia uhalifu;

(vi) Kuanzisha pia Kikosi cha Vijana cha Kitaifa cha Kuzuia Matumizi ya Madawa ya Kulevya katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika;

(vii) Kusaidia Maendeleo ya Mtandao wa Wataalamu wa Afrika kwa ajili afya ya kidijitali ili kusaidia nchi wanachama kuandaa masuluhisho ya afya ya kidijitali ya ndani ya nchi yenye miongozo na viwango vilivyo wazi na;

(viii) Kuwasilisha Sheria ya Mfano Iliyoboreshwa ya Umoja wa Afrika kuhusu Udhibiti wa Bidhaa za Tiba kwa STC kuhusu Haki na Masuala ya Kisheria kwa kujadiliwa zaidi na kupitishwa.

## III. MKUTANO WA 5 WA KAWAIDA WA STC YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UVUMBUZI (STC-ESTI 5) – Doc. EX.CL/1560(XLVI)

**21.** **LINAPOKEA** Ripoti ya Mkutano wa Kawaida wa 5 wa STC kuhusu Elimu, Sayansi na Teknolojia (STC-EST 4) uliofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 8 Novemba 2024;

**22.** **LINATHIBITISHA TENA** utashi wake katika mabadiliko ya mifumo ya elimu na ukuzaji ujuzi barani Afrika;

**23.** **LINATAMBUA** mafanikio katika utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2024;

**24.** **LIKIFAHAMU** changamoto nyingi na ngumu zinazokabili mifumo ya elimu ya Afrika, TVET, na STI, ambazo zinahitaji muda zaidi kushughulikiwa kwa ukamilifu;

**25.** **LINAREJEA** Uamuzi wake EX.CL/1417 (XLII) mnamo Februari 2023 kuhusu Azimio la Mawaziri la Algiers kuhusu biashara changa barani Afrika ambamo Baraza

liliamua kujumuisha maendeleo ya biashara changa katika shughuli za Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, na Uvumbuzi;

**26.** **LINAZINGATIA** kwa kuridhika kuitishwa kwa Mkutano wa Pili wa Afrika kuhusu Biashara Changa kuanzia tarehe 5 hadi 7 Desemba 2023, mjini Algiers na **LINAKARIBISHA** juhudi za Serikali ya Algeria katika kukuza maendeleo ya Afrika, pamoja na matokeo ya mkutano huu, hasa Azimio la Mawaziri la Algiers juu ya biashara changa na pendekezo la Mkataba wa Afrika wa Kubadilisha uhamaji wa wataalamu;

**27.** **LINAIDHINISHA** Azimio la Mawaziri la Algiers kuhusu Maendeleo ya makampuni machanga ya Kiafrika, lililoidhinishwa katika Mkutano uliotajwa hapo juu, ambao unalenga kukuza mazingira wezeshi kwa ukuaji wa makampuni machanga katika Afrika;

**28.** **LINAIPONGEZA** Kamisheni kwa kuunda mikakati mitatu ya Bara ambayo itatoa mifumo ya kuhuisha elimu, sayansi, teknolojia na ubunifu katika muongo ujao: yaani Mkakati wa Elimu ya Bara la Afrika (CESA 2025-34), Mkakati wa Bara wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (CTVET 2025-2034) na Mkakati wa Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kwa ajili ya Afrika (STISA 2025-2034);

**29.** **LINAPITISHA** Mkakati wa CESA 2026-2034, CTVET 2025-2034, na STISA 2034 kama mwelekeo wa siku zijazo wa bara kuhusu elimu, ukuzaji ujuzi, na sayansi, teknolojia na uvumbuzi;

**30.** **LINATOA WITO WA** kuandaa Mpango madhubuti wa Utekelezaji unaojumuisha Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza kwa STISA 2034;

**31.** **LINAIOMBA** Kamisheni, vyombo husika vya Umoja wa Afrika, Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, na washirika kuchukua hatua zote zinazohitajika ili kutoa elimu na kutekeleza Mikakati mipya;

**32.** **LINAIDHINISHA** uamuzi wa Mawaziri la kutangaza kipindi cha 2025-2034 kama "Muongo wa Hatua ya Mageuzi ya Haraka ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi Barani Afrika";

**33.** **LINAISIHI** Kamisheni, Nchi Wanachama, Taasisi za Kikanda, na Wadau wa Maendeleo kwa pamoja kuendelea kudumisha kasi kubwa iliyofikiwa na utekelezaji wa Mwaka wa Elimu wa Afrika wa 2024 katika muongo ujao;

**34.** **LINAIOMBA** Kamisheni, kwa kushirikiana na vyombo husika vya AU, washirika, na nchi wanachama, kuandaa mkakati wa Afrika kwa ajili ya kuendeleza biashara changa;

**35.** **LINAIOMBA** Kamisheni kuwasilisha "Mkataba wa Afrika wa kubadilisha Uhamaji wa wataalam barani Afrika" kwa ajili ya kuboreshwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa

Afrika kwa kufanya uratibu na Kamisheni ili kuwasilishwa kwenye vyombo husika vya sera ili kujadiliwa na kupitishwa;

**36.** **LINAZIOMBA ZAIDI** Kamati Ndogo zinazohusika, kwa kufanya uratibu na AUDA-NEPAD, kufanyia kazi uwezekano wa biashara changa Afrika kupata fedha zilizopo za Umoja wa Afrika ili kufadhili miradi ya kiuvumbuzi katika bara.

## IV. MKUTANO WA 7 WA KAWAIDA WA STC KUHUSU FEDHA, MASUALA YA FEDHA, MIPANGO YA KIUCHUMI NA UTANGAMANO - Doc. EX.CL/1561(XLVI)

**37.** **LINAPOKEA NA KUPITISHA** Ripoti na Azimio la Mkutano wa 7 wa Kawaida wa STC ya Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Uchumi na Utangamano, na mapendekezo yaliyomo;

**38.** **LINAZINGATIA ZAIDI na KUPITISHA** Ripoti na Azimio la Mkutano Maalumu wa 5 wa STC kuhusu Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Uchumi na Utangamano, na mapendekezo yaliyomo;

**39.** **LINAPONGEZA** maendeleo ya uanzishwaji wa Taasisi ya Fedha ya Afrika (AMI) na Mpango wa Uimara wa Kifedha wa Afrika (AFSM);

**40.** **LINATHIBITISHA** kwamba kufikia ukuaji shirikishi, maendeleo endelevu na malengo ya jumla na Matarajio ya Ajenda 2063 itahitaji taasisi za fedha za Kiafrika zenye nguvu na uthabiti ili kusaidia utafutaji wa rasilimali za ndani;

**41.** **LINATHIBITISHA ZAIDI** kwamba kuimarisha uratibu wa sera za uchumi mkuu na kisekta Afrika kutahitaji uratibu thabiti ili kukuza ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu;

**42.** **LINAAMUA**:

**Kuhusu Kuimarisha Uratibu wa Sera za Uchumi Mkuu na kisekta barani Afrika: changamoto, fursa na vipaumbele vya sera kwa ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu**

(i) **Kuzihimiza** Nchi Wanachama kuimarisha uratibu wa sera zao za uchumi mkuu na kisekta ili kufikia mageuzi yenye tija na kuunda nafasi kubwa za kazi zenye staha kwa nia ya kufikia ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu;

(ii) **Kuzihimiza zaidi** Nchi Wanachama kuwekeza katika kukuza ujuzi na miundombinu yenye tija ili kuwezesha ushirikiano wa kikanda;

(iii) **Kuiomba** Kamisheni kuunga mkono Nchi Wanachama kuimarisha uratibu wa sera zao za uchumi mkuu na fedha kwa nia ya kuunda nafasi ya kisera inayohitajika kuwekeza katika sekta za kimkakati, zikiwemo kilimo, viwanda na huduma;

(iv) **Kuisihi** Kamisheni kuunga mkono zaidi Nchi Wanachama katika kuhakikisha kwamba sera za fedha na fedha zinalenga kufikia ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu ya kiuchumi huku zikidumisha uthabiti wa bei na kuendeleza uhimilivu wa deni;

(v) **Kuisihi zaidi** Kamisheni na Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) kuendelea kutoa msaada wa kitaalamu kwa Nchi Wanachama ili kuanzisha na kutekeleza mifumo ya sera ya uchumi mpana inayounga mkono ajira, kuandaa miongozo madhubuti ya sera na kuripoti kwa STC ya 8 mwaka 2025;

(vi) **Kuiomba** Kamisheni kusaidia Nchi Wanachama katika kufanya mageuzi yanayofaa ya kimuundo yanayolenga kusaidia mazingira ya sera ya fedha ambayo yanaimarisha uthabiti wa uchumi mkuu, nidhamu ya fedha na mapambano madhubuti dhidi ya mtiririko haramu wa fedha (IFFs);

(vii) **Kuzihimiza** Nchi Wanachama kuimarisha ushirikiano na uratibu kati ya watunga sera za fedha na fedha na wizara za kisekta, ikiwa ni pamoja na kazi na ajira ili kuimarisha uwiano wa kisera na kuweka uwiano sahihi na nafasi ya kisera kwa ajili ya utekelezaji wa mafanikio wa mipango ya maendeleo yenye utajiri wa ajira;

(viii) **Kutoa wito** kwa Kamisheni, AfricaNenda na Taasisi nyinginezo za Afrika kuunga mkono juhudi za Nchi Wanachama za kuoanisha sera zao za ujumuishaji wa kifedha wa kidijitali kama njia ya kuhimiza mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

**Utekelezaji wa Hatua Muhimu za Ufungaji ili kuharakisha mageuzi ya Afrika kuelekea Uanzishwaji wa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika**

**A. Kuhusu Rasimu Iliyorekebishwa ya Mkataba wa Taasisi ya Fedha ya Afrika (AMI)**

(i) **Kuomba** hati ya mwisho ya Mkataba wa AMI kuwasilishwa kwenye mkutano ujao wa Baraza Kuu wa Februari 2026 baada ya uhakiki wa kisheria wa STC ya Haki na Masuala ya Kisheria;

(ii) **Kuiomba pia** Kamisheni kuunda timu ya wataalamu kutoka Ofisi ya AACB na wataalam kutoka Kamisheni ili kubaini athari za kifedha za AMI;

(iii) **Kutoa wito** kwa Kamisheni kutengeneza miongozo ya kuanzisha miundo ya utawala ya AU.

**B. Kuhusu Mpango wa Uthabiti wa Kifedha Afrika (AFSM)**

(i) **Kuidhinisha** ripoti ya kitaalamu na kiutendaji ya AFSM na kupendekeza kupitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wakati wa Mkutano wao wa Kawaida wa Thelathini na Nane (38);

(ii) **Kupendekeza** kwamba katika uwekaji mtaji, AFSM inapaswa kupitisha muundo wa mtaji wa ufadhili wa soko na michango ya wanachama pekee;

(iii) **Kupendekeza zaidi** kwamba kuhusu uanachama, AFSM inapaswa kukubali angalau asilimia 20 ya wanachama wasio Waafrika ili kufikia kiwango kinacholengwa cha mkopo cha Aa/AA mradi tu Nchi Wanachama za Afrika ziwe na hisa nyingi. Uanachama wa AFSM utakuwa wa hiari na kuwa wazi kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika;

(iv) **Pia kupendekeza** kwamba kwa muundo wa kisheria, AFSM ianzishwe kama shirika lenye msingi wa Mkataba lenye miundo huru ya kisheria, kifedha na utawala;

(v) **Hatimaye kupendekeza** kwamba Kamisheni na AfDB zianzishe timu ya kitaalamu kutoka kwa wataalam wa Nchi Wanachama ili kuandaa mwongozo na mfumo unaoonyesha athari za kisheria, kimuundo na kifedha za AFSM ili kuharakisha uanzishwaji wake.

**Hali ya utekelezaji wa Ufadhili Endelevu wa Umoja wa Afrika**

(i) **Kuiagiza** STC ya Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano kuwa na kipengele cha pekee katika kila kikao kuhusu Hali ya Ufadhili Endelevu wa AU na ukusanyaji wa rasilimali kuelekea utekelezaji wa haraka wa Ajenda 2063;

**Mpango Mkakati wa Hatua Muhimu za Kufikia Ukuaji Shirikishi na Maendeleo Endelevu Barani Afrika**

(i) **Linaidhinisha** Mpango Mkakati wa Hatua Muhimu za Kufikia Ukuaji Shirikishi na Maendeleo Endelevu Barani Afrika na kupendekeza kupitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wakati wa Mkutano wao wa Kawaida wa Thelathini na Nane (38);

**Ushiriki wa AU katika G20 na taarifa ya Kikosi Kazi cha Ngazi ya Juu kuhusu Marekebisho ya Muundo wa Kifedha Duniani**

**A. Kuhusu mageuzi ya muundo wa kifedha duniani:**

(i) **kuihimiza** Kamisheni kuwasilisha taarifa fupi za mara kwa mara kuhusu ushiriki wa AU katika G20 na shughuli;

(ii) **Kuihimiza zaidi** Kamisheni kuendelea kutoa uongozi katika kuendeleza misimamo ya Afrika katika G20 na Marekebisho ya Muundo wa Kifedha Duniani;

(iii) **Kutoa wito** kwa Kamisheni kuratibu kazi ya washirika wa maarifa ili kuhakikisha maandalizi ya misimamo ya Afrika inayotokana na ushahidi inayolenga kulinda maslahi ya bara katika mazungumzo ya kimataifa;

(iv) **Kuihimiza** Kamisheni, na washirika wote wa maarifa wa AU G20 kuhamaisha uwekaji wa Akiba ya Kimataifa ya Rasilimali (SDRs) kupitia Benki za Maendeleo ya Kimataifa (MDBs) kama chombo mseto cha mtaji;

(v) **Kuihimiza zaidi** Kamisheni, UNECA na washirika wengine wa maarifa kufanya utetezi kuhusu uongezaji wa deni kwa mabadiliko ya asili/tabia nchi kwa ajili ya msamaha wa madeni, hatua za tabia nchi na uhifadhi wa asili.

**Kuhusu ushirikiano wa kimataifa wa kodi**

(i) **kuzihimiza** Nchi Wanachama kuunga mkono ipasavyo michakato ya kuelekea Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa (UN) wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Ushuru unaoshughulikia masuala ya IFF, ushuru wa uchumi wa kidijitali na huduma za mipakani ili kuhakikisha mapato ya haraka kwa nchi za Afrika;

(ii) **Kutoa wito** kwa Kamisheni, Jukwaa la Usimamizi wa Ushuru wa Afrika (ATAF), Mtandao wa Haki ya Ushuru Afrika (TJNA) na UNECA kuboresha msaada wao kwa Nchi Wanachama kupitia kujenga uwezo, vikao vya majumuisho na mashauriano ya kikanda ili kuboresha uwezo wao wa kitaalamu kwa nia ya kuhakikisha ushiriki wao kamili katika mazungumzo na mijadala iliyoratibiwa;

(iii) **Kupendekeza** kwamba kwa kadiri inavyowezekana, Nchi Wanachama zifikirie kuwatuma Wataalamu wa Masuala ya Ushuru kwenye Balozi zao za Umoja wa Mataifa huko New York ili kuongeza uwezo wa kitaalamu katika mazungumzo ya Ushirikiano wa Kimataifa wa Ushuru.

**Ushughulikiaji wa Taasisi za Kifedha za Kimataifa za Afrika (AMFIs) katika Utatuzi Huru wa Madeni Afrika**

(i) **Kuthibitisha tena** jukumu kuu la Mashirika ya Kimataifa ya Kifedha ya Afrika (AMFI) na AfDB kama taasisi za kimataifa zinazomilikiwa na Afrika ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya bara;

(ii) **Kudhamiria** kuimarisha mtaji na viwango vya mikopo vya AMFI kwa nia ya kuhamasisha ufadhili wenye masharti nafuu ili kuendesha mabadiliko na ukuaji wa Afrika;

(iii) **Kuzingatia kwa wasiwasi** ripoti za hivi karibuni zinazoleta mashaka juu ya Hali Wakopeshaji wanaopendelewa wa Taasisi za Fedha za Kimataifa za Afrika;

(iv) **Kusisitiza** jukumu muhimu la taasisi za fedha za kimataifa za Afrika kama nguzo za usanifu wa kifedha wa bara, kuchochea utekelezaji wa Ajenda 2063 na kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs);

(v) **Kuthibitisha** kwamba haki zinazotolewa kwa Taasisi za Fedha za Kimataifa za Afrika na Serikali za Afrika chini ya mikataba iliyozianzisha, ikijumuisha hadhi inayopendekezwa ya wakopeshaji, ni muhimu katika mashirikiano na Mashirika ya Ukadiriaji wa Mikopo na katika kuhakikisha upatikanaji wa ufadhili wa maendeleo, kupunguza gharama za kukopa, na kukuza soko letu la mitaji la ndani na bara;

(vi) **Kudhamiria** kuimarisha Taasisi za Fedha za Kimataifa za Afrika na kuendelea kuheshimu wajibu wao kwa taasisi hizi, ikiwa ni pamoja na hali zao za mikopo wanazopendelea, kulingana na mikataba yao;

(vii) **Kupendekeza** kwamba Mkutano Mkuu uipe mamlaka Kamisheni kufanya kazi na AAMFI ili kushirikiana na wadau wakuu kuhusu suala hili, ikiwa ni pamoja na katika majadiliano ya G20.

**Taarifa kuhusu Kuanzishwa kwa Shirika la Ukadiriaji wa Mikopo wa Afrika**

(i) **Kutoa wito** kwa Kamisheni, APRM na AfDB kuharakisha utendaji kazi wa Shirika la Ukadiriaji wa Mikopo wa Afrika (ACRA) unaoendeshwa na sekta binafsi;

(ii) **Kuzihimiza** AfDB na Afreximbank kupata msaada wa kifedha na kitaalamu kwa ajili ya uendeshaji wa ACRA.

**Hali ya Utangamano wa Kikanda katika Afrika**

(i) **Kutoa wito** kwa Kamisheni kuhakikisha uwiano wa Fahirisi na viashirio vya RECs kuwa na seti moja ya data iliyounganishwa kwa ajili ya tathmini ya ujumuishaji wa kikanda;

(ii) **Kuihimiza** Kamisheni kuunda mfumo maalum wa kidijitali unaolenga kukusanya data kuhusu ujumuishaji wa kikanda na RECs ili kuwezesha utayarishaji wa ripoti jumuishi ya ujumuishaji wa kikanda;

(iii) **Kutoa wito zaidi** kwa Kamisheni, UNECA na RECs kutoa Fahirisi mara mbili kwa mwaka ili kuhakikisha utiifu na kuhakikisha Nchi Wanachama zinabaki kwenye mstari ili kufanikisha utangamano wa kikanda wa Afrika;

(iv) **Kuisihi** Kamisheni, UNECA na AfDB kuandaa warsha ya uthibitishaji kwa nia ya kujenga uwezo wa RECs na kuanza mchakato wa kusambaza Fahirisi na kuchapisha ripoti ya kwanza kwa kuzingatia Kielezo cha Ushirikiano wa Kikanda cha Afrika (ASRII) na kuripoti kwa Mashirika ya Sera ya AU.

**Maelekezo ya Huduma za Malipo kwa Afrika (PSDA)**

(i) **Kuiomba** Kamisheni na AfricaNenda kujenga utaratibu wa uratibu baina ya taasisi ili kufanya kazi kwa karibu na taasisi zote zinazohusika kama vile

Muungano wa Benki Kuu za Afrika (AACB), Afreximbank, RECs, na wadau binafsi, ili kuepusha kuingiliana na kurudiwa katika maendeleo ya PSDA;

(ii) **Kuihimiza** Kamisheni na AfricaNenda kufanya mashauriano ya kina ya wadau kuhusu maendeleo ya PSDA;

(iii) **Kuihimiza zaidi** Kamisheni na AfricaNenda kuwasilisha ripoti ya maendeleo wakati wa Mkutano wa 8 wa Kawaida wa STC.

## V. MKUTANO WA KAWAIDA WA 7 WA KAMATI MAALUM YA KITAALAM (STC) KUHUSU FEDHA, MASUALA YA FEDHA, MIPANGO YA KIUCHUMI NA UTANGAMANO, 03-07 JULAI 2024, TUNIS, TUNISIA NA STC MAALUM YA 5, TAREHE 28 HADI 30 NOVEMBA 2024, ABUJA, NIGERIA

**43.** **LINAZINGATIA KWA KURIDHISHWA** maendeleo kuelekea uanzishwaji wa Taasisi ya Fedha ya Afrika (AMI) na Mpango wa Uthabiti wa Kifedha wa Afrika (AFSM) na **LINAELEZA** msaada katika uendeshaji wa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika (AUFIs);

**44.** **LINAAMUA**:

### A. Kuhusu Mpango wa Uthabiti wa Kifedha wa Afrika (AFSM)

(i) **KUPITISHA** ripoti ya kiufundi na kiuendeshaji ya AFSM; na

(ii) **KUIPONGEZA** Kamisheni, AfDB kwa juhudi zao za bila kuchoka katika kukamilisha ripoti ya utafiti ya kiufundi na kiuendeshaji kuhusu AFSM;

(iii) **KUAGIZA** kwamba Kamisheni na AfDB zianzishe timu ya kiufundi ya wataalam kutoka Nchi Wanachama ili kuandaa mwongozo na kuunda mfumo unaoeleza athari za kisheria, kimuundo na kifedha za AFSM ili kuharakisha uanzishwaji wake.

### Mfumo wa Kimkakati wa Hatua Muhimu za Kufikia Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu Barani Afrika

(i) **KUPITISHA** Mfumo wa Kimkakati wa Hatua Muhimu za Kufikia Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu Barani Afrika;

(ii) **KUZISIHI** Kamisheni na AfDB kusaidia Nchi Wanachama, jumuiya za kiuchumi za kikanda kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo ndanin ya Mfumo huo.

### Ushiriki wa AU katika G20

**B. Kuhusu mageuzi ya muundo wa fedha wa kimataifa:**

(i) **Kuisihi** Kamisheni kuendelea kutoa uongozi katika kuendeleza Misimamo ya Afrika katika G20 na Mageuzi ya Muundo wa Fedha Duniani;

(ii) **Kutoa wito kwa** Kamisheni kuratibu kazi ya wabia wa maarifa ili kuhakikisha maandalizi ya Misimamo ya Afrika inayotokana na ushahidi inayolenga kulinda maslahi ya bara katika majadiliano ya kimataifa;

(iii) **Kuhimiza** Kamisheni, na wabia wote wa maarifa wa G20 wa AU kutetea uendeshaji wa uelekezaji wa Mali ya Akiba ya Kimataifa (SDRs) kupitia Benki za Maendeleo za Kimataifa (MDBs) kama chombo cha mseto cha mtaji.

**C. Kuhusu ushirikiano wa Kimataifa wa ushuru:**

(i) **Kuzihimiza** Nchi Wanachama kuunga mkono ipasavyo michakato ya kuelekea Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa (UN) wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Ushuru unaoshughulikia masuala ya IFF, ushuru wa uchumi wa kidijitali na huduma za kuvuka mipaka ili kuhakikisha mapato ya haraka kwa nchi za Afrika;

(ii) **Kutoa wito** kwa Kamisheni, Jukwaa la Usimamizi wa Ushuru la Afrika (ATAF), Mtandao wa Haki ya Ushuru Afrika (TJNA) na UNECA kuboresha msaada wao kwa Nchi Wanachama kupitia kujenga uwezo, vikao vya majumuisho na mashauriano ya kikanda ili kuboresha uwezo wao wa kitaalamu kwa nia ya kuhakikisha ushiriki wao kamili katika mazungumzo kwa michango iliyoratibiwa;

(iii) **Kupendekeza** kwamba kwa kadiri inavyowezekana, Nchi Wanachama zifikirie kuwatuma Wataalamu wa Masuala ya Ushuru kwenye Jumbe zao husika za Umoja wa Mataifa huko New York ili kuongeza uwezo wa kitaalamu katika mazungumzo ya kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa wa Ushuru.

**Taarifa kuhusu Uanzishwaji wa Wakala wa Ukadiriaji wa Mikopo wa Afrika**

(i) **Kuisihi** Kamisheni, APRM na AfDB kuharakisha uendeshaji wa Wakala wa Ukadiriaji wa Mikopo wa Afrika (ACRA) unaoendeshwa na sekta binafsi;

(ii) **Kuhimiza** AfDB na Afreximbank kupata msaada wa kifedha na kiufundi kwa ajili ya uendeshaji wa ACRA.

**Hali ya Utangamano wa Kikanda barani Afrika**

(i) **Kuzisihi** Kamisheni, UNECA, AfDB na RECs kuchapisha Ripoti ya kwanza ya Utangamano wa Afrika kulingana na Faharasa ya Utangamano wa Kikanda ya Afrika (ASRII) na kuripoti kwa Vyombo vya Sera vya AU.

## VI. MKUTANO WA KWANZA (1) MAALUMU WA STC KUHUSU BIASHARA, UTALII, VIWANDA NA MADINI - Doc. EX.CL/1563(XLVI)

**45.** **Kukaribisha** kuitishwa kwa Mkutano wa Kwanza Maalumu wa STC ya Biashara, Utalii, Viwanda na Madini ambao ulifanyika Makao Makuu ya Kamisheni mjini Addis Ababa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, tarehe 11-13 Desemba 2024.

**46.** **Kuzingatia** Ripoti ya Mkutano wa 1 Maalumu wa STC ya Biashara, Utalii, Viwanda na Madini na matokeo yaliyomo, kama ilivyoambatanishwa.

**47.** **LINAAMUA**: -

**A. Kuhusu Rasimu ya Utafiti wa Tathmini ya Utayari kuelekea Umoja wa Forodha wa Afrika/Soko la Pamoja**

(i) **Kuzingatia** kuwa AfCFTA bado iko katika hatua zake za awali za utekelezaji na kwamba baadhi ya vipengele vya Mkataba bado vinajadiliwa, hivyo ni mapema kujadili uanzishwaji wa Umoja wa Forodha/Soko la Pamoja.

(ii) **Kuiomba** Kamisheni, Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, RECs, AUDA-NEPAD, UNECA, Nchi Wanachama wa AU na Washirika kushirikiana katika kukamilisha Utafiti wa Tathmini ya Utayari kuelekea Umoja wa Forodha wa Afrika/Soko la Pamoja.

(iii) **Kuiagiza** Kamisheni kuandaa Kongamano maalum kuhusu tathmini ya utayari wa Umoja wa Forodha/Soko la Pamoja kwa ushirikiano na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, AUDA-NEPAD na Sekretarieti ya AfCFTA.

(iv) **Kuzihimiza** Nchi Wanachama kuharakisha utekelezaji wa AfCFTA na Protokali zake zote kabla ya kuhamia kwenye Umoja wa Forodha/Soko la Pamoja.

**B. Kuhusu Rasimu ya Mkakati wa Kubadilisha na Kuongeza Mauzo ya Nje ya Afrika**

(i) **Kuzingatia** maendeleo ya Mkakati wa Umoja wa Afrika wa Kubadilisha na Kuongeza Mauzo ya Nje ya Afrika na Kamisheni ya Umoja wa Afrika kama kazi inayoendelea.

(ii) **Kuiomba** Kamisheni na washirika wake kama vile UNECA, ITC, UNCTAD, UNIDO, Afreximbank miongoni mwa nyingine, kufanya kazi pamoja na kufanya mashauriano zaidi na Nchi Wanachama na wadau wengine ili kukamilisha mkakati huo.

(iii) **Kuagiza** kuwa Mkakati wa mwisho uwasilishwe kwenye Mkutano wa 5 wa Kamati Maalumu ya Kitaalam ya Sekta ya Utalii wa Biashara na Madini ili kujadiliwa baada ya mashauriano ya ngazi ya kitaifa.

**C. Kuhusu Rasimu ya Mkakati wa Umoja wa Afrika wa Madini yasiyoathiri mazingira**

(i) **Kupitisha** Rasimu ya Mkakati wa Afrika wa Madini yasiyoathiri mazingira: Mkakati wa Rasilimali za Madini wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya Kipindi cha Mpito cha Haki na Mustakabali wa Utoaji kaboni, pamoja na michango iliyotolewa na Nchi Wanachama kulingana na mpango wa pili wa utekelezaji wa miaka 10 wa Ajenda 2063;

(ii) **Kuipa mamlaka** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuandaa Mipango ya Utekelezaji wa nguzo mbalimbali na zigharamiwe pindi Mkakati wa Afrika wa Madini yasiyoathiri mazingira utakapopitishwa.

(iii) **Kuiagiza** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kutekeleza shughuli za uhamasishaji na uhamasishaji wa kina kuhusu Mkakati wa Madini yasiyoathiri mazingira Afrika kwa wadau wote wanaoweka mkazo katika uendelevu wa mazingira na usawa wa kijamii.

(iv) **Kutoa** shukrani kwa Washirika wote wanaohusika katika utayarishaji wa Mkakati huu na linatoa wito kwao kuunga mkono utekelezaji wa Mkakati wa Umoja wa Afrika wa Madini ya Kijani mara tu Mkakati huo utakapopitishwa na Vyombo vya Sera vya Umoja wa Afrika, ukiungwa mkono na kuendelea kwa ushirikiano wa kikanda na juhudi za utangamano, kufanya kazi kupitia RECs kwa ajili ya matokeo makubwa zaidi.

**D. Kuhusu Muongo wa Tatu wa Maendeleo ya Viwanda kwa Afrika (IDDA III) na Muongo wa Nne wa Maendeleo ya Afrika (IDDA IV)**

i. **Kuliomba** Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) litangaze muongo ujao wa ukuaji wa viwanda barani Afrika, kwa kuzingatia uzoefu wa miongo iliyopita na IDDA III inayoendelea na kutumia mazingira mazuri ya kimataifa na kikanda.

ii. **Kuiagiza** Kamisheni kushirikiana kwa karibu na UNIDO na wadau wengine husika ili kukusanya rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kukuza, kuendeleza na kutekeleza IDDA IV kwa ufanisi.

**iii.** **Kuiagiza zaidi** Kamisheni kufanya kazi kwa karibu na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), UNIDO na wadau wengine ili kuimarisha ujuzi wa kiufundi na utaalamu wa kisera katika ngazi za kikanda na kitaifa kuhusu masuala ya Uanzishaji wa Viwanda.

**VII. STC YA 9 KUHUSU USAWA WA KIJINSIA NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE - Doc. EX.CL/1564(XLVI)**

48. **LINAZINGATIA** hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Azimio Madhubuti la Usawa wa Jinsia Barani Afrika (SDGEA).

49. **LINAPITISHA** Ripoti ya Utekelezaji wa Azimio Maalumu la Usawa wa Jinsia Barani Afrika (SDGEA)

50. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ambazo bado hazijawasilisha SDGEA yao ya awali kufanya hivyo kwa Kamisheni - Kurugenzi ya Wanawake, Jinsia na Vijana.

51. **LINATAMBUA** Nchi Wanachama 45 ambazo zimeridhia Itifaki ya Maputo

52. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama 10 ambazo bado hazijaridhia kuchukua hatua zinazofaa katika ngazi ya kitaifa na kuwasilisha hati zao za kuridhia kwa Kamisheni.

**VIII. MKUTANO MAALUMU WA 3 WA STC YA USAFIRISHAJI NA NISHATI (STC-T&E) – Doc. EX.CL/1565(XLVI)**

53. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano Maalumu wa 3 wa Kamati ya Kitaalamu ya Usafirishaji na Nishati (STC-T&E) uliofanyika tarehe 3 hadi 5 Desemba 2024 na Azimio linalohusiana nalo.

54. **LINAWAPONGEZA** Mawaziri wenye dhamana ya Usafirishaji na Nishati kwa kufanikisha Mkutano Maalumu wa 3 wa Kamati ya Kitaalamu ya Usafirishaji na Nishati (STC-T&E) na kupata matokeo muhimu ya maendeleo ya usafirishaji, miundombinu ya kikanda na nishati barani Afrika. .

**(1) Kuhusiana na Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu Barani Afrika (PIDA):**

55. **LINAPITISHA** Sera ya Bara kuhusu Miundombinu Inayohimili Tabianchi na Miundombinu Bora barani Afrika.

56. **LINAIOMBA:**
   a. Kamisheni, Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kusambaza, kumiliki, na kutekeleza Sera ya Bara la Afrika kuhusu Miundombinu Inayohimili Tabianchi na Miundombinu Bora barani Afrika.
   b. Kamisheni, ECA, Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kwa ushirikiano na taasisi za Afrika nzima kwa msaada wa wabia wa maendeleo kukusanya rasilimali za kitaalamu na kifedha ili kutekeleza Sera ya Bara la Afrika kuhusu Miundombinu inayohimili Tabianchi na Miundombinu bora barani Afrika.

**(2) Kuhusiana na Sekta ya Usafirishaji:**

**57. LINAPITISHA:**

a. Mkakati wa Bara wa kusaidia maendeleo na matumizi ya Nishati Endelevu ya Usafirishaji wa Anga (SAF) na Nishati zingine za Usafiri wa Anga zenye kiwango cha Chini cha Kaboni (LCAF) barani Afrika.
b. Malengo ya Abuja yaliyoboreshwa kuhusu Usalama wa Anga.

**58. LINAIOMBA:**

a. Kamisheni na AFCAC kwa msaada wa wabia wa maendeleo kukusanya rasilimali za kitaalamu na kifedha kusaidia utekelezaji kwa wakati wa Mkakati wa kuongeza kasi ya uzalishaji, maendeleo na matumizi ya SAF na LCAF barani Afrika.
b. AFCAC kuzisaidia Nchi Wanachama kuboresha utekelezaji wao bora kama ilivyorekebishwa katika Malengo ya Abuja kuhusu Usalama wa Anga, 75% ifikapo 2024, 85% ifikapo 2026 na 95% ifikapo 2030;
c. AFCAC kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu hali ya utekelezaji wa Malengo ya Abuja kuhusu Usalama katika kila Nchi Mwanachama kwa Mawaziri wa Usafirishaji katika Mikutano ya Kawaida ya STC-T&E na majukwaa mengine ya bara yanayoshughulikia changamoto zinazokabili Nchi Wanachama katika kuhakikisha uzingatiaji wa malengo na kuonyesha mikakati iliyochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo.

**59. LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kujitolea kikamilifu katika utekelezaji mzuri wa Malengo ya Abuja yaliyoboreshwa kuhusu Usalama wa Anga.

**(3) Kuhusiana na Sekta ya Nishati**

**60. LINAPITISHA:**

a. Mkakati, Mwongozo na Mpangokazi kuhusu Ufanisi wa Nishati barani Afrika, (AfEES)
b. Mkakati na Mpangokazi wa Haidrojeni inayozingatia mazingira barani Afrika.

**61. LINAIOMBA:**

a. AFREC kwa kushirikiana na washirika wa bara na kikanda ili kukusanya rasilimali muhimu za kitaalamu na kifedha ili kutekeleza mwongozo na mpango wa utekelezaji wa AfEES huku ikitoa msaada unaohitajika kwa Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda.
b. AFREC kuchunguza matumizi ya teknolojia zinazoibuka kama vile akili mnemba na ubunifu katika sekta za nishati, usafirishaji, viwanda, kilimo, ujenzi na upishi unaotumia nishati safi ili kuongeza ufanisi wa nishati barani Afrika;
c. AFREC kuratibu utendaji kazi wa Muungano wa Ufanisi wa Nishati barani Afrika (AEEA) kama jukwaa shirikishi la kutetea maarifa ya ufanisi wa nishati na kubadilishana uzoefu, uhamishaji wa teknolojia na uwekezaji.

d. Kamisheni kwa kushirikiana na washirika wa bara na kikanda kutekeleza Mkakati na Mpangokazi wa Haidrojeni inayozingatia mazingira barani Afrika.
e. Kamisheni ikusanye rasilimali za kitaalamu na kifedha ili kusaidia Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda ili kuunda sera na mifumo ya udhibiti wa haidrojeni inayozingatia mazingira inayohusiana na mahitaji na mazingira yao mahususi.

**62. LINAZIHIMIZA:**

a. Nchi Wanachama kuitangaza Afrika kama muuzaji mkuu na mtengenezaji wa haidrojeni inayozingatia mazingira kwa ajili ya masoko ya ndani na kimataifa;

b. Nchi Wanachama kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ukuzaji wa minyororo ya thamani ya haidrojeni inayozingatia mazingira kwa viwanda na bidhaa zinazozingatia mazingira.

**IX. Mkutano wa Kawaida wa Kumi (10) wa STC ya Haki na Masuala ya Kisheria - EX.CL/1567(XLVI)**

**63. LINAZINGATIA** Ripoti na mapendekezo ya Mkutano wa Kawaida wa Kumi (10) wa STC ya Haki na Masuala ya Kisheria uliofanyika kuanzia tarehe 14 hadi 22 Disemba 2024 katika mfumo mseto: Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa njia ya video.

**64. PIA LINAZINGATIA** Rasimu zifuatazo za Hati za Kisheria:

*i) Rasimu ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana;*

*ii) Rasimu ya Mkataba wa Shirika la Usalama wa Chakula Afrika;*

*iii) Rasimu ya Viambatisho vya Protokali ya Makubaliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika kuhusu Biashara ya Kidigitali:*

*a) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Kanuni za Asili*
*b) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Vitambulisho vya Kidijitali*
*c) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Malipo ya Kidijitali ya Mipakani*
*d) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Uhamishaji Data unaovuka Mipaka*
*e) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Vigezo vya Kuamua Sababu halali na za Kisheria za Maslahi ya Umma za Ufichuaji wa Kanuni Chanzo.*
*f) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Usalama na Usalama Mtandaoni*
*g) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Teknolojia zinazoibukia na za Juu*
*h) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Teknolojia ya Fedha; na*

*iv) Rasimu ya Mkataba wa Mfumo wa Uwezo wa Raia wa Bara la Afrika kwa ajili ya Majanga, Utayari (kuthibitishwa na Baraza Kuu)*

65. **LINAAMUA** kupendekeza Rasimu ya Hati za Kisheria zilizotajwa hapo juu kwa Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa;

66. **LINAOMBA** kila Mjumbe wa Uongozi wa STC-JLA kuteua mtaalamu mmoja (1) wa kisheria kuunda Kamati ya kuandaa upya Rasimu ya Mkataba Uliorekebishwa wa Mahakama ya Utawala ya AU, kwa kushauriana na wadau husika. Hizi ni pamoja na Kamisheni, Mahakama ya Utawala ya AU, na wawakilishi wa wafanyakazi wa AU na kuripoti kwa STC kuhusu Haki na Masuala ya Kisheria kufikia Desemba 2025.

## X. MKUTANO WA 10 WA KAWAIDA WA STC KUHUSU UTUMISHI WA UMMA, SERIKALI ZA MITAA, MAENDELEO YA MIJI NA UGATUAJI (AU-STC-8) – Doc. EX.CL/1566(XLVI)

67. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano wa 5 wa Kawaida wa AU-STC8.

68. **LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Tunisia kwa kuandaa Mkutano wa Tano wa Kawaida wa Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Umoja wa Afrika kuhusu Utumishi wa Umma, Serikali za Mitaa, Maendeleo ya Miji na Ugatuaji.

69. **LINAZINGATIA** pendekezo la uhamisho wa Makazi ya Watu na Maendeleo ya Miji kutoka Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama kwenda Idara ya Miundombinu na Nishati na kuiomba Kamisheni kuheshimu kikamilifu utaratibu unaostahili katika suala hili.

70. **LINATHIBITISHA** Uchaguzi wa wajumbe wapya wa Uongozi wa AU-STC8

71. **LINAIOMBA** AUC kuharakisha utendaji kazi wa Baraza Kuu la Mamlaka za Serikali za Mitaa (HCLA) kupitia utekelezaji wa uamuzi wa Baraza Kuu 993 wa Januari 2018 na kuripoti kwenye Mkutano wa Baraza Kuu mnamo Juni 2023. **LINAIKABIDHI** AUC jukumu la kuanzisha mchakato wa kutia saini makubaliano ya nchi mwenyeji (Senegal).

72. **LINAIOMBA ZAIDI** Kamisheni kufanya uzinduzi wa maadhimisho ya Siku ya Bara la Afrika ya Ugatuaji wa Madaraka kuanzia 2026 na Mpango wa Tuzo za Ugatuaji wa Ugatuzi, Serikali za Mitaa na Maendeleo ya Afrika utakaoanza kutumika tarehe 10 Agosti 2026 na kutoa wito kwa Nchi Wanachama kushiriki kikamilifu katika mpango wa uzinduzi wa tuzo.

**UAMUZI**
**KUHUSU UTEKELEZAJI WA KAULIMBIU YA AU YA MWAKA 2024 KUHUSU ELIMU– Doc. EX.CL/1568(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2024;

2. **LINASISITIZA** umuhimu wa kufanya mageuzi ya elimu barani Afrika na haja ya kudumisha kasi hii ambayo inaweka uangalizi wa bara katika kujenga mifumo thabiti zaidi ili kuongeza upatikanaji wa Elimu jumuishi, bora na yenye tija kwa Afrika;

3. **LINATANGAZA** kipindi cha 2025-2034 kama ***“Muongo wa Hatua ya Haraka kwa ajili ya Mabadiliko ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi Barani Afrika”***

4. **LINATOA WITO KWA** Nchi zote Wanachama, Wabia wa Maendeleo, Kamisheni na wadau wote kutoacha juhudi zozote za kufufua elimu na maendeleo ya ujuzi kama kipaumbele cha bara kwa muongo ujao.

5. **LINAPITISHA** Maazimio yote ya mwisho ya shughuli na majukwaa yaliyoandaliwa na Kamisheni na Nchi Wanachama chini ya Kaulimbiu ya mwaka 2024 kuhusu Elimu, ikiwa ni Pamoja na Azimio la Mkutano wa Nouakchott kuhusu Elimu.

# UAMUZI
# KUHUSU RIPOTI YA KAMISHENI KUHUSU MAJANGA YA KIBINADAMU BARANI AFRIKA KWA KIPINDI CHA JANUARI – DESEMBA 2024.
# Doc. EX.CL/1572(XLVI)A

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu majanga ya kibinadamu barani Afrika kuanzia Januari hadi Desemba 2024.

2. **LINAELEZA WASIWASI** kuhusu changamoto za kibinadamu zinazojirudia barani Afrika, zinazosababishwa na migogoro mikali, mashambulizi ya kigaidi, migogoro ya kisiasa na kiuchumi, athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi na majanga, kama vile vimbunga, milipuko ya volkano, ukame, njaa, kufanyika jangwa, maporomoko ya ardhi, mafuriko, magonjwa ya wanyama, uvamizi wa wadudu waharibifu, magonjwa ya milipuko na magonjwa yanayoenea eneo kubwa hivyo kupelekea uharibifu wa nyumba, huduma za kijamii, shughuli za kujipatia riziki, uhaba wa chakula, na uhamaji wa watu kwa nguvu kutoka kwenye makazi yao. Uhamaji huu umeendelea kuwepo kwa muda mrefu huku kukiwa na athari za kudumu kwa watu walioathiriwa.

3. **LINATAMBUA KWA KUTHAMINI** juhudi za Nchi zote Wanachama zinazowahifadhi wakimbizi, na **LINAZIKUMBUSHA** nchi zote zilizoridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa 1951 kuhusu wakimbizi, na Mkataba wa OAU wa 1969 Unaosimamia Masuala Mahususi ya Tatizo la Wakimbizi Barani Afrika, uliopitishwa Wakuu wa Nchi na Serikali tarehe 10 Septemba 1969 mjini Addis Ababa, Ethiopia, na nchi zilizoridhia Mkataba wa 2009 kuhusu Ulinzi na Msaada kwa Watu Waliohama Makazi Nchini mwao kuhusu majukumu yao katika ulinzi wa kimataifa kwa watu wanaohitaji ulinzi huo kama ilivyoainishwa katika mikataba hiyo miwili.

4. **LINAZINGATIA KWA WASIWASI MKUBWA** rasilimali zinazopungua kwa ajili ya kuwa na mwitikio wa haraka na unaofaa kwa majanga ya kibinadamu barani Afrika na **LINAWAOMBA** wadau husika kuongeza juhudi maradufu katika kukusanya rasilimali za fedha kwa ajili ya shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu.

5. **LINATOA WITO kwa** Nchi Wanachama kutumia mbinu za jumla za kushughulikia sababu za msingi za majanga ya kibinadamu, ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika kilimo cha kutumia mashine, kwa nia ya kukuza uwezo wa kujitosheleza kwa chakula katika Bara la Afrika na kupunguza hatari na hali ya kuwa katika hatari inayohusishwa na utegemezi kwenye vyanzo vya nje vya chakula.

6. **LINAWAHIMIZA** wabia wa makundi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, na taasisi zingine za fedha za kikanda, nchi wafadhili zinazotoa msaada wa moja kwa moja kwa nchi nyingine, na sekta binafsi kuchangia katika kupunguza mzigo kwa nchi na jamii zilizoathiriwa na uhamaji katika bara zima. **LINAOMBA** ufadhili zaidi kutolewa kwa nchi zinazokabiliwa na tatizo la watu

kuhama makazi yao kwa lazima kutokana na mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili pamoja na nchi zinazohifadhi idadi kubwa ya wakimbizi barani Afrika.

7. **LINATOA WITO KWA** jumuiya ya kimataifa kutimiza wajibu wake wa kimataifa wa uwajibikaji wa pamoja na kugawana mizigo kwa kusaidia kutoa rasilimali za msaada wa kibinadamu zinazohitajika sana ili kusaidia IDPs, wakimbizi, wakimbizi wanaorejea nyumbani kwao, watafuta hifadhi na watu wasio na utaifa barani Afrika.

8. **LINAIOMBA** Kamisheni kufanya kazi na Nchi Wanachama na wabia kama vile WFP, UNHCR, FAO miongoni mwa wengine ili kuanzisha taratibu za kushughulikia masuala ya usalama wa chakula miongoni mwa watu waliokumbwa na majanga ya kibinadamu. **LINATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi Wanachama na jumuiya pana ya kimataifa kuwa na mwitikio kwa majanga ya dharura ya kibinadamu ambayo hayajawahi kushuhudiwa ambayo kwa sasa bara hili linakabiliwa nayo na kuunga mkono programu za ustahimilivu kwa watu walioathiriwa na majanga makubwa, njaa na majanga mengine.

9. **LINAKARIBISHA** uungwaji mkono unaoendelea na mshikamano unaooneshwa na Nchi Wanachama wa AU katika kushughulikia changamoto za kibinadamu barani Afrika na hususan kwa wakimbizi, watafuta hifadhi, na watu waliokimbia makazi yao, na ndani ya muktadha wa kuongezeka kwa kasi kwa mahitaji ya kibinadamu na kupungua kwa ufadhili wa msaada wa kibinadamu, **LINATOA WITO wa** Ushirikiano wa karibu miongoni mwa watendaji mbalimbali wa msaada wa kibinadamu.

10. **LINAZISIHI** Nchi W22anachama, wabia wa kimataifa wa msaada wa kibinadamu na wadau wengine muhimu, kuunga mkono utekelezaji wa mifumo ya kanuni na sera inayoendelea sana inayotungwa na AU, ili kuimarisha ufikiaji wa msaada wa kibinadamu na kupanua nafasi ya msaada wa kibinadamu.

11. **LINAZIELEKEZA** pande zote zinazohusika katika migogoro kuheshimu sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu, sheria za haki za binadamu na sheria ya wakimbizi, ikiwa ni pamoja na ulinzi wa raia wakati wa mgogoro wa kutumia silaha na uzuiaji wa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ili kuhakikisha kwamba watendaji wa msaada wa kibinadamu wako salama na wanaweza kuwafikia watu walioathiriwa na migogoro na majanga, na **KUHAKIKISHA** udumishaji wa hali ya kiraia na ya kibinadamu ya mazingira ya mkimbizi na IDP.

12. **LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Uganda kwa kupewa haki ya kuwa mwenyeji wa Shirika la Msaada wa Kibinadamu la Afrika na **LINATOA WITO** kwa Kamisheni kuharakisha uendeshaji wa Shirika hilo na **LINATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi zotec Wanachama kuunga mkono mchakato huo.

13. **LINAISIHI** Kamisheni kuendeleza uenezaji wa Azimio la Malabo la Mkutano Maalumu wa 15 wa Masuala ya Kibinadamu wa Umoja wa Afrika na Mkutano wa Ahadi na utekelezaji wa mpango kazi wa miaka 10 wa baada ya Malabo kwa ushirikiano na uratibu wa karibu na Nchi Wanachama na wabia.

14. **LINAZIKUMBUSHA ZAIDI** Nchi Wanachama ambazo hazijatimiza ahadi zao za Malabo kufanya hivyo, kwani itakuwa muhimu kwa uendeshaji wa Shirika la Msaada wa Kibinadamu la Afrika na utekelezaji wa mamlaka yake;

15. **LINAIBUA WASIWASI** kuhusu hali ya kibinadamu nchini Sudan na DRC na **LINAIOMBA** Kamisheni kupeleka Timu ya Tathmini ya Msaada wa Kibinadamu, iliyochangiwa kwa hiari na Nchi Wanachama wa AU ili kutathmini janga la kibinadamu, kuratibu na kuwezesha utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa watu walioathiriwa na migogoro nchini Sudan na DRC.

16. **LINATAMBUA** Nchi Wanachama ambazo zilipitisha sera za mipaka wazi na utangamano wa kitaifa kwa watu wote waliolazimika kuyahama makazi yao, wakiwemo wakimbizi, watafuta hifadhi na watu wasio na utaifa.

17. **LINATHIBITISHA** kwamba kuanza kutumika kwa Mkataba wa AU wa Ulinzi na Msaada wa IDPs mwaka 2012 kulikuwa ni kilele muhimu cha juhudi za Afrika za kushughulikia uhamaji wa ndani kwani uliweka chombo cha kwanza na cha pekee cha kimataifa kinachofunga kisheria kwa ajili ya ulinzi na msaada wa IDPs. Hata hivyo, miaka kumi baada ya kuanza kutumika kwake, utekelezaji wa Mkataba unabakia kuwa wa chini wa kukatisha tamaa. Kwa hiyo, **LINAUAGIZA** Mkutano wa Nchi Zilizoridhia kukutana kila baada ya miaka miwili ili kutumika kama jukwaa la ufuatiliaji wa mkataba huo.

18. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuchukua hatua za kinga na mwitikio ili kuzuia na kupunguza athari za migogoro na mabadiliko ya tabianchi kwa kushughulikia vyanzo vya migogoro na majanga ya asili na, **ZAIDI LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kufuatilia uundwaji wa mbinu jumuishi ya kuimarisha mifumo ya kilimo cha chakula , afya, na mifumo ya ulinzi wa kijamii ili kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa ajili ya jamii, wakimbizi, IDPs na jamii zinazowahifadhi.

19. **LINAPONGEZA** mchango wa Kamati Ndogo ya PRC ya Wakimbizi, Wanaorejea nchini kwao na Watu Waliohama Makazi nchini Mwao katika kuunda ajenda ya msaada wa kibinadamu katika bara na **LINAIOMBA** Kamati Ndogo na Kamisheni kuendelea kufanya kazi za tathmini ya msaada wa kibinadamu kwa mshikamano na nchi zinazohifadhi idadi kubwa ya wakimbizi, pamoja na zile zilizoathiriwa na maafa na majanga ya kibinadamu.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KAMISHENI KUHUSU HALI YA UHURU WA WATU KUSAFIRI BARANI AFRIKA
## Doc.EX.CL/1572(XLVI)D

**Baraza Kuu**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu hali ya Uhuru wa Watu Kusafiri Barani Afrika.

2. **LINATAMBUA** kuongezeka kwa umaarufu na kutambuliwa kwa mradi wa uhuru wa watu kusafiri barani humo, huku likisisitiza haja ya jitihada za uratibu za kukabiliana na pengo lililopo katika uridhiaji wa Protokali na uhamasishaji wa kina unaohakikisha mfumo mzuri kwa ajili ya utekelezaji wa Protokali na itakapoanza kutumika.

3. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama wa AU binafsi na kwa pamoja kutekeleza mkakati wa hatua kwa hatua wa uhuru wa watu kusafiri kwa kuzingatia kanuni ya mabadiliko, na kuchukua hatua zinazofaa ili "kuwezesha" uhuru wa watu kusafiri na kutoa nafasi kwa ushirikiano mpana wa kijamii na kiuchumi katika Afrika;

4. **LINAZIPONGEZA** nchi ambazo zimeridhia Protokali ya AU ya Uhuru wa Watu Kusafiri Barani Afrika, na kuzitaka zile ambazo bado hazijaridhia kufanya hivyo kwa nia ya Umajumui wa Kiafrika ili kuwezesha Protokali hiyo kuanza kutumika;

5. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuimarisha na kuunganisha mifumo ya kitaifa ya usajili wa raia, hasa uadilifu wa vitambulisho na hati za kusafiria; kuimarisha usalama na utoaji wa vitambulisho vya kibayometriki na hati za kusafiria, kama vile pasipoti zinazozingatia viwango vya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO). Kuweka vifaa vya kutosha mipakani na kuimarisha uwezo unaohusiana wa mashirika yote husika kama vile utekelezaji wa sheria, forodha, uhamiaji na mamlaka za afya.

6. **LINAIOMBA** Kamisheni kwa uratibu na Nchi Wanachama kuandaa na kutumia ufuatiliaji wa Bara na kuratibu mfumo wa kutathmini hali ya kutekeleza Protokali kwa mujibu wa Ibara za 27, 28, na 29. **PIA LINAIHIMIZA** Kamisheni kuhakikisha ufadhili endelevu wa wafanyakazi wa Protokali kuhusu Uhuru wa Watu Kusafiri ili kutoa msaada wa kutosha, kuhakikisha ufuatiliaji na ripoti ya maendeleo yaliyopatikana, na kuandaa njia ya kuendelea kwa Protokali hiyo kuanza kutumika na utekelezaji wake.

7. **LINAISIHI** Kamisheni na RECs kuratibu ushirikiano na uoanishaji wa kanuni na viwango, ili kuwezesha utekelezaji wa awamu wa Protokali ya Uhuru wa Watu Kusafiri.

8. **LINAIOMBA** sekta binafsi kufanya kazi pamoja na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na Kamisheni ili kuwezesha utekelezaji wa Protokali ya Uhuru wa Watu Kusafiri Barani Afrika.

9. **LINATOA WITO KWA** ECOSSOC na Asasi za Kiraia kufanya kazi kwa karibu na Kamisheni ili kuchangia katika uhamasishaji wa kuridhiwa kwa Protokali na kuunga mkono juhudi za Nchi Wanachama wa AU kuwezesha uhuru wa watu kusafiri ndani ya Afrika.

10. **LINATOA WITO KWA** wabia wa kimkakati wa Afrika kuendelea kutoa msaada wa kifedha na kitaalamu kwa Nchi Wanachama wa AU, Kamisheni na RECs ili kuwezesha uhuru wa watu kusafiri barani Afrika.

11. **LINAIOMBA** Kamisheni kutoa ripoti kila baada ya miaka miwili (2) kuhusu Hali ya Uhuru wa Watu Kusafiri Barani Afrika.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU (ACHPR)**
**Doc. EX.CL/1573(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti za Shughuli zilizounganishwa, za Hamsini na sita (56) na Hamsini na saba (57) za Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (ACHPR);

2. **LINAELEZA** shukrani zake kwa jitihada zilizofanywa na ACHPR wakati wa kipindi cha mapitio ili kukuza na kulinda haki za binadamu katika bara;

3. **LINAKARIBISHA** maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika, ambapo ACHPR iliandaa Mkutano wa Pamoja uliolenga katika kuendeleza haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, kwa kuzingatia kaulimbiu ya Umoja wa Afrika (AU) kwa mwaka 2024 ya “Kumuelimisha Mwafrika ili Afae kwa Karne ya 21;”

4. **LINAIPONGEZA** ACHPR kwa kuandaa Jukwaa la Kwanza la Pamoja la Mifumo Maalumu mjini Dakar, chini ya kaulimbiu “Kuendeleza Ulinzi na Ukuzaji wa Haki za Binadamu katika Afrika: Kuimarisha Ahadi, Kukabiliana na Changamoto, na Kuimarisha Fursa” ambayo ilitoa jukwaa la mipango ya ushirikiano ya kukabiliana na masuala mtambuka ya haki za binadamu;

**5.** **LINAIPONGEZA** ACHPR kwa kuwa mwenyeji wa Jukwaa la Uzinduzi la kabla ya Mkutano la Nchi zilizoridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na watu, kwa lengo la kuwezesha mjadala wa kudumu na ushirikiano kati ya ACHPR na PRC, kulingana na maelekezo kutoka EX.CL/1045(XXXIV) na EX.CL/1065(XXXV);

6. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuanza kutumika kwa Itifaki mbili muhimu, Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu na Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wazee, na LINAZIHIMIZA Nchi Zilizoridhia Mkataba kujitahidi kufanikisha uridhiaji kwa wote;

7. **LINASIFIA** kupitishwa kwa Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Vipengele Mahususi vya Haki ya Uraia na Utokomezaji wa Hali ya Kutokuwa na Uraia Barani Afrika kulikofanywa na Umoja wa Afrika, pamoja na saini za awali za Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Raia za Ulinzi wa Jamii na Hifadhi ya Jamii;

8. **LINASISITIZA** ombi lake kwa Nchi Wanachama ambazo bado hazijaridhia mikataba mingine ya haki za binadamu ya Umoja wa Afrika kuchukua hatua zote muhimu ili kufanya hivyo;

9. **LINAZIPONGEZA** Nchi zilizoridhia Mkataba wa Afrika ambazo zimekamilisha wajibu wao wa kutoa ripoti na **LINAZIHIMIZA** nchi ambazo hazijawahi kuwasilisha ripoti zao, pamoja na zile ambazo hazijawasilisha zaidi ya ripoti tatu za mara kwa mara, kuziwasilisha kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Mkataba wa Afrika, Ibara ya 26 ya Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watukuhusu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika, na Ibara ya 14 ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuwalinda na Kuwasaidia Watu Waliopoteza Makazi yao Barani Afrika;

10. **LINATOA WITO** kwa Nchi zilizoridhia mkataba kufuata maamuzi yanayotolewa na ACHPR katika Mawasilisho yanayowahusu, pamoja na mapendekezo yaliyotolewa kufuatia shughuli za Uhamasishaji na mapitio ya Ripoti ya Mara kwa mara;

11. **LINAOMBA** rasilimali za kutosha kwa ajili ya Ujumbe wa Pamoja wa ACHPR wa kutafuta ukweli na Kamisheni katika hali ya haki za binadamu nchini Sudani, uliopewa mamlaka na Baraza la Amani na Usalama la UA na **LINAHIMIZA** Serikali ya Sudani, na Nchi za jirani, kushirikiana na ACHPR na kutoa idhini kwa ujumbe wa kutafuta ukweli;

12. **LINAZINGATIA** changhamoto za bajeti zinazoikabili ACHPR katika utekelezaji wa baadhi ya vipengele vya mamlaka yake na **LINAIOMBA** PRC kufikiria kutoa msaada wa kutosha wa bajeti kuisaidia ACHPR ili kuhakikisha utekelezaji wa vipengele muhimu vya mamlaka yake kulingana na utaratibu unaofaa.

13. **LINAIHIMIZA** ACHPR kuimarisha ushirikiano na Nchi zilizoridhia mkataba na Kamisheni, kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu barani Afrika; na

14. **LINAIDHINISHA** uchapishaji wa ripoti za shughuli zilizounganishwa, ya 56 na 57 za ACHPR, kwa kuzingatia michango na maoni yaliyotolewa na Nchi zilizoridhia mkataba.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU (AfCHPR)**
**Doc. EX.CL/1574(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINATAMBUA** Ripoti ya Shughuli za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) kwa kipindi cha kuaniza tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba 2024;

2. **LINAIPONGEZA** Mahakama kwa kazi yake katika kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika, na **LINATOA WITO** kwa Mahakama hiyo kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Nchi Wanachama na wadau wengine wa haki za binadamu barani Afrika, ili kuhakikisha inatekeleza vizuri mamlaka yake.

3. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ishirini na nne (24) ambazo zimeteua Vituo Vikuu vya Kitaifa vya Mahakama, ambazo ni: Algeria, Benin, Botswana, Burkina Faso, Burundi, Cameroon, Cape Verde, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ghana, Lesotho, Liberia, Madagascar, Malawi, Mauritania, Mauritius, Msumbiji, Nigeria, Uganda, Senegal, Afrika Kusini, Tanzania na Zimbabwe, kulingana na uamuzi EX.CL/Dec.1153 (XL), uliopitishwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa 40 wa Baraza Kuu, uliofanyika tarehe 2 - 3 Februari 2022, mjini Addis Ababa, Ethiopia, na **LINAZIALIKA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, kuchukua hatua za kuteua Vituo vyao Vikuu vya Kitaifa.

4. **LINAZINGATIA KWA MASIKITIKO** kwamba zaidi ya miongo miwili baada ya kupitishwa kwake, ni Nchi Wanachama thelathini na nne (34) tu wa Umoja wa Afrika ambazo zimeridhia Itifaki na ni nchi nane tu (8) kati ya Nchi 34 zilizoridhia, zimewasilisha Azimio linalohitajika chini ya Ibara ya 34 (6), ikiruhusu watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasilisha kesi moja kwa moja kwenye Mahakama hiyo;

5. **LINAZIPONGEZA** Nchi thelathini na nne (34) zilizoridhia Itifaki kwa kuwasilisha hati zao za kuridhia, ambazo ni; Algeria, Benin, Burkina Faso, Burundi, Cameroon, Chad, Côte d'Ivoire, Komoro, Congo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Gabon, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Kenya, Libya, Lesotho, Madagascar, Mali, Malawi, Msumbiji, Mauritania, Mauritius, Nigeria, Niger, Rwanda, Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi, Senegal, Tanzania, Togo, Tunisia, Uganda na Zambia.

6. **PIA LINAZIPONGEZA** Nchi nane (8) zilizoridhia ambazo zimewasilisha Azimio chini ya Ibara ya 34(6) ya Itifaki, nchi hizo ni: Burkina Faso, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Malawi, Mali, Niger na Tunisia.

7. **LINAZIALIKA** Nchi Wanachama ambazo hazijafanya hivyo, zikubali Itifaki, na kuwasilisha Azimio linalohitajika chini ya Ibara ya 34 (6) ya Itifaki.

8. **LINATAMBUA** kwa masikitiko kiwango cha chini cha uzingatiaji wa maamuzi ya Mahakama, na **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama ambazo hazijafanya hivyo, kuzingatia kikamilifu maamuzi ya Mahakama.

9. **LINATAMBUA** vikwazo vinavyoikabili Mahakama katika utekelezaji wa Uamuzi EX.CL/Dec.1245(XLIV), ukitoa wito kwa Mahakama ya Afrika na Kamisheni *"kufanya utafiti kuhusu hali ya uzingatiaji wa maamuzi ya mashirika ya haki za binadamu ya Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na, hasa sababu za kiwango cha chini cha uzingatiaji, na kutoa mapendekezo thabiti kwa Baraza Kuu, kuhusu jinsi ya kuimarisha uzingatiaji wa maamuizi hayo kwa Nchi Wanachama."*

10. **LINASISITIZA** haja ya utafiti wa kina kufanyika juu ya suala la utekelezaji wa maamuzi ya mashirika ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika, na kwa lengo hili, **LINAIOMBA** Kamisheni kutoa rasilimali muhimu kwa Mahakama ya Afrika ili kuhakikisha utekelezaji bora wa uamuzi huo, na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu mnamo Julai 2025.

11. **LINAMSIHI** Mwenyekiti wa Kamisheni, kulingana na Maamuzi ya awali, yaani, (EX.CL/Dec.973 (XXXI); (EX.CL/Dec.994 (XXXII); EX.CL/Dec.1044 (XXXIV); (EX.CL/Dec.1064 (XXXV); na (EX.CL/Dec.1079), kuchukua hatua zote muhimu za kuendesha Mfuko wa Msaada wa Kisheria kwa Vyombo vya Haki za Binadamu vya AU, na hivyo, **LINAZIALIKA** na **KUZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika, pamoja na wadau wengine wa haki za binadamu katika bara la Afrika, kutoa michango ya hiari ya ukarimu kwa ajili ya Mfuko huu ili kuhakikisha uendelevu na mafanikio yake.

12. **LINAZINGATIA** kwamba Mahakama ya Afrika itaadhimisha miaka ishirini (20) ya kuwepo kwake mwaka 2026, na **LINAZIALIKA** Nchi zote Wanachama na wadau husika kufanya kazi na Mahakama ya Afrika ili kuandaa shughuli thabiti za kuadhimisha Miaka 20 ya ufanyaji wake wa kazi, na kutoa michango thabiti, juu ya namna gani ya kuimarisha Mahakama, kufanya ijulikane zaidi barani Afrika, na kuifanya ifae kwa kusudi ndani ya maendeleo yanayoendelea ya kijamii na kiuchumi na kisiasa barani Afrika.

13. **LINAPONGEZA** hatua zilizochukuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ujenzi wa majengo ya kudumu ya Mahakama.

14. **LINAIOMBA** Mahakama, kwa kushirikiana na PRC na Kamisheni, kutoa ripoti katika Mkutano wa Kawaida ujao wa Baraza Kuu mnamo Juni/Julai 2025, kuhusu utekelezaji wa Uamuzi huu.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA BARAZA LA KIUCHUMI, KIJAMII NA KIUTAMADUNI (ECOSOCC) – Doc. EX.CL/1575(XLVI**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli ya Mwaka ya ECOSOCC; Hati ya Mfumo iliyorekebishwa kuhusu Utaratibu wa Uidhinishaji Uliowianishwa wa AU na rasimu ya Mfumo wa Kitaasisi kuhusu Uwakilishi wa Dayaspora katika ECOSOCC.

**A. KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA ECOSOCC;**

2. **LINAIPONGEZA** ECOSOCC kwa kuadhimisha vyema Maadhimisho ya Miaka 20 ya ECOSOCC mwaka 2024 na kuitishwa kwa Kikao cha Pili cha Mkutano Mkuu wa 4 wa Kudumu wa ECOSOCC, ikiwa ni pamoja na kufanya uchaguzi wa wanachama wapya wa ECOSOCC na chaguzi za uongozi wa ECOSOCC, ikiwa ni pamoja na wajumbe wa Ofisi na Kamati ya Kudumu

3. **LINAWASHUKURU** na **KUWAPONGEZA** Wajumbe wapya waliochaguliwa wa Ofisi na Kamati ya Kudumu ya Mkutano Mkuu wa 4 wa Kudumu wa ECOSOCC.

**B. KUHUSU MAPITIO YA VYOMBO VYA SHERIA ZA ECOSOCC**

4. **LINAZINGATIA** maendeleo makubwa yaliyopatikana katika mchakato wa mapitio ya vyombo vya kisheria vya ECOSOCC na **LINAELEKEZA** Sekretarieti ya ECOSOCC kuanza mchakato wa uthibitishaji wa rasimu ya hati hizi. Maandishi ya rasimu yaliyorekebishwa yanapaswa kuwasilishwa katika kikao kijacho cha STC ya Haki na Masuala ya Kisheria mwaka wa 2025.

**C. KUHUSU MIFUMO YA TAASISI YA USHIRIKIANO BORA WA AZAKI NA UMOJA WA AFRIKA.**

5. **LINATAMBUA** Mfumo wa Uwiano wa AU uliohakikiwa kwa ajili ya kutoa hadhi ya Uangalizi na Ushauri kwa Asasi za Kiraia na marekebisho yaliyoletwa na Kamati ya Kudumu ya Wawakilishi.

6. **LINAIDHINISHA** Mfumo uliokebishwa na **LINAIOMBA** ECOSOCC kufanya kazi kwa ushirikiano na Kamisheni, Vyombo vya AU na Nchi Wanachama kwa utekelezaji wake wa kiutendaji.

7. **LINAKUBALI** mfumo wa kitaasisi wa AU uliorekebishwa kwa ajili ya uwakilishi wa AZAKi za watu wanaoishi nje ya nchi katika ECOSOCC na marekebisho yaliyofanywa na PRC.

8. **LINAIDHINISHA** mfumo wa kitaasisi wa uwakilishi wa AZAKi za dayaspora katika ECOSOCC na **LINAISHAURI** ECOSOCC kuharakisha utendakazi wake.

9. **LINAISIHI** ECOSOCC kuendelea na mashauriano na Nchi Wanachama kuhusu Mfumo Uliooana wa AU kwa ajili ya kutoa hadhi ya mwangalizi kwa AZAKi na Mfumo wa Kitaasisi wa uwakilishi wa AZAKi za Diaspora katika ECOSOCC na kuhakikisha kuwa Utekelezaji wa Mifumo hii utakuwa kwa mashauriano na Nchi Wanachama.

## D. KUHUSU HATI YA ECOSOCC KUHUSU FIDIA KWA WAAFRIKA NA WATU WENYE ASILI YA AFRIKA NA NAFASI YA UMOJA WA AFRIKA

**LIKIKUMBUKA** uamuzi wa kihistoria wa Kikao cha Thelathini na Sita cha Kawaida cha Wakuu wa Nchi na Serikali, kilichofanyika tarehe 18 hadi 19 Februari 2023, Addis Ababa, Ethiopia, kuhusu "kujenga umoja wa kuendeleza haki na malipo ya fidia kwa Waafrika";

**LIKIKUMBUKA ZAIDI** kutangazwa kwa Kaulimbiu ya Mwaka 2025 ya AU: "Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Kiafrika kwa njia ya Fidia," kwa kutambua umuhimu wake katika kuendeleza mjadala wa haki na hatua za fidia kwa waaathiriwa wa dhulma za kihistoria;

**LIKISISITIZA** kwamba kutafuta fidia ni dhima ya kimaadili na kisheria inayojikita katika kanuni za haki, haki za binadamu na utu wa kibinadamu na kwamba inawakilisha dhamira imara ya kushughulikia makosa ya kihistoria na kuendeleza upatanisho kati ya watu wa Afrika na watu wa asili ya Afrika;

**LIKITHIBITISHA** jukumu la Asasi za Kiraia za Kiafrika (CSOs) kama washirika muhimu wa kutekeleza dhamira ya AU ya kushughulikia dhuluma za kihistoria na kukuza fidia kama njia ya haki ya kijamii na kiuchumi, uthabiti na kuangazia historia kwa mataifa na jamii za Kiafrika zilizoathiriwa na dhuluma;

**LIKITHIBITISHA TENA** jukumu muhimu la ECOSOCC katika kuhamasisha sauti za asasi za kiraia za Afrika kuhusu ajenda ya AU na hivyo kutekeleza dira ya AU inayozingatia watu;

10. **LINAKARIBISHA** Hati ya Asasi za Kiraia kuhusu Fidia kama mfumo wa kutumia utaalamu wa wadau wa asasi za kiraia barani Afrika katika kuunga mkono Msimamo wa Pamoja wa Afrika na Mpango wa Utekelezaji wa Fidia;

11. **LINAIPONGEZA** ECOSOCC kwa kuratibu ubadilishanaji mada kuhusu ulipaji fidia kati ya watu na watu, na hasa kuangazia uzoefu wa jamii za makundi kutoka bara

zima ili kufahamisha na kuongoza jitihada za bara hili za ulipaji fidia kama ilivyoelezwa kupitia tamko la Kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya 2025 ya Mwaka;

12. **LINAPENDEKEZA** Hati ya Asasi za Kiraia kuwa sehemu muhimu ya chombo cha kitaasisi cha maarifa kuhusu ulipaji fidia na hati ya msingi ya kufanya kazi ili kufahamisha kazi ya Kamati ya Wataalamu wa Kiafrika juu ya Fidia, mara tu baada ya kuundwa, katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuendeleza Jamii ya Afrika kwa Nafasi na Mpango wa Utekelezaji wa Malipo.

13. **LINAIOMBA** ECOSOCC, kwa kushirikiana na Tume na vyombo vingine vinavyohusika vya Muungano, kuandaa mfumo wa utetezi ili kuwezesha mchango kamili na endelevu wa wadau wa asasi za kiraia barani humu na katika dayaspora ya Afrika katika ajenda ya malipo ya Umoja wa Afrika; ikilenga hasa maeneo muhimu ya kisera kama vile:

    (i) Kampeni ya asasi za kiraia za bara kuunga mkono marekebisho ya mifumo ya fedha ya kimataifa, masharti ya biashara, haki ya hali ya hewa na msamaha wa madeni kwa mataifa ya Afrika kama vipengele muhimu vya haki ya upatanisho;

    (ii) Kuanzishwa Mfumo wa Uratibu Mkuu wa Umoja wa Afrika (CCM) kuhusu Fidia; kitakachoundwa kwa vyombo na taasisi za Umoja wa Afrika zinazoshughulikia kaulimbiu hiyo, ikiwa ni pamoja na ECOSOCC, CIDO, Tume ya Afrika ya Haki za Kibinadamu na Watu, Bunge la Afrika, miongoni mwa mengine, kuratibu juhudi za Umoja wa Afrika za ulipaji wa kitaasisi, kufuatilia maendeleo, na kuhakikisha utoaji wa taarifa kwa vyombo vya sera na nchi wanachama.

    (iii) Kutumia utaalamu na mitandao ndani ya asasi za kiraia za Kiafrika, kama vile vyuo vikuu, taasisi za utafiti, na makundi ya ushauri, ili kutoa kipaumbele kwa mafunzo ya fidia na kuundwa shirika la Kiafrika kuhusu fidia, na hivyo kukuza msingi wa maarifa katika bara zima kusaidia sera na kufanya maamuzi ya kisiasa kuhusu fidia.

    (iv) Kubuni mbinu za kurejesha vifaa vya maarifa ya Kiafrika, vitabu, hati za maandishi, na kazi za sanaa ambazo zilitolewa kutoka Afrika wakati wa Biashara ya Utumwa katika Bahari ya Atlantiki na ukoloni.

# UAMUZI
# KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA BODI YA USHAURI YA UMOJA WA AFRIKA DHIDI YA RUSHWA (AUABC) – DOC. EX.CL/1576(XLVI)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya 16 ya Shughuli ya Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika dhidi ya Rushwa;

2. **LINAELEZA SHUKRANI** zake kwa shughuli zinazofanywa na Bodi ya kuendeleza harakati za kupambana na rushwa katika bara hili na haswa kwaajili ya kufanya uchunguzi kuhusu hali ya ufichuzi katika nchi wanachama wa AU kutokana na jukumu kubwa la ufichuaji katika kupambana rushwa;

3. **LINAZISIHI** Nchi wanachama ambazo hazisaini Mkataba kuchukua hatua zinazofaa kuusaini, kuridhia na kukubaliana na Mkataba huo;

4. **LINATOA WITO** kwa Nchi Zilizoridhia ambazo hazijakaguliwa kukubali maombi ya Bodi kwaajili ya Misheni za mapitio ili kuwezesha Bodi kutathmini hali ya Utekelezaji wa Mkataba na kukamilisha taratibu za Utekelezaji wa Mkataba na kukamilisha michakato ya kuripoti ya Nchi**;**

5. **LINATOA WITO** kwa Nchi Zilizoridhia ambazo haziwasilisha ripoti zao za msingi kufanya hivyo;

6. **LINAIDHINISHA** Kaulimbiu ya Siku ya Afrika ya Kupambana na Rushwa na Mdahalo wa Afrika wa Kupambana na Rushwa kwa mwaka 2025, ambayo ni **"Kukuza Utu wa Binadamu katika Mapambano dhidi ya Rushwa".**

7. **LINAZIOMBA** mamlaka za Tanzania kukamilisha michoro ya Usanifu wa muundo wa kudumu unaopendekezwa na kuuwasilisha kwa Bodi ili ikaguliwe na kuudhinishwa na Kamisheni ya AU**;**

8. **LINAISIHI** Kamisheni kuwezesha mchakato sahihi na kuharakisha utekelezaji wa uamuzi EX.CL/Dec.1200 (XLII) kuhusiana na makazi ya Mwenyekiti kwenye makao makuu ya Bodi mjini Arusha kwa mwaka uliopo.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA BUNGE LA AFRIKA (PAP)**
**Doc. EX.CL/1577(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli ya PAP, ikijumuisha Maazimio na Mapendekezo yaliyopitishwa wakati wa Vikao vyake vya Kawaida vya Juni, Agosti na Novemba 2024;

2. **LINAZINGATIA ZAIDI** kufanikiwa kufanyika kwa Mkutano Maalumu mwezi Machi 2024, kwa mujibu wa EX.CL/Dec.1242(XLIV)

3. **LINAZINGATIA** matokeo ya kikundi kazi kinachoundwa na Kamisheni, PAP na Balozi wa Jamhuri ya Kongo, mjumbe wa Uongozi (*Bureau*) wa PRC, juu ya kutofautiana kati ya itifaki ya PAP na Kanuni zake za Utaratibu kuhusu mamlaka ya wajumbe wa Uongozi wa PAP.

4. **LINAPITISHA kuwa** muda wa Uongozi wa sasa uongezwe kwa miezi saba (7) kuanzia tarehe 01 Julai 2025 kutokana na hali ya mgogoro iliyoikumba PAP mwaka 2023;[2]

5. **LINAAMUA** kuwa chaguzi za uongozi wa PAP ufanyike Februari 2026;

6. **LINATOA MAMLAKA** kwa PRC kupitia Kamati Ndogo ya Kanuni, Viwango na Uthibitishaji wa Sifa na Taratibu, kwa kushirikiana na Kamisheni na PAP, kukamilisha kupatanisha Kanuni za Utaratibu na Itifaki ya PAP kuhusiana na mamlaka na kusisitiza kanuni ya mzunguko na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu mnamo Julai 2025;

7. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuweka Sheria ya Mfano kuhusu vyama vya ushirika barani Afrika na Sheria ya Mfano kuhusu Usalama wa Chakula na Lishe barani Afrika katika mifumo yao ya kisheria ya kitaifa; na **LINAIHIMIZA ZAIDI** PAP kuendelea na kazi yake ya utungaji wa Sheria nyingine za Mfano katika maeneo mbalimbali yenye mada kwa ushirikiano na Vyombo vingine vya AU na STCs husika za AU;

8. **LINAIOMBA** PRC, kupitia Kamati Ndogo husika, kufikiria upya bajeti ya 2026 ya PAP na Bajeti ya nyongeza ya 2025 ili kuwezesha Bunge kukidhi mahitaji yake ya kiutendaji, ikiwa ni pamoja na kuajiri wafanyakazi wa usimamizi mkuu na wa huduma muhimu za bunge na za lugha, na uwekaji kamili kidijitali wa Ukumbi wa Bunge, na kutimiza wajibu wake ipasavyo, kuhakikisha utawala bora wa kitaasisi na kupunguza shinikizo lisiloepukika kwenye bajeti ya uendeshaji ya PAP;

[2] Reservation entered by the Republic of Botswana

9. **AIDHA LINAIOMBA** PRC, kupitia Kamati Ndogo husika, kupitia uamuzi EX.CL/Dec.1057(XXXV) kuhusu Uoanishaji wa Posho na Manufaa kwa Vyombo vya Uamuzi wa Umoja wa Afrika ili kurejesha mishahara ya Wabunge wa PAP ili kuwezesha PAP na Wabunge wake kufanya kazi ipasavyo;

10. **LINAAMUA** kuanzishwa kwa kikao kazi cha pamoja cha PAP-PRC, na PAP-PSC, ili kuimarisha ushirikiano na kukuza ushirikiano katika kushughulikia changamoto za utangamano wa bara zinazowakabili raia wa Afrika;

11. **LINAIOMBA** PAP, Kamisheni na PRC kutoa ripoti kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Uamuzi huu katika Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA TUME YA UMOJA WA AFRIKA YA SHERIA ZA KIMATAIFA (AUCIL)**
**Doc. EX.CL/1578(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAPOKEA** ripoti ya Shughuli ya AUCIL ya kipindi cha Julai 2023 – Januari 2025, na mapendekezo yaliyomo**;**

2. **PIA LINAZINGATIA** mada mbalimbali za kisheria zinazotolewa na tafiti zinazofanywa na AUCIL na **LINAIPONGEZA** AUCIL kwa tafiti kadhaa kuhusu sheria za kimataifa zilizokamilika hadi sasa;

3. **AIDHA LINAPOKEA KWA WASIWASI** rasilimali zisizotosheleza zinazotolewa kwa AUCIL ambazo zinaathiri ufanisi wake na **LINAREJEA** Uamuzi wake EX.CL/Dec.1176(XLI) unaoitaka PRC na Kamisheni kushirikana kwa karibu na AUCIL na kuipa nyenzo muhimu kwaajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

4. **LINAKUMBUKA** Uamuzi Assembly/AU/Dec. 821(XXXV) uliofanyia marekebisho mkataba wa AUCIL na kuwezesha uhamishaji wa Sekretariati yake, pamoja na uamuzi EX.CL/Dec.1243(XLIV) unaoitaka Kamisheni kufanya shughuli ya tathmini ya kuwa mwenyeji wa AUCIL na kuripoti kwa Vyombo vya Sera mnamo Februari 2025;

5. **PIA LINAKUMBUKA** uamuzi Assembly/AU/Dec.850(XXXVI) uliopitisha muundo wa Sekretarieti ya AUCIL na kutoa nafasi ya kuajiri watumishi kumi na watano kwa awamu ya kwanza kuanzia 2023 mpaka 2025;

6. **LINAAMUA** kama ifuatavyo:

   (i) **LINAIOMBA** Kamisheni ikisaidiwa na Kamati ndogo husika za PRC kuharakisha misheni za tathmini za kuwa mwenyeji wa AUCIL na kutoa ripoti kwa Vyombo vya Sera mnamo Februari 2026;

   (ii) **LINAISIHI** PRC na Kamisheni kuharakaisha utekelezaji wa muundo mpya wa Sekretarieti ya AUCIL na kuipa AUCIL nyenzo muhimu ili kutekeleza majukumu yake;

7. **LINAIPONGEZA** AUCIL kwa kufanikisha Kongamano la 10 lenye Kaulimbiu *“Sheria ya Kimataifa, Haki Mbadala na Migogoro ya Kutumia Silaha Barani Afrika”* na **LINAIOMBA** AUCIL kusambaza matokeo ya Jukwaa hilo kwa Nchi Wanachama na wadau wengine husika.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA KAMATI YA AFRIKA YA WATAALAMU WA HAKI NA USTAWI WA MTOTO (ACERWC)**
**Doc. EX.CL/1579(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati ya Afrika ya Wataalamu wa ya Haki na Ustawi ya Mtoto.

2. **LINAPITISHA** Ripoti na kuipongeza Kamati kwa kazi inayofanywa katika kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi ya Mtoto.

3. **LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi[3] kwa kuridhia Mkataba wa Watoto wa Afrika na **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijaridhia Mkataba wa Watoto wa Afrika ili kuharakisha uridhiaji wa Mkataba huo.

4. **LINAZIPONGEZA** Nchi zilizoridhia Mkataba huo ambazo zimewasilisha ripoti zao juu ya uekelezaji wa Mkataba wa Watoto wa Afrika na kuzisihi Nchi zilizoridhia Mkataba ambazo bado hazijaripoti kwa Kamati kuzingatia wajibu wao wa utoaji wa ripoti.

5. **LINASHUKURU** Nchi wanachama kwa hatua walizochukua katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika kwa Mwaka 2024 juu ya kaulimbiu- “Haki ya Elimu kwa Watoto Wote Afrika-Wakati ni Sasa” na kuhimiza Nchi Wanachama kutekeleza mapendekezo ya Kamati na kuyatolea ripoti.

6. **LINAZISHUKURU** Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania kwa hatua walizochukua katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati, na **KUZIHIMIZA** kuzingatia kikamilifu Maoni na Mapendekezo ya ACERWC.

7. **LINASISITIZA** uamuzi wa Baraza Kuu kuhusu Kaulimbiu ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2025 kuwa juu ya ***'Kuandaa mipango na Kupanga Bajeti ya Haki za Watoto: Maendeleo tangu 2010*'.**

8. **LINAZISHUKURU** Jamhuri ya Malawi, Msumbiji, Zimbabwe, Rwanda, Zambia na Namibia kwa kuwasilisha ripoti zao za mara kwa mara kwa ACERWC na **KUHIMIZA** Nchi Zilizoridhia Mkataba kutekeleza mapendekezo ya Kamati.

9. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuchukua hatua za kisheria ili kuhakikisha elimu ya msingi bila malipo na ya lazima na hatua kwa hatua elimu ya sekondari bila malipo; kutoa maendeleo ya awali ya utoto; kusimamia shule za binafsi; kupiga marufuku aina zote za vikwazo vya kupata elimu; na kuhakikisha elimu jumuishi.

---

22. [3] Reservation expressed by the Kingdom of Morocco

10. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama husika kutekeleza mapendekezo ya ACERWC kutoka kwenye utafiti wa mwaka 2019 kuhusu '*Mapping children on the move within Africa*'.

11. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama husika kushughulikia matatizo ya watoto katika mazingira ya migogoro na kuwalinda watoto dhidi ya wanyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji wa kijinsia Pamoja na uraibu wa dawa za kulevya na biashara ya dawa za kulevya katika bara la Afrika.

12. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kushughulikia changamoto za watoto waliofungwa na wazazi na walezi wao na kuimarisha utekelezaji wa Ibara ya 30 ya Mkataba wa Watoto wa Afrika kwa kutoa ulinzi wa kisheria ili kuweka kipaumbele kwa hukumu zisizohusisha kufungwa jela.

13. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama husika kushughulikia changamoto za Watoto wenye ualbino.

14. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuadhimisha miaka 35 ya kupitishwa kwa Mkataba Wa Watoto wa Afrika na kushirikiana na ACERWC kuhusu hilo.

15. **LINAISHUKURU** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua iliyochukua kutekeleza mapendekezo ya ACERWC katika muktadha wa Mawasiliano No: 0012/Com/001/2019 katika suala *kati ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Kituo cha Haki za Uzazi (kwa niaba ya wasichana wa Tanzania) dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*, na **LINAHIMIZA** Nchi hiyo iliyoridhia kuzingatia kikamilifu uamuzi na mapendekezo ya ACERWC.

16. **LINAIHIMIZA** Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria, Nchi ya Eritrea, Jamhuri ya Malawi, Jamhuri ya Ghana, na Jamhuri ya Burundi kuendelea kushirikiana na ACERWC katika muktadha wa Mawasiliano yanayosubiri.

17. **LINAPITISHA** 'Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya Umoja wa Afrika' na **LINAIOMBA** Kamisheni kuendesha na kutekeleza sera hiyo kwa kushirikiana na ACERWC.[4]

18. **LINAIHIMIZA** Jamhuri ya Sierra Leone kutekeleza mapendekezo ya ACERWC kwa kutumia kifungu kinachozuia kwa uwazi ukeketaji wa wanawake katika Sheria ya Haki za Mtoto.

19. **LINAKARIBISHA** shughuli zilizofanywa, maazimio, tafiti na viwango vilivyoundwa na Vikundi Kazi vya ACERWC, na **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kutumia mbinu hizo ndani ya ACERWC.

20. **LINAPONGEZA** Ufalme wa Lesotho kwa kuhakikisha kufanyika vizuri shughuli za Sekretarieti ya ACERWC; na **LINAHIMIZA** nchi mwenyeji kuendelea kutoa mahitaji

23. [4] Reservation expressed by the Federal Democratic Republic of Ethiopia

kulingana na makubaliano ya nchi mwenyeji, ikiwa ni pamoja na ujenzi kwa wakati wa majengo ya kudumu ya ofisi.

21. **LINAIOMBA** Kamisheni kuharakisha kumalizika kwa mchakato wa kuajiri wafanyakazi wa Sekretarieti ya ACERWC na kutoa mwongozo juu ya uwezekano wa kuruhusu ACERWC kuajiri wafanyakazi wake.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA VITUO VYA KUDHIBITI MAGONJWA AFRIKA (AfCDC)-**
**EX.CL/1581(XLVI)**

**Baraza Kuu**

1. **LINAKARIBISHA** Ripoti ya Africa CDC na **KUPONGEZA** hatua iliyofikiwa mwaka 2024, hususan kutangaza na kusimamia mlipuko wa Mpox kama Dharura ya Afya ya Umma ya Usalama wa Bara (PHECS) na juhudi za ushirikiano katika kushughulikia Marburg, kipindupindu, ugonjwa wa mlipuko usio na sababu inayojulikana, Homa ya Lassa, na milipuko mingine.

2. **LINATAMBUA** kazi kubwa inayotekelezwa na Africa CDC katika kulinda afya ya umma barani Afrika kwa kutoa mwelekeo wa kimkakati, kujenga uwezo na uwezo wa Nchi Wanachama katika kujiandaa, kuzuia, na kukabiliana na vitisho vya magonjwa na milipuko ya afya.

3. **LINAZINGATIA KWA KUPONGEZA** maendeleo katika uendeshaji wa Africa CDC, ikiwa ni pamoja na mchakato wa kuajiri chini ya muundo ulioidhinishwa na maendeleo katika kuanzisha Vituo vya Uratibu vya Kikanda (RCCs).

4. **LINAELEZEA WASIWASI WAKE** juu ya kuongezeka kwa idadi ya milipuko mipya kama vile AMR (usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Anti-Microbial Resistance)) inayoathiri Nchi zote Wanachama, Mpox inayoathiri takriban 50% ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, Marburg, kipindupindu, Ugonjwa X, kidingapopo (dengue), homa ya Lassa, na mingine, ambayo inaweza kusababisha majanga makubwa ya magonjwa ya Afrika ikiwa hayatasimamiwa ipasavyo kwa sababu ya uhaba wa rasilimali watu na fedha, udhaifu katika mifumo ya afya, na ukosefu wa bidhaa za afya.

5. **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika kutekeleza Assembly/AU/Dec.880 (XXXVII) katika kuanzisha mfumo wa uwajibikaji ili kutekeleza vizuri Ajenda ya Lusaka ya kuimarisha Mipango ya Afya Duniani (GHIs), kwa kushirikiana na Kamisheni, kufanikisha Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) barani Afrika.

6. **LINAELEZA WASIWASI** kuhusu upungufu unaozidi kuongezeka wa uratibu na utayari miongoni mwa Nchi Wanachama wakati wa kuhudhuria mikutano ya bodi na Mipango mbalimbali ya Afya Duniani na Majukwaa mengine ya Afya ya Dunia, hivyo kusababisha mbinu iliyogawanyika ambayo inadhoofisha ajenda ya Afrika katika ngazi ya kimataifa.

7. **LINAKUMBUKA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.835(XXXV) kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko Afrika (AfEF), unaosisitiza kwamba utayari na mwitikio mzuri wa dharura wa Afrika kwa milipuko ya siku za usoni vinahitaji mbinu bunifu na thabiti za ufadhili zinazohakikisha ufikiaji kwa wakati katika ngazi za kikanda na kitaifa kupitia rasilimali sahihi za kiufundi na kifedha.

8. **LINAMPONGEZA** Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Mhe. Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania, akisaidiwa na Mtetezi wa Afrika kuhusu Uzuiaji, Utayari na mwitikio kwa majanga ya magonjwa Mhe. Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini na Mhe. Mousa Faki Mahamat, Mwenyekiti wa Kamisheni kwa uongozi na mwongozo wao uliotolewa kwa Africa CDC kwa ajili ya mwitikio wa kupambana dhidi ya Mpox na milipuko mingine.

9. LINAIPONGEZA Africa CDC, AfreximBank, na UNECA kwa hatua nzuri zilizopigwa kuelekea utengenezaji wa ndani wa bidhaa za afya ndani ya Afrika kupitia jukwaa la PHAHM (*Platform for Harmonized African Health Manufacturing*) na uendeshaji mzuri wa APPM (*African Pooled Procurement Mechanism*).

10. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama zinazopiga hatua katika utengenezaji wa ndani ikiwa ni pamoja na Algeria, Benin, Botswana, Burkina Faso, Cameroon, Cape Verde, Cote d'Ivoire, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Egypt, Eritrea, Ethiopia, Ghana, Guinea, Kenya, Lesotho, Liberia, Madagascar, Malawi, Mali, Mauritius, Moroko, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, Senegal, Sierra Leon, Afrika Kusini, Sudan, Tanzania, Togo, Tunisia, Uganda, Zambia, Zimbabwe katika eneo la utengenezaji wa ndani wa chanjo, dawa, vifaa vya uchunguzi na matibabu.

11. **LINAAMUA** kuupa jijna mpango wa ufadhili wa utengenezaji wa ndani kuwa "Mpango wa Rais Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani wa Kufadhili Utengenezaji wa Ndani wa Bidhaa za Afya barani Afrika," kwa kutambua uongozi na msaada usioyumba kutoka kwa Mhe. Rais Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani, Rais wa Mauritania na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, katika kukusanya dola za Marekani bilioni 3.2 ili kusaidia ajenda ya Africa CDC ya utengenezaji wa ndani wa chanjo, dawa, vifaa vya uchunguzi, na bidhaa zingine za afya.

12. **LINAZINGATIA** kazi inayofanywa na Africa CDC ili kuhakikisha uhakika wa mahitaji na kutabirika kupitia ahadi ya nchi wanachama ya kununua bidhaa za watengenezaji wa Afrika kwa ajili ya uendelevu wa watengenezaji waliopo barani Afrika.

13. **LINATAMBUA** jitihada endelevu za Africa CDC za kukusanya fedha kutoka kwa wabia mbalimbali ili kusaidia Nchi Wanachama katika kukabiliana na milipuko mbalimbali na **LINAKARIBISHA** Vyombo vya Sera vya AU kwa utengaji ulioongezeka wa fedha kwa Africa CDC kwa muundo ulioidhinishwa wa idadi ya chini ya wafanyakazi 312 wa kulipwa na Nchi Wanachama, jambo ambalo litahakikisha utendaji kamili wa shirika na uwezo wa kutekeleza mamlaka yake;

14. **LINAZINGATIA** maendeleo katika uendeshaji wa Africa CDC, **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kwa msaada endelevu na ushirikiano wa karibu na Africa CDC katika kukabiliana na dharura za afya ya umma zinazolikumba bara.

15. **LINATOA WITO KWA NCHI WANACHAMA:**

(i). Kusaidia jitihada za Africa CDC za kujiandaa, kuzuia, na za kukabiliana na matishio yanayoendelea na yajayo ya afya ya umma.

(ii). Kuunga mkono mbinu bunifu ya ufadhili inayoongozwa na Mtetezi wa AU kuhusu rasilimali za ndani, Mhe. Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, ili kutumia rasilimali zaidi kwa Africa CDC na Vyombo vingine vya AU vinavyohusika na masuala ya afya kubadilika kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kimataifa kuhusiana na kupungua kwa ufadhili wa afya ya kimataifa na kusaidia vizuri zaidi Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika.

(iii). Kuongeza mgao wa ufadhili kwa Africa CDC ili kuhakikisha uendeshaji wa muundo unaofaa kwa Africa CDC ili kusaidia vyema Nchi Wanachama.

(iv). Mbali na wadau wote kushiriki kikamilifu katika Africa Health ExCon ya 2025, iliyoandaliwa kwa pamoja na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Africa CDC, kukuza uzalishaji wa ndani na kuendeleza ajenda ya usalama wa afya ya bara.

16. **LINAIDHINISHA** mfumo wa utawala wa Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko (AfEF), kama ilivyoelekezwa na Uamuzi Assembly/AU/Dec.835(XXXV, ili kuhakikisha mwitikio kwa wakati kwa dharura za afya ya umma.

17. **LINATAMBUA NA KUIDHINISHA** jukumu la Africa CDC, kwa mujibu wa Sheria zake, kama wakala wa afya ya umma wa Afrika ili kusimamia kikamilifu na kwa kina masuala yote ya afya ya umma barani Afrika, kwa kushirikiana na Kamisheni, AUDA-NEPAD, Wakala wa dawa Afrika (AMA), AFCFTA na vyombo na taasisi zingine, ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusiana na ufadhili wa afya, utengenezaji wa ndani, Utaratibu wa Ununuzi wa Pamoja wa Afrika (African Pooled Procurement Mechanism), kujenga uwezo, ushirikishwaji wa jamii, mifumo ya taarifa za afya, na uvumbuzi.

18. **LINAIAGIZA** Africa CDC kuunganisha sauti ya Nchi Wanachama wanaowakilisha bara katika mipango mbalimbali ya afya (GHIs), **LINAIHIMIZA** Africa CDC kuwasilisha maombi ya kuwa mjumbe wa bodi wa mipango hii (GHIs) ili kuunga mkono vyema ajenda ya Afrika.

19. **LINAIAGIZA** Africa CDC kuendelea kuongoza Ajenda ya Lusaka kwa ushirikiano na vyombo na idara zote za AU kwa mujibu wa ibara ya 3(k) ya Mkataba wa Africa CDC na kutumika kama Sekretarieti ya mpango huu, kusaidia ajenda ya ufadhili unaofaa wa mifumo ya afya barani Afrika, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa rasilimali za ndani.

20. **LINAIHIMIZA** Africa CDC kuendelea kusaidia Nchi Wanachama katika majadiliano ya Mkataba wa Janga la Ugonjwa (Pandemic Agreement), yatakayokamilishwa wakati wa Mkutano wa Afya Duniani wa 2025, na kutoa ripoti kwa Mkutano Mkuu.

21. **LINAVISIHI** Vyombo vyote vya Umoja wa Afrika, Taasisi, Nchi Wanachama, na wabia wa nje kuimarisha ushirikiano wao na Africa CDC ili kuhakikisha mwitikio

jumuishi na uliowiana kwa changamoto za afya, ikiwa ni pamoja na dharura za afya ya umma, katika kutekeleza Agizo Jipya la Afya ya Umma.

22. **LINAIAGIZA** Africa CDC kutoa taarifa juu ya kazi yake na kutoa ripoti kwa Mkutano wa Kawaida wa 47 wa Baraza Kuu wa Julai 2025.

23. **LINAAMUA** kuendelea kushughulikia suala hilo.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA *AFRICAN RISK CAPACITY (ARC*)**
**Doc. EX.CL/1582(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINATAMBUA** michango muhimu ya *African Risk Capacity* (ARC) katika kuimarisha uwezo wa Nchi Wanachama wa AU kupanga, kuandaa, na kukabiliana kwa matokeo na matukio ya hali ya hewa kali, majanga ya asili, na dharura nyingine;

2. **LINATAMBUA** faida kubwa kwa Nchi Wanachama katika kushiriki katika mipango ya ARC, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mipango ya kujenga uwezo, zana za juu za kupanga dharura, mifumo ya onyo la mapema, usimamizi wa hatari ya maafa ya jinsia, na uhusishaji katika bima za majanga ya ARC unaoshughulikia ukame, vimbunga vya kitropiki, magonjwa, na mafuriko.

3. **LINAHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa AU kuweka kipaumbele katika kuridhia au kujiunga na Mkataba wa ARC ili kuimarisha umiliki, kuongeza ushirikiano, na kuhakikisha uendelevu wa kazi muhimu ya ARC;

4. **LINATOA WITO** kwa Nchi zote Wanachama kushirikiana kikamilifu na ARC kwa kutumia utaalamu wake wa kiufundi, kushiriki katika vikao vya kuelimishana, na kutumia rasilimali zake kufanya maamuzi yanayonufaisha kuhusiana na usimamizi wa majanga na fedha;

5. **LINATAMBUA** umuhimu wa kukuza ushirikiano wa karibu na ushiriki kati ya ARC na Vyombo na mashirika ya AU**,** ikiwa ni pamoja na PRC na Baraza Kuu;

6. **LINASISITIZA** umuhimu mkubwa wa malipo ya kawaida ya uanachama na michango kutoka kwa Nchi Wanachama ili kuhakikisha uendelevu wa taasisi muhimu za AU kama vile shughuli na programu za ARC. Kwa vile Michango ya kawaida ya kifedha haitaongeza tu uwezo wa ARC kukabiliana na dharura bali pia itaonyesha umiliki wa pamoja na dhamira ya kujenga ustahimilivu katika bara lote.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPPOTI YA SHUGHULI YA TAASISI YA UJENZI WA UWEZO YA AFRIKA (ACBF)- Doc. EX.CL/1583(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti iliyowasilishwa na ACBF kuhusu shughuli zake kwa mwaka 2024.

2. **LINAIPONGEZA** ACBF kwa mafanikio yaliyopatikana katika uwanja wa Kijamii na Kiuchumi wa Bara la Afrika.

3. **LINAZINGATIA** kwa kuridhika sana utekelezaji wa uamuzi EX.CL/Dec.1160 kupitia mafunzo ya wanadiplomasia yaliyofanyika Februari 2024 kuhusu AfCFTA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo kamati ya AfCFTA.

4. **LINATOA WITO** kwa ACBF kuandaa vikao sawa kuhusu mada mbalimbali za maslahi kwa wanadiplomasia waliotumwa kwenye misheni za kudumu katika AU.

5. **LINAIOMBA** ACBF kuandaa semina kuhusu Kaulimbiu ya Mwaka 2025 ya AU inayoongozwa na wanahistoria wa Afrika, mafunzo kuhusu usalama wa mtandao kwa kushirikiana na wabia wa AU na warsha ya ujasiriamali wa vijana na uundaji wa biashara changa kama sehemu ya kujenga uwezo katika eneo la uundaji wa biashara na uwasilishaji wa fursa za upatikanaji wa ufadhili katika ngazi ya bara na kimataifa.

6. **LINAHIMIZA** ACBF kuandaa orodha ya mahitaji ya mafunzo kwa kushauriana na PRC.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI ZA SHIRIKA LA AFRIKA LA KAHAWA (IACO)-Doc. EX.CL/1585(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya shughuli ya IACO na MoU iliyosainiwa kati ya AU na IACO mnamo Novemba 2024.

2. **LINASISITIZA** uamuzi wake kuhusu umuhimu wa kahawa katika mtangangamano wa kiuchumi wa na Utekelezaji wa Agenda ya AfCFTA.

3. **LINAKUMBUKA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.899(XXXVII) wa Februari 2024 ulioteua Shirika la Afrika la kahawa (IACO) kama wakala wa Afrika mbobezi wa kahawa ili kushirikiana na Kamisheni na Nchi Wanachama kwaajili ya mageuzi yenye tija ya mnyororo wa thamani Afrika kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa AfCFTA katika kukuza biashara ya kilimo ndani ya Afrika.

4. **LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kwa kuandaa kwa mafanikio Mkutano wa Kahawa wa Afrika mwaka 2024.

5. **LINAKARIBISHA** IACO na Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa tatu (3) wa Wakuu wa Nchi wa G25 jijini Dar es Salaam, Tanzania mnamo tarehe 21 na 22 Februari 2025, na mkutano wa pili (2) wa Wiki ya Kahawa kuanzia tarehe 24 hadi 28 Februari 2025 na linaiomba Kamisheni kutoa msaada unaohitajika kwa IACO na Tanzania kufanikisha Mkutano wa tatu wa Wakuu wa Nchi wa G25**.**

6. **LINAZIOMBA** Kamisheni na IACO kutekeleza makubaliano yalisainiwa baina ya pande husika na kuzijengea uwezo nchi wanachama katika masuala ya kahawa na kuitambua kahawa kama bidhaa ya kimkakati chini ya Agenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika.

7. **LINAIOMBA** IACO kutoa ripoti ya utekelezaji wa uamuzi huu na maendeleo yaliyofikiwa wakati wa Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu wa mwaka 2026.

**UAMUZI**
**KUHUSU JUKWAA LA AFRIKA LA UTAMADUNI WA AMANI NA UTULIVU "LUANDA BIENNIAL"**
(***Kipengele Kilichopendekezwa na Jamhuri ya Angola***)
**Doc. EX.CL/1591(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** taarifa fupi iliyowasilishwa na Jamhuri ya Angola kuhusu matayarisho ya Toleo la 4 la Jukwaa la Afrika la Utamaduni wa Amani na Utulivu "Biennale of Luanda", chini ya kaulimbiu "Kuheshimu Yaliyopita, Kuthamini Mafanikio, Kujenga Afrika Tunayoitaka" ambalo litafanyika kwa awamu mbili (2), yaani kuanzia tarehe 2 hadi 4 Julai, na tarehe 12-13 Novemba, 2025, mjini Luanda, Jamhuri ya Angola.

2. **LINAZINGATIA ZAIDI** kipengele kilichopendekezwa na Angola na L**INAPENDEKEZA** rasimu ya uamuzi kujadiliwa na kupitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

## UAMUZI
## KUHUSU SHIRIKA LA WANAWAKE WA AFRIKA JUU YA UENDESHAJI NA UTEKELEZAJI WAKE

**Baraza Kuu,**

1. **LINAKUMBUKA** uamuzi Assembly/AU/Dec.621(XXVIII) wa 2017 unaotoa hadhi ya Shirika Maalumu kwa Shirika la Wanawake wa Afrika (PAWO);

2. **LINAKUMBUKA ZAIDI** jukumu muhimu lililofanywa na PAWO katika kupigania uhuru wa nchi za Afrika, dhidi ya ubaguzi wa rangi, na kudumisha haki za binadamu za Watu wa Afrika popote walipo;

3. **LINAZINGATIA** kazi muhimu iliyofanywa na PAWO katika uundaji wa OAU, Umoja wa Afrika wa leo, kama Taasisi ya Sauti Moja ya Watu wa Afrika na bara;

4. **LINAZINGATIA ZAIDI** haja ya kujumuisha wanawake ili kuziba mapengo, kukuza haki za wanawake, na kuharakisha utekelezaji wa huduma za Serikali;

5. **LINATAMBUA** msaada wa kifedha unaotolewa na Nchi Wanachama na Kamisheni kwa PAWO kupitia Kurugenzi ya Wanawake, Jinsia na Vijana;

6. **LINAZINGATIA KWA WASIWASI** kwamba mgawo wa sasa wa fedha kwa PAWO hautoshi kutokana na mahitaji makubwa na tofauti ya Ofisi tano za Kanda na ushirikishwaji ujao wa diaspora;

7. **LINAAMUA** kujumuisha PAWO katika mchakato wa mfumo wa bajeti ya AU na **LINAIOMBA** Kamisheni na PRC kutenga bajeti ya kutosha, inayotosha kutekeleza shughuli za PAWO kwa kufuata mchakato sahihi;

8. **LINAIOMBA** Kamisheni kutaarifu mkutano ujao wa Baraza kuu mnamo Julai 2025 kuhusu hali ya utekelezaji na uendeshaji wa PAWO kama Shirika Maalumu la AU.

## UAMUZI WA UCHAGUZI NA UTEUZI WA MAKAMISHNA SITA (6) WA KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA

**Baraza la Mawaziri,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Tume ya Uchaguzi na Uteuzi wa Makamishna sita (6) wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika;

2. **LINACHAGUA NA KUTEUA** Makamishna wafuatao wanne (4) wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka minne (4):

| NA. | JINA | KAZI | NCHI | UKANDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bw. Moses Vilakati | Kamishna wa Kilimo, Maendeleo Vijijini, Uchumi wa Buluu na Mazingira Endelevu (ARBE) | Eswatini | Kusini |
| 2 | Bi. Lerato D. Mataboge | Kamishna wa Miundombinu na Nishati (I&E) | Afrika Kusini | Kusini |
| 3 | Balozi. Bankole Adeoye (Bw.) | Kamishna wa Masuala ya Siasa, Amani & Usalama (PAPS) | Nigeria | Magharibi |
| 4 | Balozi. Amma A. Twum- Amoah (Bi.) | Kamishina wa Afya, Masuala ya Binadamu na Maendeleo ya Kijamii (HHS) | Ghana | Magharibi |

3. **LINAWAPONGEZA** Makamishna wapya waliochaguliwa ambao watakula kiapo cha kuingia madarakani mbele ya Mwenyekiti wa Kamisheni;

4. **LINAAMUA** kwamba uchaguzi wa Makamishna wawili (2) wafuatao utafanyika katika Kikao Maalum cha Baraza la Mawaziri:
   - Kamishna wa Maendeleo ya Kiuchumi, Biashara, Utalii, Viwanda na Madini (ETTIM); na
   - Kamishna wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (ESTI).

5. **LINAAMUA** kusisitiza nafasi ya wagombea wa nafasi ya Kamishna wa -ETTIM kwa mgombea mwanaume/mwanamke kutoka **Ukanda wa Kati**, kwa mujibu wa vifungu vya Mkataba wa Kamisheni pamoja na Kanuni za Utaratibu za Mkutano Mkuu;

6. **LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1237(XLIV), ambao unateua wajumbe wa Jopo la Watu Mashuhuri kwa uchaguzi wa 2025 wa Kamisheni na **LINAWAOMBA** Watu Mashuhuri kuendelea na kazi yao, na pale inapolazimu, wakisaidiwa na kampuni huru ya ushauri ya Afrika kulingana na ratiba iliyowekwa kwenye Uamuzi huu.

7. **LINAIDHINISHA** ratiba ifuatayo:
   a) Kamisheni kuwasiliana na Nchi Wanachama kuwasilisha Wagombea ifikapo tarehe 25 Februari;

b) Nchi Wanachama kuwasilishaji Wagombea kutoka Kanda ya Kati Kupitia Kiongizi wa Kanda ifikapo tarehe 7 Machi -2025);
c) Kusambazwa kwa orodha ya wagombea iliyopokelewa kwa Nchi Wanachama ifikapo tarehe 10 Machi 2025;
d) Tathmini ya wagombea inayofanywa na Jopo ifikapo tarehe 21 Machi 2025.
e) Usambazaji wa orodha ya alama za wagombea waliokidhi vigezo kwa Nchi Wanachama ifikapo tarehe 28 Machii 2025;
f) Uchaguzi wa nyadhifa zilizobaki za Tume na nafasi za vyombo vingine utafanyika kabla ya tarehe 15 Aprili 2025 wakati wa Mkutano Maalumu wa Ishirini na Nne wa Baraza Kuu.

8. **LINAIOMBA** Kamisheni kuchukua hatua zote muhimu katika utekelezaji wa Uamuzi huu na **LINAIAGIZA** PRC, ikisaidiwa na Kamati zake ndogo husika, kutoa msaada unaotakiwa katika kubainisha bajeti inayotakiwa.

9. **LINAKASIMISHA** Uongozi wa Baraza Kuu, kupitisha uongezaji unaofaa kwa ratiba ikiwa itakuwa vigumu kufanya uchaguzi ndani ya muda uliopangwa hapo juu.

**UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI WA WAJUMBE WATANO (5) WA BARAZA LA AMANI NA USALAMA LA UMOJA WA AFRIKA**
**Doc. EX.CL/1596(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Tume kuhusu Uchaguzi wa Wajumbe Watano (5) wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

2. **LINACHAGUA** wajumbe[5] wafuatao wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha **miaka mitatu (3):**

| NA. | NCHI | UKANDA |
|---|---|---|
| 1. | Cameroon | Kati |
| 2. | Ethiopia | Mashariki |
| 3. | Eswatini | Kusini |
| 4. | Nigeria | Magharibi |

3. **LINAPENDEKEZA** wajumbe waliochaguliwa wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika katika Mkutano wa Kawaida wa 38 wa Bunge, kwa ajili ya uteuzi.

4. **LINAAMUA** kwamba uchaguzi wa mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kutoka Ukanda wa Kaskazini utafanyika wakati wa Mkutano Maalumu wa Ishirini na Nne wa Baraza Kuu.

[5] **Re-elected for a 2nd term**

**UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA MJUNBE MMOJA (1) WA BARAZA LA ANGA AFRIKA**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Mjunbe Mmoja (1) wa Baraza la Anga Afrika;

2. **LINAAMUA** kuahirisha uchaguzi na uteuzi wa mjumbe mmoja (1) mwanamke wa Baraza la Anga kutoka Ukanda wa Kati hadi katika Mkutano Maalumu wa Ishirini na Nne wa Baraza kuu;

3. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama za Ukanda wa Kati kuwasilisha wagombea wanawake kwa ajili ya Baraza la Anga.

## UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA MAKAMU MWENYEKITI WA BARAZA LA PAU

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afrika (PAU);

2. **LINAMCHAGUA NA KUMTEUA** afuataye kuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la PAU kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

| JINA | JINSIA | NCHI | KANDA |
|---|---|---|---|
| Amani EL-SHARIF* | Ke | Misri | Kaskazini |

***Amechaguliwa kwa awamu ya pili**

## UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA MJUMBE MMOJA (1) WA KAMATI YA WATAALAMU WA AFRIKA KUHUSU HAKI NA USTAWI WA MTOTO

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Mjumbe Mmoja (1) wa Kamati ya Afrika ya Wataalamu kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto.

2. **LINAMCHAGUA na KUMTEUA afuataye** kuwa mjumbe wa ACERWC kwa muhula hadi Februari 2026:

| JINA | JINSIA | NCHI | UKANDA |
|---|---|---|---|
| Joseph Sunday **SINNAH** | Me | Sierra Leone | Magharibi |

# UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA WAJUMBE WATANO (5) WA BODI YA USHAURI YA UMOJA WA AFRIKA YA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa wajumbe watano (5) wa

2. **LINAWACHAGUA NA KUWATEUA** wafuatao kuwa Wajumbe wa AUABC **kwa kipindi cha miaka sita (6):**

| NA | JINA | JINSIA | NCHI | KANDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Benjamini Kiunsi **KAPERA** | Me | Tanzania | Mashariki |
| 2 | Yvonne Mutepuka **CHIBIYA*** | Ke | Zambia | Kusini |
| 3 | Graciano Franscisco **DOMINGOS** | Me | Angola | Kusini |
| 4 | Absatou Ly **DIALLO** | Ke | Senegali | Magharibi |
| 5 | Kwami Edem **SENANU*** | Me | Ghana | Magharibi |

***Amechaguliwa tena kwa muhula wa pili**

**UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA WAJUMBE SITA (6) WA TUME YA UMOJA WA AFRIKA YA SHERIA ZA KIMATAIFA (AUCIL)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamisheni kuhusu uchaguzi na uteuzi wa wajumbe sita (6) wa Tume ya Umoja wa Afrika ya Sheria za Kimataifa (AUCIL);

2. **LINAWACHAGUA na KUWATEUA** wajumbe watano (5) wafuatao wa AUCIL kwa muda wa **miaka mitano (5):**

| NA. | JINA | JINSIA | NCHI | KANDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Narindra Arivelo **RAMANANARIVO*** | Me | Madagaska | Mashariki |
| 2 | Kennedy **GASTORN** | Ke | Tanzania | Mashariki |
| 3 | Mohammed S. **HELAL*** | Me | Misri | Kaskazini |
| 4 | Steven W. **KAYUNI** | Ke | Malawi | Kusini |
| 5 | Jane Gasu **AHETO** | Me | Ghana | Magharibi |

*** Wamechaguliwa kwa awamu ya Pili**

3. **LINAAMUA** kuahirisha uchaguzi na uteuzi wa mwanachama Mmoja (1) wa kiume wa AUCIL kutoka Ukanda wa Magharibi hadi kwenye Mkutano Maalumu wa Ishirini na Nne wa Baraza la Kuu.

# UAMUZI KUHUSU MKATABA WA ENEO HURU LA BIASHARA BARANI AFRIKA (AfCFTA)
## Doc. EX.CL/1603(XLVI)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Taarifa ya Sekretarieti ya AfCFTA kuhusu matokeo ya Mkutano wa Kumi na Tano (15) wa Baraza la Mawaziri wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) wanaohusika na Biashara, uliofanyika kuanzia tarehe 9 - 10 Novemba, Addis Ababa, Ethiopia;

2. **LINAZIPONGEZA** Nchi Zilizoridhia za AfCFTA ambazo zimechapisha kwenye gazeti la serikali au kutangaza ndani ratiba zao zilizopitishwa za ahadi mahususi na KUZISHAURI Nchi Wanachama ambazo bado hawajafanya hivyo, ili kuharakisha mchakato wao wa ndani ili kuharakisha ushirikiano wa bara;

3. **LINAIDHINISHA** agizo kwa Sekretarieti ya AfCFTA kurekebisha utafiti kuhusu Biashara ya Afrika na wahusika wengine kwa kuzingatia mabadiliko ya mahusiano ya kibiashara na kiuchumi kote ulimwenguni;

4. **LINASIHI** Baraza la Mawaziri la AfCFTA kuhitimisha mazungumzo yote yanayosubiri mwisho kufikia 2026;

5. **LINAZINGATIA** kuwa Mkataba wa AfCFTA umeingia katika awamu ya utekelezaji, na linatambua kuwa Sekretarieti itahitaji kuongeza uwezo wa rasilimali;

6. **ZAIDI LINAZINGATIA** mafanikio ya kuanzishwa kwa Mpango wa Biashara ya Kuongozwa (GTI) na jukumu muhimu la Kampuni za Biashara za AfCFTA (ATC) katika kuendeleza ushirikiano wa soko chini ya AfCFTA; na

7. **LINAIDHIHISHA** Biashara Afrika kama mpango mkuu wa AfCFTA ufunguo wa kuendeleza sera za ushirikiano wa soko la bara chini ya AfCFTA na kuendeleza zaidi maslahi ya Sekta ya Kibinafsi katika Bara zima.

8. **LINAIAGIZA** Sekretarieti ya AfCFTA kutoa ripoti ya maendeleo kwenye Mkutano wa saba wa Uratibu wa Nusu Mwaka.

# UAMUZI
# KUHUSU URAIS WA G20 WA AFRIKA KUSINI

**Baraza Kuu,**

1. **LNAKARIBIBISHA KWA MOYO MKUNJUFU Taarifa** ya kina juu ya vipaumbele muhimu na matokeo makuu tarajali yanayoweza kufikiwa ya Urais wa Afrika Kusini wa G20 mwaka 2025.

2. **LINATHIBITISHA TENA k**uiunga mkono kikamilifu Afrika Kusini katika utekelezaji wa majukumu yake kama Rais wa G20 mnamo 2025.

3. **LINAFAHAMU** Mkutano ujao wa ngazi ya juu wa G20 utakaofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwaka 2025 wakati wa Urais wa Afrika Kusini una lengo la kuimarisha ushirikiano wa karibu ambao tayari upo kati ya Afrika Kusini na Kikosi Kazi cha AU cha G20.

4. **LINAIOMBA** Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kutoa ripoti kwa Baraza Kuu, Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Uchumi na Biashara, na STC ya Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano kuhusu utekelezaji wa Urais wa G20 kwa ushirikiano wa karibu na Mratibu wa G20 wa AU.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MKUTANO WA PAMOJA WA KAMATI YA MAWAZIRI KUHUSU KIWANGO CHA TATHMINI NA MICHANGO NA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA TANO WA FEDHA (F15)
# Doc. EX.CL/1608(XLVI)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAPOKEA** Ripoti ya Mkutano wa Pamoja wa Kamati ya Mawaziri kuhusu Kiwango cha Tathmini na Michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15) uliofanyika tarehe 7 Februari 2025.

**A. Kuhusu Hali ya Michango ya Nchi Wanachama kwa Bajeti ya Kawaida na Mfuko wa Amani:**

2. **LINAREJELEA Uamuzi** wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.802(XXXIV) wa Februari 2021 mjini Addis Ababa, Ethiopia, ambapo Mkutano huo uliamua kukasimu mamlaka yake kwa Baraza Kuu, kutumia Utawala wa Uamuzi wa AU, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 23 (1) ya Katiba na Kanuni ya 36 ya Kanuni za Mkutano Mkuu.

3. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuchangia dola za Marekani **172,209,559.83**, sawa na **86%** ya dola za Marekani **200,000,000** mchango uliotathminiwa kwa bajeti ya kawaida ya 2024**.**

4. **PIA LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuchangia tangu 2017, dola za Marekani **341,492,924.84**, katika Mfuko wa Amani wa AU, ikionyesha dhamira ya juu ya Umoja wa Afrika ya kutekeleza kikamilifu Mfuko huo.

5. **AIDHA LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo zilitoa michango kamili ya tathmini zao za mwaka 2024 na **KUZIOMBA** Nchi Wanachama kulipa michango yao iliyotathminiwa ya mwaka 2025 kwa kuzingatia Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Kifedha za AU, kwa kuzingatia tofauti za miaka ya fedha ya Nchi Wanachama.

6. **LINAAMUA** kuweka vikwazo kwa Nchi Wanachama zifuatazo ambazo zimerudi nyuma kwenye malipo ya michango yao iliyotathminiwa**:**

   a. **Vikwazo vya kati: Uganda, Gabon, Burkina Faso, Niger na Mali.**
   b. **Vikwazo vya kina: Guinea.**

B. **Kuhusu Nchi Wanachama zinazokumbwa na hali ya mkwamo nje ya uwezo wao inayozifanya zishindwe kwa muda kulipa michango yao iliyotathminiwa**:

7. **LINAREJELEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1071(XXXV) wa Julai 2019 ambao ulizingatia hali ya usalama na kisiasa ya Somalia na ulizuia kuweka vikwazo kwa kutolipa michango, na ulioomba Kamisheni kushauriana na nchi hiyo ili kukubaliana juu ya

mpango wa malipo wa kufuta malimbikizo ndani ya miaka minne (4) tangu kupitishwa kwa Uamuzi huo**.**

8. **ZAIDI LINAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.752(XXXIII) wa Februari 2020 ambalo ulizingatia ombi la Jamhuri ya Burundi na changamoto ambazo nchi ilikumbana nazo katika kufikia michango yake ya kila mwaka ya Umoja wa Afrika, na kuitaka Kamisheni ishirikiane na Nchi Wanachama zinazokabiliwa na matatizo ya kulipa michango yao kwa Umoja wa Afrika na zile zinazodaiwa malimbikizo ya miaka miwili (2) au zaidi ili kukubaliana utaratibu wa kulipa malimbikizo ya madeni yao.

9. **PIA LINAREJELEA** UAMUZI EX.CL/Dec.1119(XXXVIII) wa Februari 2021 ambao ulizingatia ombi la Jamhuri ya Sudan kuhusu haja ya kukagua mchango wake uliotathminiwa na kuomba Kamisheni kushauriana na Jamhuri ya Sudan kwa kuzingatia Kiwango cha Tathmini cha sasa ili kukubaliana kuhusu mpango wa Malipo wa kulipa malimbikizo ya madeni haraka iwezekanavyo, ndani ya miaka minne (4) baada ya kupitishwa kwa Uamuzi huo.

10. **LINAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.802(XXXIV) wa Februari 2021 ambao uliidhinisha mipango ya malipo ya Jamhuri ya Shirikisho la Somalia na Jamhuri ya Burundi kufuta malimbikizo yao.

11. **LINAREJELEA ZAIDI** Uamuzi EX.CL/Dec.1272(XLV) wa Julai 2024 ambao:

    a. Lilizingatia ombi la Jamhuri ya Shirikisho la Somalia la kufanyia marekebisho mpango wake wa malipo na kuiomba Kamisheni na Jamhuri ya Shirikisho la Somalia kukubaliana kuhusu mpango wa malipo uliorekebishwa na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu mnamo Februari 2025.

    b. Liliidhinisha Uamuzi EX.CL/Dec.1119(XXXVIII) wa Februari 2021 na, kwa kuzingatia changamoto kubwa za kisiasa na kiusalama ambazo Sudan inaendelea kukabiliana nazo, liliiomba Kamisheni hiyo kuwasilisha ripoti ya hali hiyo kwa Baraza Kuu katika mkutano wake wa Februari 2025, likijumuisha hatua zilizochukuliwa kuhusu kukubaliana juu ya mpango wa malipo na Sudan, ili kuzingatiwa zaidi na kufanyiwa Uamuzi.

12. **LINAZINGATIA NA KUIDHINISHA:**

    a. Mpango wa malipo uliopendekezwa na Jamhuri ya Shirikisho la Somalia kulipa malimbikizo yake ya jumla ya Dola za Marekani 1,722,316.95 iliyokokotolewa kufikia tarehe 1 Januari 2025, katika kipindi cha miaka mitano pamoja na michango yake iliyotathminiwa kila mwaka kuanzia 2025 hadi 2029.

    b. Ombi la Jamhuri ya Burundi la nyongeza ya miezi sita (6) kwenye mpango wake wa malipo hadi tarehe 30 Juni 2025 kulipa malimbikizo yake yanayofikia Dola za Marekani 1,306,050.97.

13. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamisheni kuhusu hali ya Jamhuri ya Sudan pamoja na hatua zilizochukuliwa ili kukubaliana kuhusu mpango wa malipo na **LINAIOMBA** Kamisheni na Jamhuri ya Sudan kukamilisha majadiliano kuhusu mpango wa malipo na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu mwezi Julai 2025.

### C. Juu ya uwekaji wa kiwango kipya cha tathmini

14. **AIDHA LINAZINGATIA** kuwa 2026 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa kiwango cha sasa cha tathmini ya michango ya Nchi Wanachama (2024-2026) na **LINAIAGIZA** Kamisheni kuanza mchakato wa kuweka kiwango kipya cha tathmini ili kuzingatiwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu mnamo Februari 2026, kufuatia taratibu zinazostahili.

**UAMUZI WA KAMATI YA MAWAZIRI KUHUSU UFUATILIAJI WA AJENDA 2063**
**Doc. EX.CL/1610(XLVI)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAREJELEA** Uamuzi wake ***EX.CL/Dec.998(XXXII),*** ulioanzisha Kamati ya Mawaziri kuhusu utekelezaji wa Ajenda 2063 na **LINATAMBUA** jukumu lake muhimu katika kuongoza na kusimamia utekelezaji bora wa Ajenda 2063;

2. **LINAREJELEA ZAIDI** uamuzi EX.CL/Dec.1260(XLIV) ambao kupitia huo STYIP ilipitishwa na Baraza Kuu iliomba kuongezwa kwa Mradi Maalumu wa kamisheni kwa kushirikiana na AUDA-NEPAD ili kuuingiza kwenye mipango ya ndani, kujenga uwezo, kufuatilia na kuratibu utendaji na utoaji taarifa kuhusu Ajenda 2063. Pia **ILIIAGIZA** Kamisheni na AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na taasisi husika za Afrika kukamilisha kazi za mfuko wa maendeleo wa Ajenda 2063 na kuiwasilisha ili kujadiliwa na Kamati ya Mawaziri kuhusu Ajenda 2063 miongoni mwa miundo mingine;

3. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji na linapongeza hatua iliyofikiwa na Kamisheni na Kikosi Kazi cha Kitaalamu katika kutengeneza mifumo na nyenzo husika;

4. **LINAPITISHA** mifumo na nyenzo muhimu za Ajenda 2063 STYIP, ikijumuisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini, Kitabu cha Viashirio vya Msingi, Miongozo ya Kutumia ndani ya nchi, Mkakati wa Mawasiliano, Uhamasishaji na Chapa na Jukwaa la Kidijitali;

5. **LINAPENDEKEZA** kuanzishwa kwa Ajenda 2063 kama kipengele cha kawaida katika ajenda ya Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali, pamoja na ajenda zote za STCs na mikutano yote ya kisheria ya taasisi za AU ili kuimarisha uwajibikaji, kuimarisha umiliki, na kuendeleza kasi katika utekelezaji wake;

6. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuweka kipaumbele kwenye mikakati ya Utafutaji wa Rasilimali za Ndani kwa kutumia msaada wa kitaalamu, mbinu bunifu za ufadhili na ushirikiano wa wabia;

7. **LINAIAGIZA** Kamisheni na AUDA-NEPAD kwa kushirikiana na Nchi Wanachama kukamilisha upembuzi yakinifu wa kuundwa kwa Mfuko wa Ajenda 2063 na Mkutano wa Baraza Kuu mwezi Julai 2025. Na kufanya kazi kwa ajili ya Ajenda ya Maendeleo ya Umoja wa Afrika 2063 kama jitihada muhimu za kutafuta rasilimali ili kuharakisha utekelezaji wa mpango wa STYIP;

8. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama, RECs, na Vyombo vya AU na wabia kurekebisha kadiri inavyofaa nyenzo za matumizi ya ndani, huku ikijumuisha Ajenda 2063 katika mipango ya maendeleo, na inaelekeza Kamisheni na vyombo

vya kitaalamu vya AU na taasisi husika kuimarisha mchakato wa matumizi ya ndani kwa kuweka mazingira mazuri kwa watafiti, wataalam, wanataaluma, na Waafrika wote, ikiwa ni pamoja na Diaspora na kuandaa miundombinu, mbinu na mikakati yenye ubunifu ambazo zitatoa suluhu za Kiafrika kwa matatizo ya Afrika, ambazo zitafanyiwa majaribio na kuigwa;

9. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama na RECs kuoanisha bajeti zao za kitaifa na kikanda na Agenda 2063 Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP);

10. **LINAPITISHA** Mkakati wa Mawasiliano wa Ajenda 2063 ikijumuisha Jukwaa la Kidijitali kama sehemu ya nyenzo muhimu za kuendeleza STYIP;

11. **LINAIAGIZA** Kamisheni kwa ushirikiano wa karibu na Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji kupendekeza kaulimbiu inayowiana na malengo saba ya Ajenda 2063 STYIP kama Umoja wa Afrika inayozunguka “Kaulimbiu ya Mwaka” kuanzia 2026, na **LINAAGIZA** zaidi kuwa Siku ya Afrika (25 Mei) na Siku ya Umoja wa Afrika (9 Septemba) zitumike kama siku za kuadhimisha Ajenda 2063.

12. **LINAIAGIZA** Kamisheni kufanya mapitio ya kina ya utawala, uongozi, na miundo ya kitaalamu ya Ajenda 2063 ili kuimarisha uwiano na ufanisi. Hii ni pamoja na kutathmini masuala ya kisheria, kufafanua majukumu ya kamati zilizopo, na kuchunguza uwezekano wa kuanzisha kamati ndogo ya PRC kuhusu Ajenda 2063 kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji ili kujadiliwa. Baada ya hapo matokeo yawasilishwe kwa Baraza Kuu kabla ya Julai 2025;

13. **LINAMWOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuimarisha Ofisi ya Mipango Mikakati na Utekelezaji kwa kutenga rasilimali watu na fedha zaidi na kutaka nchi Wanachama kuongeza mchango kwenye Mradi Maalum (kutumika ndani ya nchi, mawasiliano, ufuatiliaji na tathmini, utafutaji wa rasilimali);

14. **LINAAMUA** kurasimisha Kikosi Kazi cha Kitaalamu (TWG) katika Ajenda 2063 chini ya Ofisi ya Mipango Mikakati na Utekelezaji kwa ajili ya utekelezaji bora wa Mradi Maalumu;

    **LINASISITIZA** haja ya ushiriki wa wajumbe wote wa Kamati ya Mawaziri na Mabalozi ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Ajenda 2063 katika mikutano ya kisheria ya Kamati. **LINAZIOMBA** Kanda zote kuwateua wawakilishi wao katika Kamati za Mawaziri na Mabalozi na kusisitiza haja ya wajumbe wa kamati hizo kutoa taarifa mara kwa mara kwenye kanda zao kuhusu kazi za Kamati; na

15. **LIKIREJELEA** uamuzi EX.CL/Dec.1260(XLIV) **LINAPENDEKEZA** kuitishwa kwa Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Wakuu wa Nchi na Serikali utakaofanyika mwaka 2025. Hii itaendesha uangalizi wa kimkakati, kuhakikisha uwiano kati ya nchi wanachama, jumuiya za kiuchumi za kanda na kuendeleza kasi katika utekelezaji wa Ajenda 2063.

# UAMUZI
# KUHUSU KUMALIZIKA KWA MCHAKATO WA UTEUZI WA KIKUNDI HURU CHA TATHMINI YA MFUKO WA AMANI WA UMOJA WA AFRIKA

**Baraza Kuu,**

1. **LINAREJELEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1233(XLIV) wa Mkutano wa Arobaini na Nne wa Kawaida uliofanyika Februari 2024 mjini Addis Ababa, Ethiopia ukiiomba Kamisheni kufanya uteuzi wa Kikundi Huru cha Tathmini kupitia Jopo la Waafrika Mashuhuri ili kuhakikisha mchakato wa uteuzi wa haki na uwazi na kuzitaarifu rasmi Nchi Wanachama zilizoteuliwa na kutoa wito huku zikitambua uwezo wa Nchi Wanachama wa kupendekeza uteuzi.

2. **LINAZINGATIA** ripoti ya Jopo la Waafrika Mashuhuri na **LINAWAPONGEZA** wajumbe wa Jopo hilo kwa mchango wao katika kuisaidia Kamisheni kwa kuteua wagombea watano (5) wenye sifa zinazostahili kuteuliwa na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Amani.

3. **LINATAMBUA** changamoto zilizojitokeza kwenye Jopo katika kupata wagombea wote kumi (10) wenye sifa za kushika nafasi za ujumbe wa Kikundi Huru cha Tathmini.

4. **LINAPENDEKEZA** kuwa Kamisheni iendelee kufanya kazi na Jopo la Waafrika Mashuhuri na **KUTOA WITO** wa maombi ya wajumbe watano (5) waliosalia katika kanda (Kati (2) Kusini (2) na Magharibi (1)) ambazo wagombea wenye sifa hawakubainishwa katika mchakato wa awali wa uteuzi.

5. **AIDHA LINAPENDEKEZA** kuwa Kamisheni iwajumuishe wagombea watano waliobainishwa na kukamilisha mchakato wa uteuzi wa wajumbe watano wa ziada wa Kikundi Huru cha Tathmini kwa ajili ya kuteuliwa na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Amani na kuripoti kwa Baraza Kuu mnamo Julai 2025.

# UAMUZI KUHUSU MAOMBI YA KUGOMBEA YA AFRIKA NDANI YA MFUMO WA KIMATAIFA

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati ya Mawaziri kuhusu Maombi ya kugombea ya Afrika ndani ya Mfumo wa Kimataifa;

2. **LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Ghana (Ukanda wa Afrika ya Magharibi) kwa kuteuliwa kwa aliyekuwa Waziri wake wa Mambo ya Nje kuwa **Katibu Mkuu** ajaye wa **Jumuiya ya Madola**, wakati wa uchaguzi uliofanyika Oktoba 2024 nchini Samoa;

3. **PIA LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ukanda wa Afrika Mashariki) kwa kumchagua raia wake kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya WHO-Afrika; na **LINATOA** salamu za dhati za rambirambi kwa Serikali na Wananchi wa Tanzania kwa kuondokewa na mgombea huyo miezi mitatu baada ya kuchaguliwa kwake;

4. **LINAYAOMBA** Makundi ya Afrika mjini New York na Geneva kufanya kazi kwa karibu na Sekretarieti ya Kamati, inayosimamiwa na Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (DPAPS) na kuoanisha miongozo yao ya kazi ya ndani na Kanuni za Utaratibu zilizopitishwa;

5. **LINAIDHINISHA MAOMBI YA SERIKALI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

   **A.** Kwa ajili ya kuwa mwenyeji wa **Ofisi ya Kanda ya Afrika ya Mkutano wa The Hague kuhusu Sheria Binafsi za Kimataifa kwa kipindi cha 2025-2027**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Machi 2025, New York, Marekani, maombi ya:

   - **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

   **B.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Baraza la Kiuchumi na Kijamii la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, Marekani, wagombea:

   - **Jamhuri ya Burundi** (Kanda ya Afrika ya Kati)
   - **Jamhuri ya Chad** (Kanda ya Afrika ya Kati)
   - **Jamhuri ya Sierra Leone** (Kanda ya Afrika Magharibi)
   - **Jamhuri ya Msumbiji** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

   **C.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa Tume ya Takwimu kwa kipindi cha 2026-2029, kwa uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

   - **Jamhuri ya Burundi** (Kanda ya Afrika ya Kati)
   - **Jamhuri ya Eritrea** (Kanda ya Afrika Mashariki)
   - **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

- **Jamhuri ya Benin** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**D.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Tume ya Idadi ya Watu na Maendeleo kwa kipindi cha 2026-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Cameroon** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**E.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa Tume ya Hadhi ya Wanawake (CSW) kwa kipindi cha 2027-2030, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Nchi Mwanachama** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Cabo Verde** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

***NB: Nafasi tano (5) zimetengwa kwa ajili ya Afrika. Kanda ya Afrika Mashariki inashauriwa kushauriana na kukubaliana kuhusu Mgombea mmoja. Kanda ya Afrika ya Kusini inahimizwa kumteua mgombea wake.***

**F.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Tume ya Umoja wa Mataifa ya Dawa za Kulevya (CND) kwa kipindi cha 2026-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Cote d'Ivoire** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Nchi Mwanachama** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Ghana** (Kanda wa Afrika ya Magharibi)

**G.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Kamati ya Programu na Uratibu (CPC) kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**H.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Bodi Tendaji ya Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**I.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Bodi Tendaji ya UNDP, UNFPA na UNOPS kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Rwanda** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**J.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Bodi Tendaji ya Shirika la Chakula Duniani (WFP) kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Nchi Mwanachama** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**K.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa **Programu ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu VVU/UKIMWI (UNAIDS) kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Aprili 2025, New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**L.** Kwa Nafasi ya Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha 2026-2028, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2025, New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Rwanda** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Nchi Mwanachama** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Inasubiriwa** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**M.** Kwa Nafasi ya Makamu wa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa wakati wa Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kwa uchaguzi utakaofanyika Juni 2025, New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Tunisia** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Ufalme wa Lesotho** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)

- **Jamhuri ya Cabo Verde** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**N.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza Kuu la Shirika la Utalii Duniani (UN-WTO), kwa kipindi cha 2025-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2025 huko Abuja, Nigeria, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shelisheli (Kanda ya Afrika Mashariki)**
- **Ufalme wa Morocco (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)**

**O.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya UNESCO kwa kipindi cha 2025-2027**, kwa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2025, Samarkand, Uzbekistan, maombi ya:

- **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Togo** (Kanda ya Afrika ya Magharibi)

**P.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2025, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Mauritius** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Zambia** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Kanda ya Afrika ya Kusini). ***Kuchaguliwa tena***

***NB: Nafasi nne (4) zimetengwa kwa ajili ya Afrika. Kundi la Afrika mjini New York linaombwa kutoa ushauri juu ya nini kifanyike***

**Q.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) "Kategoria ya 3" kwa kipindi cha 2025-2028,** wakati wa uchaguzi utakaofanyika Septemba 2025, Montreal, Canada, maombi ya**:**

- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Ufalme wa Morocco - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Guinea ya Ikweta - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Uganda - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Angola - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini - Sehemu ya III** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

***NB: Orodha hii iliidhinishwa na AFCAC kupitia Tamko la Kidiplomasia Na.: AC-HQ/1.1-561 la tarehe 13 Desemba 2024***

**R.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Utawala na Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa kipindi cha 2026-2029**, wakati wa uchaguzi utakaofanyika Septemba 2025, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**S.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO) "Kategoria C" kwa kipindi cha 2025-2028**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Novemba 2025, London, Uingereza, maombi ya:

- **Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia la Ethiopia** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria** (Kanda ya Afrika ya Magharibi)

**6. LINAZINGATIA MAOMBI YA SERIKALI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**A.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2027-2029**, kwa uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2026 huko New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**B.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya UNESCO kwa kipindi cha 2027-2031**, kwa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026, Paris, Ufaransa, maombi ya:

- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**C.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Mamlaka ya Kimataifa ya Bahari (ISA) kipindi cha 2027-2030**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026, Kingston, Jamaika, maombi ya:

- **Jamhuri ya Ghana** (Kanda ya Afrika Magharibi) ***Kuchaguliwa tena***

**D.** Kwa Nafasi ya **Mwanachama Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2028-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2027, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Guinea Bissau** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Ufalme wa Morocco** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Nchi ya Libya** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

***NB: Nafasi mbili (2) zimetengwa kwa ajili ya Afrika. Kundi la Afrika mjini New York linaombwa kutoa ushauri juu ya nini kifanyike***

**E.** Kwa Nafasi ya **Mwanachama Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2029-2030,** kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2028, New York, Marekani, maombi ya**:**

- **Jamhuri ya Uganda** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**F.** Kwa Nafasi ya **Mwanachama Asiyekuwa wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2031-2032**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2030, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**G.** Kwa Nafasi ya **Mwanachama Asiyekuwa wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2032-2033**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2031, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania** (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

**7. LINAIDHINISHA MAOMBI BINAFSI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**A.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria za Bahari (ITLOS) kwa kipindi cha 2026-2035**, uliopangwa kufanyika Juni 2025, New York, Marekani, maombi ya:

- **Dkt. Sylvia Adusu** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika Magharibi)

**B.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kipindi cha 2025-2030**, kwa uchaguzi utakaofanyika Mei 2025, mjini Abidjan, Côte d'Ivoire, maombi ya:

- **Dkt. Bajabulile Swazi Tshabalala** wa Jamhuri ya Afrika Kusini (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Dkt. Samuel Munzele Maimbo** wa Jamhuri ya Zambia (Kanda ya Afrika ya Kusini)

- **Dkt. Sidi Ould Tah** wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Dkt. Amadou Hott** wa Jamhuri ya Senegal (Kanda ya Afrika Magharibi)

***NB. Kanda zinashauriwa kushauriana na kukubaliana kuhusu Mgombea mmoja***

**C.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani (UN-WTO), kwa kipindi cha 2025-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Mei 2025, Madrid, Hispania, maombi ya:

- **Balozi Muhammed Adam** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika ya Magharibi)

**D.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Kupinga Mateso (CAT), kwa kipindi cha 2026-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Julai 2025, Geneva, Uswisi, maombi ya:

- **Bw. Abderrazak Rouwane** wa Ufalme wa Morocco (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

**E.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Kutokomeza Ubaguzi wa Rangi (CERD), kwa kipindi cha 2026-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2025, New York, Marekani, maombi ya:

- **Bw. Diaby Bakari Sidiki** wa Cote D'Ivoire (Kanda ya Afrika ya Magharibi) **Kuchaguliwa tena**
- **Bi. Mazalo Tebie Amoussou-Kouetete** wa Jamhuri ya Togo (Kanda ya Afrika ya Magharibi)
- **Jaji Regine Esseneme** wa Jamhuri ya Cameroon (Kanda ya Afrika ya Kati)

**F.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Jukwaa la Kudumu la Umoja wa Mataifa kuhusu Masuala ya Jamii za Wenyeji (UNPFII), kwa kipindi cha 2026-2030**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2025, New York, Marekani, maombi ya:

- **Bi. Anne-Chantal Nama** wa Jamhuri ya Cameroon (Kanda ya Afrika ya Kati)

**G.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Usafiri wa Anga (ANC) la Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) kwa kipindi cha 2025-2027**, wakati wa uchaguzi utakaofanyika Septemba 2025, Montreal, Canada, maombi ya:

- **Bw. Charles Kouadio Kanga** wa Cote d'Ivoire (Kanda ya Afrika ya Magharibi)
- **Jina litawasilishwa** na Jamhuri ya Uganda (Kanda ya Afrika Mashariki)

***NB: Orodha hii iliidhinishwa na AFCAC kupitia Tamko la Kidiplomasia Na.: AC-HQ/1.1-561 la tarehe 13 Desemba 2024***

**H.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Umoja wa Posta Duniani (UPU) katika kipindi cha 2025-2029**, wakati wa uchaguzi utakaofanyika Septemba 2025, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu, maombi ya:

- **Bw. Isaac Gnamba-Yao** wa Jamhuri ya Côte d'Ivoire (Kanda ya Afrika ya Magharibi)

**I.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Masuala ya Utawala na Bajeti (ACABQ) kwa kipindi cha 2027-2030**, wakati wa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026, New York, Marekani, maombi ya:

- **Bw. Adou Mohamed Ali** Jamhuri ya Djibouti (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Balozi Osama Abdelkhalek** wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Balozi Joseph Masila** wa Jamhuri ya Kenya (Kanda ya Afrika Mashariki)

**8. LINAPOKEA TAARIFA YA WAGOMBEA BINAFSI WAPYA WALIOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**J.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) kwa kipindi cha 2027-2030**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2026, New York, Marekani, maombi ya:

- **Dkt. Brenda Akia** wa Jamhuri ya Uganda (Kanda ya Afrika Mashariki) <u>**kuchaguliwa tena**</u>

**K.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Jaji wa Mahakama ya Kimataifa (ICJ) kwa kipindi cha 2027-2032**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika katika robo ya 2026, New York, Marekani, maombi ya:

- **Dkt. Olufemi Elias** wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (Kanda ya Afrika ya Magharibi)
- **Dkt. Charles Chemor Jalloh** wa Jamhuri ya Sierra Leone (Kanda ya Afrika ya Magharibi)

**L.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe na Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Mataifa ya Utumishi wa Umma (ICSC) kwa kipindi cha 2027-2030**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026, New York, Marekani, maombi ya:

- **Bw. Ali Ayad Ali Kurer** wa Nchi ya Libya (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)
- **Balozi Andrew Gbebay Bangali** wa Jamhuri ya Sierra Leone (Kanda ya Afrika ya Magharibi)

- **Balozi Zéphyrin Maniratanga** wa Jamhuri ya Burundi (Kanda ya Afrika ya Kati)

***NB: Nafasi moja (1). Kanda zote mbili zinashauriwa kushauriana na kukubaliana kuhusu mgombea mmoja kwa wadhifa huu muhimu. Kundi la Afrika mjini New York linaombwa kutoa ushauri juu ya nini kifanyike***

## 9. KUHUSU MASUALA MENGINE

A. **LINAPONGEZA** kazi ya Sekretarieti ya Kamati ya Mawaziri kuhusu Wagombea wa Afrika ndani ya Mfumo wa Kimataifa na Sekretarieti yake chini ya uongozi wa Kamishna wa Masuala ya Siasa, Amani na Usalama;

B. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama wa AU kuendelea kufanya uungaji mkono unaohitajika wa kisiasa kwa Kamati kwa kuzingatia mshikamano wetu wa Kiafrika na kwa lengo la jumla la kuhakikisha uwepo thabiti wa Waafrika ndani ya Mfumo wa Kimataifa;

C. **LINAIAGIZA** Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) kuweka mgao wa kutosha wa bajeti na rasilimali watu ili kusaidia shughuli za Kamati ya Mawaziri kuhusu maombi ya Kugombea ya Afrika ndani ya Mfumo wa Kimataifa;

D. **LINAYAOMBA** Makundi ya Afrika kuoanisha Muundo na Miongozo yao na Kanuni za Uendeshaji zilizopitishwa za Kamati ya Mawaziri;

E. **PIA LINAIOMBA** Kamisheni kuendelea na mpango wa *E-Portal* na kuandaa mwongozo wa mafunzo na kuendeleza programu elekezi zinazoendelea kwa Nchi Wanachama wa AU.